**8 MEI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 8 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao cha Ishirini na Moja.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**8 MEI, 2024**

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Meatu, aulize swali lake.

Na. 272

**Ujenzi wa Uzio Shule ya Sekondari ya Nyalanja – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Shule ya Sekondari ya Nyalanja Meatu ili kurahisisha ulinzi wa mali na wanafunzi wa bweni wapatao 600?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024, Serikali ilipeleka shilingi milioni 916.2 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali yakiwemo madarasa 14, mabweni 4 na matundu ya vyoo 22 katika shule ya Sekondari Nyalanja kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa uzio kwa ajili ya ulinzi wa mali na wanafunzi wa bweni. Hata hivyo, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni ujenzi wa miundombinu ya msingi inayowezesha kuongeza nafasi za udahili wa wanafunzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais

wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na kipaumbele chake toka akiwa Makamu wa Rais cha kuongeza mabweni ili kuongeza idadi zaidi ya watoto wa kike kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita. Ni zaidi ya mabweni manne tumepewa matano, sasa basi kutokana na kutoka bweni moja hadi mabweni saba kuna ongezeko la watoto wengi zaidi, katika miundombinu ya msingi. Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja ya kujenga sasa maktaba katika shule hiyo maalum ya wasichana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kutokana na wale watoto waliokuwepo 80 hatuna bwalo katika miundombinu ya msingi. Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kujenga bwalo katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyalanja? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba Shule ya Sekondari ya Nyalanja katika Halmashauri ya Meatu ni moja ya shule ambazo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, ujenzi wa mabweni na mabweni matano yamejengwa na yanatumika na wanafunzi. Kwa hivyo, idadi ya wanafunzi imeongezeka na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye mpango wa *SEQUIP* awamu hii tumeshatenga fedha kwa ajili ya kujenga bwalo pamoja na maktaba katika Shule ya Sekondari ya Njalanja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari ya Bukongo Jimboni Ukerewe inachukua watoto wa kike kwa kidato cha tano na sita, lakini haina uzio, jambo ambalo limekuwa na athari kubwa sana kwa namna mbalimbali kwa watoto hawa. Je, ni lini Serikali itatenga fedha na kujenga uzio kwenye shule hii ya Sekondari ya Bukongo? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka vipaumbele katika ujenzi wa miundombinu ya elimu, tumeanza na ujenzi wa madarasa ili tuweze kuwa na uhakika watoto wetu wote wenye sifa za kwenda shule waingie madarasani. Kazi hiyo imefanyika kwa ufanisi mkubwa tumejenga mabweni na hivi sasa tunakwenda kujenga uzio katika shule zile ambazo zina mazingira hatarishi zaidi kwa wanafunzi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapoanza mpango wa ujenzi wa uzio katika shule hizo, tutatoa kipaumbele shule hii katika Halmashauri ya Ukerewe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 273

**Ujenzi wa Barabara ya Mwendokasi Dar es Salaam**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mwendokasi inayotoka Kigogo - Tabata Dampo hadi Segerea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka ya Kigogo - Tabata Dampo hadi Segerea ni miongoni mwa barabara ambazo zimepangwa kujengwa katika awamu ya tano ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka *(Bus Rapid Transit – BRT)*. Awamu hii ya tano inajumuisha Barabara ya Nelson Mandela kutoka Ubungo hadi Daraja la

Mwalimu Nyerere (Daraja la Kigamboni) na Tabata – Segerea hadi Kigogo. Kwa sasa, taratibu za kupata mkandarasi zinaendelea ambapo Mhandisi Mshauri atakayesimamia ujenzi ameshapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa fedha za ujenzi wa barabara hiyo ambayo ni miongoni mwa barabara zitakazojengwa katika awamu ya tano, zipo kupitia Washirika wa Maendeleo wa Ufaransa *(AFD)*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Massaburi.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu yenye matumaini ya Serikali nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi hii na hasa katika miundombinu ya barabara. Ukiangalia Barabara ya Nyerere mpaka Gongo la Mboto kazi inaenda kwa kasi sana, tunashukuru. Pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Mwendokasi kutoka Segerea kuelekea Kinyerezi, Malamba Mawili, mpaka Stendi Kuu ya Mabasi kule Mbezi kwa Magufuli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani pia wa kujenga Barabara ya Mwendokasi kutoka Gongo la Mboto, Pugu, Chanika, Msongola, Chamazi na kuunganisha na Barabara ya Mbagala? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa Barabara ya Matumbi - Segerea ambapo barabara haitaingia kwenye awamu ya tano ya utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka. Ujenzi wa Barabara hii ya Segerea - Malamba Mawili hadi

Stendi ya Magufuli itaingia kwenye awamu ya saba na ya nane ya Mradi wa *BRT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kuhusiana na Barabara ya Gongo la Mboto - Chanika – Msongola - Chamazi mpaka Mbagala, tayari Serikali imeshafanya tathmini na itaingiza ujenzi wa barabara hizi kwenye awamu ya saba na ya nane na hivi sasa tayari Mhandisi Mshauri ameshapatikana na kazi iliyobaki sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa barabara hizo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo nimekuona.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Barabara ya Mwendokasi inayotoka Gerezani, Kariakoo mpaka Mbagala itafunguliwa na mabasi kuanza kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana kwa kujenga Barabara ya Mwendokasi toka Gerezani kwenda Mbagala. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ile iko hatua za mwisho kabisa na hivi karibuni itaanza kutumika kwa ajili ya kusafirisha wananchi katika eneo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 274

**Hitaji la Dawa Katika Zahanati, Vituo Vya Afya na Hospitali za Mkoa wa Mara**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha dawa zinapatikana na kukidhi mahitaji katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Mkoa wa Mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilitoa shilingi bilioni 266.7 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya katika ngazi ya afya ya msingi. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 200 zilikuwa za ununuzi wa dawa na vitendanishi na shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaatiba. Aidha, Mkoa wa Mara ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 4.67 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi kupitia Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* na washitiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya dawa na vifaatiba ambapo imetenga shilingi bilioni 322.3 kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma ngazi ya afya ya msingi. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 205 ni kwa ajili ya dawa na vitendanishi na shilingi bilioni 117.3 kwa ajili ya vifaa na vifaatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2024, Mkoa wa Mara tayari umepokea shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya vifaa na vifaatiba. Aidha, kumekuwa na ongezeko la upatikanaji wa dawa kwenye vituo katika Mkoa wa Mara kutoka 88% Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi 90.01% Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ghati Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kumekuwa na tatizo la *MSD* kupeleka madawa kwenye hospitali, vituo vya afya yanayokaribia kwisha muda wake. Je, Serikali ina mkakati gani wa

kuhakikisha tatizo hili au jambo hili linamalizika kabisa ili lisilete madhara kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kituo cha Afya cha Muriba katika Jimbo la Tarime Vijijini kinahudumia wananchi wa Kata tano ambao idadi yao ni 73,000 na zaidi, lakini idadi ya dawa zinazopelekwa ni za kuhudumia wananchi wa Kata moja yaani wananchi 14,000. Je, ni kwa nini Serikali isipeleke dawa kulingana na idadi ya watu wanaohudumiwa pale? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishakubaliana Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya kuhusiana na dawa zinazopelekwa kwenye vituo vyetu kuwa na muda mrefu kabla hazijafikia *expiring date* yake. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tangu Mwaka wa Fedha 2021/2022, tayari kwa kiasi kikubwa sana dawa zinazopelekwa kwenye vituo vyetu angalau zina miezi 12 kabla ya ku-*expire* na tutaendelea kuhakikisha kwamba suala hili linasimamiwa hivyo ili wananchi wetu wapate dawa salama pia ziweze kutumika badala ya kuharibika zikiwa vituoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wakati tunapeleka dawa kwenye vituo vya afya, hatuangalii kituo cha afya kiko katika Kata ipi kwa maana kwamba hatuweki mipaka kwamba wananchi wa kata ile tu ndiyo watapata huduma, tunaangalia *catchment population* ya wananchi wote hata kama ni kata tano, sita zinapata huduma katika kituo kile basi tunahakikisha tunapeleka fedha kwa ajili ya dawa zinazotosha wananchi wote ambao wanapata huduma ile. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutakiangalia kituo hicho cha afya ili tuweze kukiongezea pia bajeti ili kihudumie vizuri wananchi wa kata za Jirani. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso nimekuona.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Karatu tumepata Hospitali mpya ya Wilaya lakini bado kuna upungufu wa vifaa na rasilimali watu. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha hospitali hiyo inapata mahitaji hayo ili kuwepo na ufanisi katika utoaji wa huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imejenga Hospitali mpya ya Halmashauri ya Karatu na Serikali inatambua kwamba kweli kuna upungufu wa watumishi na vifaatiba. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwanza tumeshapeleka fedha zaidi ya shilingi milioni 800 katika Halmashauri ya Karatu kwa ajili ya kununua vifaatiba na vituo vingine vya afya na zahanati pia tutaendelea kupeleka fedha hiyo katika mwaka wa fedha huu na mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na watumishi tayari Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa kibali cha ajira ya watumishi zaidi ya 46,000. Watumishi wa Sekta ya Afya ni miongoni mwa watumishi watakaoajiriwa, tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwa Hospitali ya Halmashauri ya Karatu ili itoe huduma bora zaidi kwa wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma na Mheshimiwa Mwita Getere niliwaona.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, Serikali ni lini itawasaidia wastaafu ambao wameambiwa bima zao zimesitishwa ambapo na wao wanaendelea kuumwa hawapati dawa huko kwenye sehemu zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umemwelewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki ya wastaafu kuendelea kupata huduma za afya kupitia bima. Naomba tulichukue jambo hili, tuweze kufuatilia ni wastaafu gani ambao wamepata changamoto hiyo. Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tutalifanyia kazi ili wazee hawa wapate haki yao ya matibabu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere nimekuona, Mwita Getere nimekuita au hukusimama?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Hunyari, Kituo cha afya Mgeta na Kituo cha Afya Ikizu mara nyingi sana vinakosa dawa na mahitaji maalum kwenye maeneo yao. Je, ni lini Serikali itapeleka dawa kwenye vituo hivyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Afya vya Mgeta, Hunyari na kituo kingine ambacho amekitaja ni miongoni mwa vituo ambavyo tayari Serikali ilishaviweka kwenye mpango wa kuhakikisha kwamba vinapata dawa zote za msingi, dawa zote muhimu kwa 100%. Naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuhakikisha anakaa na Mganga Mkuu wa Halmashauri na Mganga Mkuu wa Mkoa kufanya tathmini ya upatikanaji wa dawa na kuona dawa ambazo zinapungua ili waweze kuzinunua haraka iwezekanavyo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafuatilia hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe aulize swali lake.

Na. 275

**Kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma**

**MHE. EDWIN E. SWALE** aliuliza:-

Je Serikali ina Mkakati gani wa kuboresha maslahi ya watumishi wa umma nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza hatua na afua mbalimbali za kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kwa uchache, naomba nizitaje.

Mosi, Julai, 2022 Serikali iliongeza kima cha chini cha Mishahara kwa Watumishi wa Umma kwa 23.3%;

Pili, Serikali imeweka nyongeza ya mwaka ya mishahara *(annual salary increment)* ambapo jumla ya shilingi bilioni 153.9 zimetengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 na shilingi bilioni 150 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kugharamia nyongeza ya mwaka ya mishahara;

Tatu, Serikali imehuisha viwango vya malipo ya posho ya safari za kikazi ndani ya nchi na posho ya masaa ya ziada kwa lengo la kuwawezesha watumishi wa umma kumudu gharama za maisha kwa kuzingatia hali halisi ya kiuchumi;

Nne, Serikali imerejesha utaratibu wa kuwapandisha vyeo watumishi wenye sifa stahiki kila baada ya miaka mitatu badala ya miaka minne kuanzia mwaka huu wa fedha. Kwa msingi wa uamuzi huo, Serikali inaendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo

watumishi 81,515 waliokasimiwa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa gharama ya shilingi bilioni 130.4 kwa mwaka na watumishi wengine 219,924 wamekasimiwa kupandishwa vyeo katika Ikama na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa gharama ya shilingi bilioni 252.7. Aidha, Serikali imeridhia kulipa mishahara ya wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 113 zilizopo hapa nchini zenye jumla ya watumishi 691 kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma ikiwemo, kutenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kugharamia nyongeza za mishahara ya kila mwaka, posho na marupurupu kwa watumishi kwa kadri ya hali ya uchumi itakavyoruhusu ili kuongeza motisha na chachu ya uwajibikaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kujali maslahi ya watumishi nchini. Kwa kweli watumishi wana matumaini makubwa na Serikali hii, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Serikali imekuwa na mpango wa kujenga nyumba za watumishi maeneo mbalimbali na wapo watumishi ambao huwa wanapata hizi nyumba na wengine wanapanga nyumba zao kwa hela zao wenyewe. Naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kuwa na fedha maalum za kuwapatia watumishi ambao hawana nyumba za Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mwaka 2020 Serikali ilitoa maelekezo kwamba halmashauri ambazo zilikuwa kwenye miji au nje ya maeneo yao wahamie kwenye maeneo yao. Halmashauri ya Njombe *DC* ni sehemu ya hizo halmashauri ambazo walihama kutoka Njombe Mjini kwenda Mtwango na baadaye kwenda Kidegembye, lakini mpaka leo watumishi hao ambao walihama kwenye maeneo hayo hawajalipwa fedha za uhamisho kwenye hayo maeneo. Je, ni lini watumishi wangu wa

Halmashauri ya Njombe *DC* watalipwa fedha zao za uhamisho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Swalle ambaye kwa hakika anafanya kazi kubwa ya kufuatilia maslahi ya watumishi na sisi kama Serikali tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watumishi ambao wanakwenda kwenye vituo vya kazi wanakosa nyumba na kwamba wanaangaliwaje katika masuala mazima ya kuwa-*motivate*. Serikali kwanza imeendelea kuhakikisha kwamba watumishi wote wa umma hasa wale ambao wanakwenda katika maeneo ambayo yana changamoto kama ambazo amezieleza Mheshimiwa Mbunge, tumeendelea kuwaangalia katika maslahi yao kupitia taratibu mbalimbali zikiwemo zile taratibu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo wamekuwa wanatoa *token* kwa ajili ya kuwasaidia watumishi hawa waweze kukaa katika mazingira ambayo watafanya kazi bila kujilaumu kwamba kwa nini wamekwenda kufanya kazi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, yapo baadhi ya maeneo, Serikali kupitia mapato ya ndani imekuwa inatoa pesa kuwanunulia vifaa ikiwemo magodoro na vitanda. Pia, halmashauri nyingine zile ambazo zina uwezo mkubwa wamekuwa wanatoa pesa kuwasaidia hata kuwapangia nyumba watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Swalle kwamba katika utaratibu huu kwangu mimi kama Mheshimiwa Waziri mhusika wa Watumishi, nataka nielekeze halmashauri zetu zote kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuhakikisha watumishi wetu wanaendelea kuwa *motivated* kwa maana ya kutengenezewa mazingira mazuri ya kuendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya swali la pili kwa watumishi ambao wamehamishwa mara mbili, wale watumishi wa Halmashauri ya *Njombe DC*. Nataka kulihakikishia Bunge lako pamoja na Mheshimiwa Mbunge Swalle kwamba Serikali haina nia ya kuwadhulumu watumishi hao. Serikali itaendelea kuweka kipaumbele kimojawapo ikiwemo kulipa au kutenga pesa kwa ajili ya kuwalipa madeni haya ambayo yameendelea yakitokea katika maeneo hayo hususan katika Halmashauri yako ya *Njombe DC*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Issa Mtemvu niliwaona, maswali mafupi.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kwamba Watumishi wa Umma Kada ya Ualimu ndiyo kada pekee ambayo hainufaiki na aina yoyote ya *allowance*. Hawana *extra duty allowance,* hawana *sitting allowance,* hawana *acting allowance* na aina nyingine ya *allowance*. Kwa dhamira hiyo njema ya Serikali; je, Serikali ipo tayari sasa kufikiria kukaa ili kutoa *teaching allowance* kwa walimu? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo mazuri yanayotolewa na Mheshimiwa Mbunge kwetu sisi Serikali ni kupokea, kuchukua na kwenda kuangalia kwa sababu unapozungumzia *allowance* yoyote ile jambo kubwa au kigezo kikubwa ni uwezo wa kipato wa kibajeti ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tutaendelea kuangalia haya mawazo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge. Kama uwezo wa kuweka *allowance* hizi utakuwepo tutaendelea kuangalia. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na hasa kundi kubwa analolisemea la walimu, Serikali imeendelea kuwaangalia walimu katika maslahi mengi sana yakiwemo maslahi ya kuhakikisha walimu wanaendelea kupunguziwa mzigo wa masomo kwa kuongeza namba kubwa ya walimu ambapo

katika mwaka huu wa bajeti watakuja kueleza hapa wenzetu jinsi ambavyo Serikali inaendelea kuongeza namba ya walimu. Pia, kuendelea kuwawekea mazingira mazuri ya kuwapa motisha nzuri ili waendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kulihakikishia Bunge lako na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua hilo. Tutalichukua na tutaendelea kufanyia kazi kwa uwezo wa kibajeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, nilikutaja na Mheshimiwa Janejelly

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mpango wa kurithishana madaraka Serikalini au wanaita *succession plan*. Hii inasababishwa na kutokustaafu kwa watu wengi, lakini kutokuajiri kada nyingi kwa muda mrefu. Je, ni upi mpango wa Serikali kusimamia hii *succession plan* au mpango huu kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba Serikali inao mpango wa *succession plan* katika kada zote. Kwa sababu katika utaratibu wa kupitisha muundo ili muundo wako uweze kukubalika katika Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi, moja ya kitu kikubwa ambacho lazima ukiweke ndani ni *succession plan* na hili Mheshimiwa Mbunge na Bunge linaweza likathibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na maombi mengi sana yanayoletwa kwa Katibu Mkuu tukiombwa kuongezea baadhi ya kada fulani au watu fulani muda wa nyongeza kabla hawajastaafu na Katibu Mkuu amekuwa anasisitiza sana. Hili jambo liende kwa Wizara na Taasisi zote ikiwemo wenzetu wa Serikali za Mitaa kwamba, kabla haujaleta muundo kwa Katibu

Mkuu Utumishi, ni vyema uhakikishe kwamba ndani yake upo mpango wa kurithishana madaraka kama ambavyo inaelekezwa katika taratibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Serikali kwa juhudi wanazofanya kuboresha maslahi ya watumishi, lakini swali langu ni moja. Katika majibu ya Waziri amesema sasa wamerudisha watumishi kupandishwa vyeo baada ya miaka mitatu. Je, watafanyaje kwa hawa ambao walishaumia kwa miaka minne na imewapotezea tayari *gap* la kupata *promotion* nyingine? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali zuri lililoulizwa na Mheshimiwa Janejelly ni kwamba kila inapokuja sheria yoyote utaratibu ni kwamba sheria hairudi nyuma inakwenda mbele, hili jambo nataka Bunge lako lifahamu. Serikali katika kuhakikisha kwamba huu msawazo, niite msawazo katika lugha nzuri; msawazo wa kimamlaka wa Watendaji wa Serikali unakuwepo, imeendelea kuangalia ili wasije watu wengine wakaachwa nyuma. Ndiyo maana Serikali ikaja na wazo la kuwa na kitu kinachoitwa vyeo vya mserereko ili kusaidia kufanya hiyo ambayo kwa lugha ya Kingereza tunaita *adjustments* ili kila mmoja akae katika cheo anachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nilihakikishie Bunge lako na Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo wazo lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge ni moja ya wazo ambalo tunalichukua na tumekwishaanza kulifanyia kazi. Nataka nimhakikishie na nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna mfanyakazi atakayeachwa katika kupandishwa vyeo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 276

**Uchumi wa Mji Mdogo wa Mtambaswala – Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya utafiti katika Mji Mdogo wa Mtambaswala ili kubaini ni namna gani unaweza kuchangia uchumi wa nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Mipango imejipanga kuhakikisha kuwa upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo unazingatia tafiti za kisayansi na ushahidi wa kitakwimu. Katika kutekeleza hilo, Tume ya Mipango imeanza zoezi la utafiti kuhusu uchumi wa mipakani *(border economies)* katika miji mbalimbali kwa lengo la kubainisha fursa, changamoto na namna miji hiyo inavyoweza kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi ikiwemo Mji wa Mtambaswala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa utafiti huu kutawezesha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi kuhusu uchumi wa mipakani zitakazosaidia katika mipango ya maendeleo ili kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na *agenda* za kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Serikali ilifanya Sensa ya Makazi na Watu mwezi Agosti mwaka 2022 na takribani shilingi 350,000,000,000 zilitumika kwa shughuli hii. Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni takwimu gani ambazo wanazihitaji kuzifanya nje na takwimu ambazo Sensa ya Makazi ilizifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mji huu wa Mtambaswala umeunganishwa na Mji wa Msumbiji kwenye Daraja la Umoja na Daraja hili lilikuwa kwenda sambamba na ujenzi wa bandari kavu katika Mji wa Nangomba. Je, ni lini bandari kavu hii itajengwa ili kuchochea uchumi wa mji huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Ally Yahya Mhata kwa kuwa amekuwa akifuatilia sana suala hili la mpakani kwa maana ya mpaka ule wa Tanzania na Msumbiji kupitia pale Mtambaswala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumesema takwimu hizi ambazo zipo ikiwemo za sensa ambayo imefanyika hapa nchini na tafiti nyingine tunataka tuone katika mipaka yote ikiwemo Mtambaswala tunajenga kitu kinaitwa *One Stop Border Post* (vituo vya mpakani). Hivi vituo sasa ndiyo lengo baada ya kuona takwimu sahihi ambazo tunazo kupitia mpaka huu tunajenga hicho kituo *OSBP* pale ili kuchangamsha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo takwimu hizo ndizo zinatusaidia kufanya maamuzi au utekelezi wa mipango ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli katika Halmashauri ya Nanyumbu kuna Daraja lile la Umoja ambalo linaunganisha kupitia pale Nangomba na kwenda Msumbiji. Ndiyo maana

tunasema moja ya mambo ambayo tunayafanya ni kuongeza kwanza biashara katika mpaka ule na huo ndiyo sasa utatupelekea kujenga na hii ambayo tunalenga kuwa na bandari kavu ambayo itasaidia sana kuhakikisha uchumi kwa sababu mahitaji makubwa kwa wenzetu pale ni kuchukua bidhaa kutoka kwetu. Kwa hiyo tutumie fursa hii ili tuweze kufaidika na soko zuri lililopo kwa majirani zetu pale Msumbiji kwa maana ya kupitia mpaka huu wa Mtambaswala. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi aulize swali lake.

Na. 277

**Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Kakozi Tunduma**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kakozi, Tunduma utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa *TAZA* unaotekelezwa na *TANESCO* ipo katika hatua za awali za ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Nkangamo kilichopo takribani kilometa 28 kutoka Kijiji cha Kakozi. Ujenzi wa Kituo hiki unatarajia kuanza hivi karibuni ambapo kwa sasa mkataba kati ya *TANESCO* na mkandarasi atakayejenga kituo hiki tayari umeshasainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa Kituo hicho kutawezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Kijiji cha Kakozi na maeneo mengine ya Jimbo la Mbozi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kituo hiki kinasubiriwa kwa hamu sana na wananchi wa Mkoa wa Songwe kutokana na matatizo ya umeme yaliyopo ndani ya Mkoa wa Songwe kwani itaondoa utegemezi wa Mkoa wa Songwe kutoka Kituo cha Mwakibete pale Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tangu kuwashwa kwa mtambo wa umeme Na.9 katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, sisi Mkoa wa Songwe bado hatujafaidika na kuwashwa huko kwani bado tatizo la umeme limeendelea kuwa kubwa Mkoani Songwe *especially line* ya Mlowo-Kamsamba na *line* ya Tunduma. Nini hasa kinachosababisha matatizo ya umeme kuendelea katika Mkoa wa Songwe licha ya kuwashwa kwa mtambo Na.9 katika Bwawa la Mwalimu Nyerere?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo ya watu wa Mbozi na Mkoa mzima wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na umeme kukatika katika *line* ya Mlowo-Kamsamba pamoja na Tunduma. Mkoa wa Songwe unapata umeme kutoka katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Mwakibete kilichopo Mbeya. *Line* kutoka Mbeya mpaka Songwe ni ndefu sana na hivyo kupelekea tatizo la *low voltage*. Serikali tumeshaliona, kwa sasa kupitia Mradi wa Gridi Imara tunakwenda kujenga *switching station* pale Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupitia Mradi wa *Tanzania-Zambia Interconnector* tunakwenda kujenga Kituo cha Kupoza Umeme Songwe kwa ajili sasa watu wa Songwe waweze kupata umeme kutoka Kituo cha Kupoza Umeme Songwe na *switching station* ambayo itakuwa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Mkoa wa Songwe, tumeliona tatizo hili na tutalifanyia kazi kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Songwe, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, nimekuona.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiambiwa kuwa changamoto ya kukatikakatika kwa umeme imekwisha katika nchi yetu, lakini eneo la Loliondo Wilaya ya Ngorongoro changamoto hii inazidi kukua kila siku. Nataka kufahamu, je, Loliondo sio sehemu ya Tanzania? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hilo siyo swali kwa sababu Loliondo ni sehemu ya Tanzania. Mheshimiwa Margaret Sitta nilikuona na Mheshimiwa Condester. *(Kicheko)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Urambo kuangalia Kituo chetu cha Kupozea Umeme kinachojengwa sehemu ya Uhuru. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri naweza kutwambia lini kituo kile kitaisha ili na sisi tupate umeme kwa sababu tuna tatizo kubwa sana la umeme Urambo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia Kituo hiki cha Uhuru. Kituo cha Uhuru kipo katika hatua za kwenda kumalizika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunakisimamia kwa hali na mali kuhakikisha kinakamilika na kinaanza kuwanufaisha watu wa Urambo. Kwa hiyo, kwa sababu kimeenda vizuri sana na hata fidia watu wa eneo la Urambo wamelipwa, nimweleze Mheshimiwa Mbunge azma ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wa Urambo wanaendelea kupata umeme wa uhakika na tutasimamia Kituo hiki kimalizike ili wananchi wako wa Urambo waweze kupata umeme wa uhakika zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester nimekuona.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa ufafanuzi mzuri sana na kutoa matumaini mazuri sana juu ya Kituo cha Nkangamo kilichopo ndani ya Jimbo la Momba. Sasa kwa kuwa maisha ya wananchi yanaendelea na wanahitaji umeme; je, upi mkakati wa dharura wa Serikali kwa ajili ya kutusaidia kuondoa changamoto hiyo wakati tunasubiri mpango wa muda mrefu huu ambao ametoa ufafanuzi, naomba majibu ya kuridhisha? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya dharura tayari inaendelea. Kwanza tunaendelea na kuboresha miundombinu iliyopo katika Mkoa wa Songwe na majimbo yote yaliyopo katika Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ya dharura nimeelezea ni kujenga *switching station* pale Songwe kwa ajili ya kuboresha *low voltage* ya umeme ambayo inatokea Mwakibete hadi Songwe. Kwa hiyo niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tumeshaanza kuchukua hatua za dharura ikiwemo kuboresha miundombinu kuhakikisha umeme haukatiki katiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; tunaenda kuanza utekelezaji wa kujenga *switching station* kwa ajili ya kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ng’wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 278

**Kuwapatia Vijana Vifaa vya Kutengeneza Vihenge**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuwapatia vijana 400 vifaa vya kutengeneza vihenge visivyoruhusu hewa kwa mujibu wa Ilani ya CCM ya 2020 - 2025?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania *(TANIPAC)* imewapatia vijana 420 vifaa vya kutengeneza Vihenge vya Chuma visivyopitisha hewa vyenye thamani ya shilingi 548,479,105 ambapo kila kijana alipatiwa seti moja iliyojumuisha *Arc Welding Machine, Angle Grinder Machine, Portal Grilling Machine, Steel Divider, Tape Measure, Try-square, Centre Push, Hand Hacksaw* na *Safety Goggles*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifaa hivi vilizinduliwa na kugawanywa kwa vijana 420 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane tarehe 08/08/2023 katika viwanja vya maonesho vya John Mwakangale, Mbeya.  Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza nianze kwa kuishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa majibu mazuri. Pia, nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na hii ndiyo maana nzima ya kuahidi na kutenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 - 2025 ukurasa wa 43 iliahidi kutoa vifaa hivi na

kuwawezesha vijana 400, lakini jibu la Mheshimiwa Waziri linaonesha kwamba wamewawezesha vijana 420. Maana yake ni zaidi ya utekelezaji wa 100%. Sina swali la nyongeza, naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, naomba sasa kuwepo na *series* ya ufuatiliaji wa vijana hawa ili vifaa hivi walivyopewa viweze kweli kuwaletea yale manufaa ambayo yalitegemewa tangu mwanzo na manufaa kwa wakulima katika utunzaji wa chakula baada ya mavuno. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwona Mheshimiwa Ussi Pondeza na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda nichukue nafasi hii kumuuliza swali dogo Mheshimiwa Waziri; Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kiuchumi wananchi vijana wa Jimbo la Kibiti katika Mkoa wa Pwani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umemwelewa? Mheshimiwa Ussi Pondeza, rudia kidogo swali lako.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kiuchumi vijana ambao wapo katika Jimbo la Kibiti, ambapo ukipita Jimbo la Kibiti, ukiangalia mazingira watu wengi wanaonekana hali zao ni za chini. Sasa tunataka kujua Serikali yetu hii sikivu inawainuaje kiuchumi na ina mpango gani wa kuwawezesha...

**MWENYEKITI:** Sawa, umeeleweka. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenifahamu?

**MWENYEKITI:** Tayari nimekufahamu. Mheshimiwa Waziri, majibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake lina wigo mpana, lakini katika Sekta ya Kilimo, moja ya malengo ya Serikali tuliyonayo kwa Jimbo la Kibiti hususan lile Bonde zima; ni kwamba sasa hivi tumeshatangaza *tender* kwa ajili ya kwenda kujenga mabwawa mawili makubwa kule na mifumo ya umwagiliaji. Kwa hiyo tukishatengeneza ile miundombinu kwenye maeneo yale maana yake vijana wengi wa Jimbo la Kibiti watanufaika na ile miradi. Kwa hiyo, watakuwa na shughuli za kiuchumi za kufanya. Hiyo ni kwenye Sekta ya Kilimo. Kwa sekta nyingine Waheshimiwa Mawaziri wengine wamesikia na watalifanyia kazi jambo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, nilikutaja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa, Serikali imeanzisha Mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora kwa vijana nchini; je, ni lini Serikali sasa italeta Mpango huu katika ngazi za majimbo na halmashauri nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora unaanza katika mwaka wa fedha unaokuja. Ndiyo maana katika bajeti ambayo Bunge lilitupitishia tumeainisha halmashauri 100 zitakazotenga maeneo kwa ajili ya vijana hao. Sisi Wizara tutakuja kwa ajili ya kujenga miundombinu yote. Shughuli hiyo ya kuwateua hao vijana itafanyika katika ngazi za majimbo na halmashauri husika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana aulize swali lake.

Na. 279

**Sheria ya Mwendo wa Magari kwa Kilometa**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kubadilisha sheria ya mwendo wa magari kutoka kilometa 80 hadi kufikia kilometa 100 kwa saa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 ya Mwaka 1973 iliyorejewa Mwaka 2002, Kifungu cha 51(8) inayoelekeza matumizi ya mwendokasi wa kilomita 50 kwa saa na mwendokasi wa kilomita 80 kwa saa, bado ni sahihi ukizingatia aina ya barabara tulizonazo nchini kwa sasa. Aidha, Wakala wa Ujenzi wa Barabara wakiboresha barabara na madereva wakielimishwa ipasavyo kuheshimu sheria za usalama barabarani, maboresho ya sheria yanaweza kufanyika na kufikia kilomita 100 kwa saa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, pamoja na majibu ya Serikali kwa swali langu, lakini miundombinu yetu ya barabara imeimarika sana, hususan barabara kuu. Hizi sheria zilizotunga *speed limit* ya 50 na 80 kiukweli ni kama zimepitwa na wakati. Sasa hivi tuna magari yanakimbia mpaka *speed* 280 na yeye kama Naibu Waziri atakuwa shahidi; je, hawaoni sasa uko umuhimu wa lazima wa kubadilisha sheria ya *speed* 50 kwenda angalau 80 na ile ya 80 kwenda angalau mpaka 100 hadi 120. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vilivyopo sasa hivi vya kilometa 50 kwa saa na 80 kwa saa viliwekwa baada ya kufanya tathmini ya hali ya barabara na kupokea maoni ya wadau mbalimbali na hatimaye zikawekwa kisheria. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafanya tathmini ya hali ya barabara ilivyo nchini na kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kabla ya kubadilisha sheria hii ya viwango vya 50 kwenda 80 na 80 kwenda 100. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Saashisha Elininkyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, aulize swali lake.

Na. 280

**Kumaliza Kero ya Maji – Hai**

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza na kumaliza kero ya maji katika Jimbo la Hai aliyoitoa Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa mwaka 2020 wakati wa ziara Wilayani Hai ya kumaliza tatizo la maji katika wilaya hiyo, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi sita ukiwemo Mradi wa Maji wa Kikafu - Bomang'ombe ambao umezinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango wakati wa ziara yake mwezi Machi, 2024, Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa miradi hiyo kumeboresha huduma ya maji katika Mji wa Hai hususani kwa wakazi 63,049 waishio kwenye Kata tatu za Bomang'ombe, Muungano na Bondeni; pamoja na wananchi wapatao 41,963 wa Vijiji vya Kwasadala, Rundugai, Kawaya, Foo, Nshara, Uduru, Wari Ndoo na Wari Sinde, Isawerwa, Kimira, Mudio, Roo Sinde, Roo Ndoo, Mkombozi Kware, Uswaa, Mamba na Mungushi, Ngosero, Mbatakero na Chekimaji. Aidha, utekelezaji wa miradi mitatu ya upanuzi wa skimu za usambazaji maji inaendelea ili kumaliza tatizo la huduma ya maji katika Jimbo la Hai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali na naishukuru sana Serikali kwa kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea bilioni 3.39 na mradi umezinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kuna Mradi wa Visima 18 unapeleka maji Arusha na Sera ya Maji inasema kwenye chanzo cha maji chochote, wananchi wanaozunguka eneo lile wanatakiwa wapate maji. Je, ni lini sasa Serikali itaanza utaratibu wa kuwapatia wananchi wale walioko kwenye ule mradi wa visima vya maji ili na wao waweze kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwepo na changamoto kubwa sana, wananchi wa Mkalama, Shirimatunda, Shiri Muungano, Shiri Njoro, Mijongweni, Longoi na Kikavu Chini,

kutokana na kwamba mradi wa maji kwenye maeneo haya unasimamiwa na Mamlaka ya Maji Moshi Mjini; je, ni lini Serikali itaondoa Mamlaka ya Usimamizi wa Maji Moshi Mjini na kurejesha kwenye *RUWASA,* Wilaya ya Hai ili Wilaya ya Hai iweze kusimamia yenyewe, Mamlaka ya *RUWASA* isimamie maeneo haya ili wananchi waweze kutatuliwa matatizo yao? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kila mradi unaokuwepo katika jimbo lake, lakini siyo hivyo tu na kufuatilia utekelezaji wake. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Vilevile Mheshimiwa Mbunge ameongelea kuhusu Sera ya Maji. Ni kweli kabisa Sera yetu ya mwaka 2002 inaelekeza kuhakikisha kwamba pale palipo na vyanzo vya maji ni lazima vijiji vinavyozunguka pale wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika ile miradi mikubwa, bomba kuu la maji linapopita, *at least* kilometa 12 upande wa kushoto na kulia, wananchi wanaoishi katika maeneo hayo waweze kunufaika. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, changamoto ambayo imebainika pale baada ya Wizara kufanya tathmini; kwa kutumia ule mradi wa visima 18 ili tuweke *pump* na kusukuma maji kuwafikia wananchi walioko pale, tumegundua kwamba *pump* itahitaji kusukuma maji kilometa 30, maana yake ni kwamba gharama ya maji ambayo yanawafikia wananchi yatakuwa yana gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri ameelekeza *RUWASA* Kilimanjaro kufanya tathmini na usanifu ili twende kutumia maji ya kutoka Njoro Bluu kwenye chanzo ambacho ni maji mserereko, ambapo itakuwa na gharama rahisi zaidi kuwafikia wananchi na kupata maji ambayo yana gharama ndogo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba hilo linakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kweli kabisa kama ambavyo ameomba, kwamba mamlaka ya maji anahitaji isimamiwe na *CBWSOs*; naamini kwamba alikuwa anamaanisha *CBWSOs; of cause CBWSOs* iko kisheria; na sisi Wizara ya Maji, kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Jumaa Aweso, hatutaki kuwa kikwazo kwa wananchi kupata maji.

Mheshimiwa Spika, sisi pale ambapo tunaamini kwamba maji yenye ubora, toshelezi na salama yatafikishwa basi tutatumia mfumo huo ambao utaweza kuwarahisishia wananchi kupata maji ambayo ni safi na salama zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Ally Jumbe na Mheshimiwa Zedi, nimewaona. Maswali yawe mafupi tafadhali.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mvua zinazoendelea nchini sasa hivi zimeharibu sana miundombinu ya maji, hasa kule ambako mafuriko yametokea, ikiwemo Mabogini, Chekereni na Chemchem kule Mkoani Kilimanjaro ambayo ni tambarare ya mlima. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya haraka kwenda kuwapatia wananchi hao maji safi na salama ili wasije wakapata kipindupindu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji ina mikakati ya kuhakikisha kwamba inaweza ku-*manage* maji mengi. Maji mengi maana yake ni mafuriko na maji machache, maana yake ni ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kukifanya pale ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza *catchments* za maji ya kutosha na baadaye tunafanya *treatment* ili wananchi ambao wako katika maji machache ambao ni ukame waweze kupata

maji na wale ambao wanaweza kuathiriwa basi tuweze kuya-*control* na kuhakikisha kwamba tunayatumia kama *resource* ambayo itawasaidia wananchi kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, niwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kushirikiana kwa sababu sisi hatutakuwa kikwazo kwa wananchi ambao amewataja kupata maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Jumbe, kwa ufupi.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini Mradi wa Sinyanga *Group* Wilayani Kyela utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge amekuwa akipambana nao tangu mwaka 2023. Natambua kwamba kulikuwa na changamoto ya malipo na mkandarasi *GOPA contractors* ambaye bado anatudai takriban milioni 122. Serikali tayari tumeshawasiliana na wenzetu Wizara ya Fedha, wameshaanza kuandaa kwa ajili ya kumlipa. Mradi tayari umeshafikia asilimia tano kwa sababu tayari kuna jengo la *CBWSOs* limeshajengwa na limefikia kwenye *lintel*. Tunaamini kwamba fedha zikishaingia na mkandarasi atarudi *site*. Tunaamini kwamba ndani ya mwaka wa fedha litakuwa limekamilika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zedi, swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Bukene wanapata maji safi na salama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Jimbo la Bukene linapitiwa na Mradi wa Ziwa Victoria. Tayari tunakwenda kuunganisha Jimbo la Bukene ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Takriban wananchi 80,000 wanakwenda kupata huduma ya maji na vijiji 20 vitanufaika na mradi huu kutoka Ziwa Victoria. Vilevile tuna takriban vitongoji 100 vinakwenda kupata huduma ya maji. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mradi huu uko kwenye utekelezaji, tayari umeshaanza na muda siyo mrefu ukikamilika wananchi wake watapata maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 281

**Kupunguza na Kufuta baadhi ya Tozo Sekta ya Uvuvi**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali katika kupunguza baadhi ya tozo na kufuta zingine ili kuleta unafuu kwa wavuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020 na mwaka 2022 Serikali ilifanya maboresho ya tozo mbalimbali ambapo ilipelekea baadhi ya leseni kuunganishwa na tozo nyingine kupunguzwa. Tozo ambazo zilipunguzwa ni ushuru wa zao la dagaa wanaozalishwa Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi kutoka dola 0.16 hadi kufikia dola 0.1 kwa kilo na tozo ya dagaa wa Ziwa Tanganyika kutoka dola 0.5 hadi kufikia dola 0.3 kwa kilo. Pia, gharama za tozo ya kusafirisha minofu ya samaki ya sangara

nje ya nchi ilipunguzwa kutoka dola 0.2 hadi kufikia dola 0.1 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, imepunguza ushuru wa uingizaji mazao ya bahari nchini kutoka dola 2.5 hadi kufikia dola 0.5 kwa kilo kwa mazao ya ngisi, pweza na kaa. Aidha, maeneo mengine ambayo yamefanyiwa maboresho ni kupunguza gharama ya ada za leseni za kusafirisha dagaa kutoka dola 1,000 hadi kufikia dola 250 kwa dagaa wa maji chumvi na maji baridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuboresha na kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi nchini kadiri itakavyowezekana na kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nikiwa kama Mlezi wa Chama cha Wavuvi, Mkoa wa Kagera natambua fika changamoto mbalimbali za wavuvi kwenye Ziwa Victoria; kwa hiyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kila halmashauri inatoza ushuru tofauti. Nitatoa mfano haraka haraka; Chato kwa kilo moja ya sangara wanatoza shilingi 100, kwa gunia la dagaa wanatoza shilingi 1,000. Sengerema, sangara ni shilingi 100 na gunia la dagaa ni shilingi 1,500. Bukoba Mjini, kilo ya sangara ni shilingi 100 na gunia la dagaa shilingi 2,000. Muleba kilo ya sangara shilingi 300 na dagaa kilo moja shilingi 100. Je, Wizara iko tayari kutoa mwongozo ambao utazielekeza na kuwezesha hizi halmashauri zitoze tozo inayofanana ili kutoendelea kuangamiza wavuvi wetu kwa kutoza tozo tofauti tofauti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika hizi kanuni ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri alizisema hapa, Kanuni ya

Usafirishaji wa Samaki ya mwaka 2020 imetoa *exemption,* yaani imetoa msaada wa kodi pale ambapo mvuvi atakuwa anasafirisha chini ya kilo 30 za samaki kama kitoweo. Kwa maana kama chakula, hapaswi kulipa tozo wala hahitaji leseni; lakini hivi sasa halmashauri zinatoza wavuvi tozo pamoja na kudai leseni. Je, Serikali ipo tayari kutoa mwongozo ambao utaelekeza kanuni hizi zifuatwe ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kwanza, kwamba tozo zinatofautiana katika kila halmashauri. Ukweli ni kwamba kanuni hizi zinapangwa na halmashauri wenyewe. Halmashauri wamepewa mamlaka ya kupanga kanuni na sheria ndogo ambazo zinawaongoza katika halmashauri yao. Kwa hivyo, wao wanaangalia kulingana na mazingira yao, mazingira ya wavuvi wetu, mazingira ya wafanyabiashara wetu wa dagaa, samaki na mazao ya ziwani, wanaangalia namna ambavyo mazingira yao yanawapelekea kupanga kanuni hizo na wanazipeleka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwenda kupitisha kanuni hizo kama zinakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara tunachofanya ni kutoa mwongozo ili kanuni hizo zisivunje sheria kubwa ambayo ni sheria mama, ni Katiba ya Nchi na sheria inayoongoza masuala ya uvuvi. Kwa hiyo, kama kuna changamoto namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Mifugo itakwenda kukaa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili tuzipitie kanuni hizo. Kama zina changamoto kulingana na mazingira yanayohusika basi tutakwenda kuzirekebisha kadri itakavyowezekana. Ukweli ni kwamba kanuni na sheria ndogo hupangwa na halmashauri husika kwa faida ya halmashauri yenyewe kulingana na makusanyo na mazingira ya wafanyabiashara wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili swali la pili, Wizara iko tayari kufuatilia ili kuona kama kuna mwananchi, mfanyabiashara ama mwananchi yoyote anayebeba kilo 30 na kusumbuliwa. Kwa

sababu ukweli ni kwamba kilo 30 ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Kama kuna maeneo ambayo halmashauri wanatoza tozo ama wanakatisha ushuru kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa namna hii. Wako wafanyabiashara wenye kilo 30, wanakwenda kufanya biashara hiyo ni ruksa kwa sababu wako chini ya kanuni lakini wako walio na kilo 30 kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Kama kuna maeneo ambayo watu hao wanasumbuliwa, nitoe rai kwa halmashauri, Maafisa Mifugo wote na Maafisa Uvuvi kuacha mara moja kuwatoza faini ama kuwatoza tozo yoyote wananchi wa namna hii kwa sababu wako ndani ya sheria na sheria inawalinda kwamba hii ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna taarifa zozote za siri, tuko tayari kuzipokea na kwenda kuzifanyia kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 282

**Mkakati kuhusu Kiwanda cha Nyama Shinyanga**

**MHE. DKT.CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango mkakati gani juu ya Kiwanda cha Nyama kilichopo Shinyanga ambacho hakifanyi kazi iliyokusudiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga ni miongoni mwa viwanda vitatu vya nyama vilivyokuwa vinamilikiwa na Kampuni ya *Tanzania Packers Limited (TPL)*. Kiwanda kilianza kujengwa mwaka 1975 na kukamilika mwaka 1978 kwa 84% ila kiwanda hakijawahi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kilibinafsishwa kwa Kampuni ya *Triple S Beef Limited*, mwaka, 2007. Hata hivyo, mwekezaji hakuweza kuendeleza kiwanda hicho kulingana na makubaliano ya mkataba wa ubinafsishaji, jambo lililosababisha Serikali kuamua kukirejesha mwaka 2017 na kwa sasa kiwanda kipo chini ya usimamzi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta mwekezaji mahiri mwenye nia thabiti ambaye atawekeza katika kiwanda hicho ili kiweze kufanya kazi iliyokusudiwa kwa maslahi ya Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Serikali ilitumia fedha nyingi sana katika kuwekeza kiwanda hiki. Kwa majibu ya Naibu Waziri anasema kwamba wanaendelea kutafuta mwekezaji mahiri. Swali la kwanza, je, ni lini sasa huyo mwekezaji mahiri atapatikana ili kiwanda kiweze kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa toka mwaka 1974 kilivyojengwa hakijawahi kufanya kazi na eneo lipo na majengo yapo. Je, Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha walau matumizi ya hicho kiwanda ili uwekezaji mwingine ukafanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kweli kwamba Serikali ilitumia pesa nyingi sana kujenga kiwanda hiki mwaka 1975. Ukweli ni kwamba sasa majengo hayo yamekaa kwa muda mrefu na eneo hilo limekaa kwa muda mrefu bila matumizi. Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali inaendelea kutafuta mbia ambaye ana uwezo wa kukifufua kiwanda hiko ili kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lengo la Serikali ilikuwa ni kusogeza huduma hizo za kiwanda hicho katika eneo hilo la Shinyanga na maeneo ya Kanda ya Ziwa. Kwa hivyo, tuko katika harakati za kuendelea kutafuta wawekezaji. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama anaweza akatusaidia pia na sisi tuko tayari kushirikiana naye kuhakikisha kwamba tunapata mwekezaji katika eneo hili atakayefufua kiwanda hiki ili aweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la kubadilisha matumizi, Wizara tutakwenda kuangalia kama tulivyosema kwamba tuko katika hatua za kutafuta mwekezaji, lakini kwa mawazo hayo ya Mheshimiwa Mbunge pia tuko tayari kufuatilia kuona kama tunaweza kubadilisha matumizi. Tutaangalia wapi kwenye tija, kuendelea kutafuta mwekezaji ama kwenda kuangalia namna gani bora zaidi ya kwenda kuboresha katika eneo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru kwa majibu haya.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke aulize swali lake.

Na. 283

**Wafanyabiashara Kulipwa Riba Wanapocheleweshewa Malipo**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wafanyabiashara kulipwa madai na riba pindi wanapocheleweshewa malipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa madai yanayotokana na kupokelewa kwa bidhaa au huduma huzingatia masharti ya mikataba ya zabuni au kandarasi iliyoingiwa baina ya Serikali na mtoa huduma. Hivyo, Serikali hulipa au hulipwa riba pindi masharti ya mikataba ya zabuni au kandarasi yanapokiukwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza maswali mawili. Swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari sasa kutoa maelekezo kwa wale ambao wanaingia mikataba ili waweze kulipwa na riba wakati huo? Kwa sababu, wao pia wanapokuwa wameingia mikataba pamoja na kuwa labda Serikali imewapa mkataba na mashirika ya nje, wale mashirika ya nje wanapokuja kuwapa mkataba wajasiriamali wa ndani, nao wanachelewa kuwalipa wale ambao tayari wanakuwa wameingia mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, hawa wanaangaliwaje kwa sababu tayari Serikali wameshindwa kuwalipa kwa wakati, *let say* mfanyabiashara wa ndani naye anashindwa kulipwa na kushindwa kuwalipa wale. Je, mikataba yao ikoje? Je, Serikali wako tayari sasa kuweka au kutoa maelekezo pale ambapo wanakuwa tayari wameandika au wametoa hati za kumaliza mkataba? Kuna muda au wakati ambao na wao wapewe ili walipwe kwa wakati na wao walipe wengine kwa wakati? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge makini kabisa kwa kulileta swali hilo. Serikali inafanyia kazi hilo na naamini sasa hivi tunakamilisha Kanuni za Manunuzi baada ya Bunge lako kurekebisha Sheria ya Manunuzi ya Umma. Lengo ni kuhakikisha kwamba *contractors* wetu wananufaika na kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda hatua mbele zaidi ya hiki alichokiuliza Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu, mbali na

ucheleweshwaji ambao *contractors* wetu wanapata kutoka kwa *main contractors* wa kutoka nje, lakini pia, wale *main contractors* mikataba yao huwa tunaingia nao wengine inakuwa ya dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wao wanapowalipa *contractors* wazawa wanawalipa kwa shilingi na wanakuwa wamewacheleweshea sana. Kwa hiyo, hii hoja aliyoisema tutaifanyia kazi na tunawaza tuangalie uwezekano wa kuiweka kwenye Kanuni za Manunuzi ili iweze kuwalinda vizuri wazabuni wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 284

**Kurejesha 20 *Retention* ya Kodi ya Ardhi Halmashauri**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kurejesha 20% *(Retention)* ya Kodi ya Ardhi kwenye Halmashauri kama ilivyopitishwa katika Sheria ya Fedha 2023/2024?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hili.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilifanya maboresho ya ukusanyaji wa kodi ya ardhi ambapo halmashauri kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI zinatakiwa kukusanya kodi hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hadi Aprili 2024, taratibu za kuwezesha halmashauri kuanza kukusanya kodi ya ardhi hazijakamilika, hususan kufungamanisha Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Ardhi na Mfumo wa Kukusanya Mapato ya Halmashauri *(TAUSI)*.

Hivyo, 20% inayopaswa kurejeshwa halmashauri itaanza mara tu zoezi la kukusanya kodi ya ardhi litakapoanza kutekelezwa rasmi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, utaratibu huo unatarajiwa kuanza kabla au ifikapo 30 Juni, 2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, sababu ya kuleta sheria hii ambayo tulipitisha hapa Bungeni ilikuwa ni kuzi-*stimulate* halmashauri kwa maana zitakapobakiwa na ile 20% itazisaidia, siyo tu katika kuboresha namna ya kukusanya, lakini pia kukusanya katika Sekta ya Ardhi kwa ujumla wake. Je, sisi kwa mfano mpaka sasa tumeshakusanya milioni 367, Serikali iko tayari kuturejeshea milioni 73.4 mara utaratibu utakapokuwa umeiva?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tulikadiriwa tukusanye milioni 900 kwa maana kwamba 20% itakuwa milioni 180. Je, tutakapokuwa tumekamilisha watarejeshea hizo fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya msingi ni kwamba utaratibu huu ambao unahusisha kurejesha utaenda sambamba na ukusanyaji kuanza kufanya kazi kwa kutumia TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa hiyo, mara utaratibu huu wa kufungamanisha mifumo utakapokuwa umekamilika na ukusanyaji kuanza mara moja na urejeshwaji nao utaanza kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ahsante sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 285

**Huduma ya Mawasiliano Kata ya Simbay**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya Mawasiliano Kata ya Simbay - Hanang'?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeainisha changamoto ya mawasiliano katika Kata ya Simbay (Kijiji cha Simbay) na utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa kadri ya fedha zitakapopatikana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa, niishukuru Serikali kwa kuendelea kutatua changamoto ya mawasiliano katika nchi yetu. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa katika Wilaya ya Hanang' kwa maeneo kama Sirop, Gisambalang, Gidahababieg, Lalaji pamoja na Hirbadaw bado tuna changamoto kubwa ya mawasiliano. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuweka Kata hii ya Simbay na haya maeneo niliyoyataja ya Wilaya ya Hanang' katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kumekuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano katika Kata ya Nkaiti, Vilima

Vitatu na Wilaya ya Babati Vijijini. Je, Serikali haioni haja sasa ya kupeleka minara ya mawasiliano katika maeneo haya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Asia Halamga amekuwa mfuatiliaji mzuri katika hili na kama ambavyo mara ya mwisho amekuja Wizarani tukaongea kwa pamoja. Niendelee kumpa matumaini, maeneo haya yote aliyoyataja, mazingira yake tumeelewa na nipende kuiagiza *UCSAF* katika mwaka ujao wa fedha tuhakikishe tunawafikia wananchi na kuwapatia mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusu lini tutajenga mnara katika Kata ya Vilima Vitatu, Nkaiti, Babati Vijijini. Haya maeneo pia tayari wameshafanya *survey* na sasa wanaelekea kufanya *tendering* ya hivi vifaa vya kujengea mnara na ndani ya miezi sita tunatarajia katika maeneo haya ya Nkaiti, Babati Vijijini mnara huo utajengwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, aulize swali lake.

Na. 286

**Eneo Lililochukuliwa katika Kijiji cha Kasesya – Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya eneo lililochukuliwa bila fidia na halijaendelezwa katika Kijiji cha Kasesya mpakani mwa Tanzania na Zambia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu la swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili lilikuwa linafanyiwa marekebisho jana na niombe radhi tu kwamba sasa tunawasilisha jibu linalotakiwa kukaa kwenye *records* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilitwaa sehemu ya Ardhi ya Kijiji cha Kasesya kilichopo mpakani mwa Tanzania na Zambia ili kulifanya eneo kuwa la uwekezaji kwa kuwa lipo mpakani. Eneo hili lilitwaliwa kwa Sheria ya Ardhi ya wakati huo ambayo ilibainisha fidia kwa kuzingatia maendelezo tu, ambapo wakati huo eneo halikuwa na maendelezo yeyote hivyo hakukuwa na suala la fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lililotwaliwa lilipangwa na kupimwa na kutoa viwanja 52 ambapo halmashauri ilivitangaza viwanja kuanzia namba 5-36 vilichukuliwa na Taasisi ya *Tanzania Chambers of Commerce Industries and Agriculture* kwa Barua ya Toleo yenye Kumb. Na. LD/SDC/178/3 ya tarehe 10 Desemba, 2002, kwa matumizi mchanganyiko. Taasisi ya *Tanzania Chambers of Commerce* imeendeleza eneo dogo sana kwa kujenga machinjio na bucha chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeanza mazungumzo na Taasisi hiyo ambayo inamiliki eneo hilo kihalali ili kuona jinsi ya kufikia makubaliano ya kuona uwezekano wa kulirejesha eneo hilo kwa wananchi kwa kuwa halijafanyiwa maendelezo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia jambo hili linalohusu wananchi wake wa Kijiji cha Kasesya, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kijiji cha Kasesya kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea kutafuta ufumbuzi wa suala hili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali la kwanza; kwa sababu, upo uwezekano mkubwa Serikali imetwaa maeneo mengi ndani ya nchi hii ambayo haijafanyia maendeleo. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu maeneo yote ambayo wametwaa na wameshindwa kufanya maendelezo yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa hivi sasa ujenzi unaendelea wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Matai kwenda Kasesya ambapo kwa hakika eneo lile linaonekana kuwa ni *potential* kwa sababu liko mpakani. Je, nini mtazamo wa Serikali kuhakikisha kwamba wanalipa fidia na eneo hilo liweze kutumiwa na *TRA* kwa maana ya kujenga ofisi na nyumba za watumishi? Ili tuondokane na tatizo ambalo lipo la msongamano katika mpaka wetu wa Tunduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kauli kwenye maeneo yoyote ambayo hayajafanyiwa maendelezo kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba kwenye eneo hili ambalo ni *specific* la Kasesya tumeanza mazungumzo na mamlaka husika ili eneo hili liweze kurejeshwa, kwa wao kushindwa kulifanyia kazi kama walivyolilenga mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, Wizara ya Fedha ione umuhimu wa namna ambavyo inaweza ikapatumia pale kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *TRA,* nadhani Mheshimiwa Waziri amelisikia hili, kwa vyovyote litachukuliwa kwa namna ambavyo Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mbunge mtaona inafaa kushauriana kwa matumizi ya eneo hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Tumemaliza muda wetu wa maswali kwa siku ya leo na sasa ni wakati wa matangazo. Tutaanza na matangazo ya wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Tuna wageni waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ambao ni wageni wawili wa Mheshimiwa Spika kutoka *Serena Hotel* kuna Seraphin Lusala, Mkurugenzi wa Mauzo na Masoko Dar es Salaam, *Serena Hotel;* na David Sem, *Country Sales Manager, Serena Hotels.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Hamis Dihenga, Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Profesa. Karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Kuna mgeni mwingine wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, *Liaison Officer* kutoka *UN-WFP* Dodoma.

Kuna wageni 25 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Watumishi Wanawake kutoka Kata ya Pwaga, Jimbo la Kibakwe. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mapadre wa Peramiho, Jimbo Kuu la Songea kutoka Mkoa wa Ruvuma. Karibuni sana, Mapadre wetu kutoka huko Peramiho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kutoka Kampuni ya Heinken. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine, ni mgeni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, rafiki yake kutoka Jijini Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati ya Siasa ya Wilaya wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya wa Wanging'ombe; Mheshimiwa Frank Chaula, Mwenyekiti wa CCM, Wilaya; Ndugu *Highness* Munisi, Katibu wa CCM, Wilaya; Mheshimiwa Claudia Kitta, Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe; Ndugu Veronica Sanga, Katibu Tawala Wilaya; na Mheshimiwa Agnepe John Pangile, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wanging'ombe. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Noah Saputu Mollel, ndugu zake kutoka Arumeru Mashariki, Mkoa wa Arusha. Karibuni sana.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Cecilia Paresso, wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa kutoka Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ally Kassinge, Kiongozi wa CWT kutoka Chamwino, Mkoa wa Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Rashidi Shangazi, ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Augustine Vuma, wanafamilia kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa George Mwenisongole, rafiki yake kutoka Jijini Dodoma. Sijamwona, karibu. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambapo:-

Wapo wageni 50 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Tuna wageni watano ambao ni familia ya Yona Magwai kutoka Nzuguni, Jijini Dodoma. Karibuni sana katika Bunge letu waheshimiwa wageni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

Karibu Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kupata nafasi ya kutoa mchango wangu, labda tutulizane kwanza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tutulizane au tufanye kwa utaratibu mambo yetu ili tuweze kusikia michango ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naipongeza Wizara, hii kazi wanayoifanya ni kubwa kweli kweli, lazima tuwapongeze. Tuipongeze Serikali yetu na Mheshimiwa Rais kwa zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoanza kuwashauri ni naiomba Wizara ipitie historia ya mabadiliko ya elimu hapa nchini na hasa waanze kwenye kipindi, tunapata uhuru na miaka 10 ya kwanza ya uhuru, Mwalimu alifanya mabadiliko katika hiyo miaka

10. Kwa nini inabidi wapitie hapo? Ni kwa sababu inawasaidia kujua mahala ambapo hapakufanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu wakati anafanya mabadiliko kati ya mwaka 1961 na 1971 toka kwa zilizokuwa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu, alikuwa na Wizara moja tu ya Elimu na ukiangalia alivyokuwa amepanga Wizara ya Elimu ndiyo ilikuwa karibu sana na Ikulu. Bajeti ya Mwalimu karibu 20% mpaka 30% ya bajeti ilikuwa inapelekwa elimu. Alifuta darasa la nane, alitaifisha shule na shule zilikuwa na walimu kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka shule yangu ilivyotaifishwa mwalimu wangu wa *English* wa *form one* alienda kufundisha *English Makerere University*, alikuwa anaitwa *Brother* Richard. Mwalimu alifuta Mitihani ya *Cambridge* ya C*ommonwealth*. Kwa hiyo hii kazi tunayoifanya ni kubwa, tuwaunge mkono na tuisaidie Serikali, lakini watu wanabadilisha mitaala siyo tu kwa sababu ya kubadilisha mitaala. Kwenye karne ya 20 na 21 kila Taifa linajitahidi liyashinde Mataifa mengine kwenye nyaja ya teknolojia, sayansi na ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, ni kila Taifa linataka lipate bidhaa nyingi sana za kuuza, *export oriented economic strategy*. Ili kufanya hayo yafanikiwe vitu vitatu vinahitajika, mfumo wa elimu uwe mzuri ndiyo tunauongelea, Taifa liwe la watu walioelimika ni muhimu sana kuwa na *educated population,* halafu na wananchi wawe na ari ya kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechukua mifano miwili tu wakati najaribu kutafakari mabadiliko yetu. Je, tuko sawa awa? Je, ni ya muhimu kufanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukichukua hiyo mifano usichukue mifano kwa watu ambao ni dhaifu, lazima uende kwenye Mataifa ambayo siyo dhaifu, lakini ambayo mnafananafanana, kwa hiyo, nimechukua mfano wa kwanza wa Seychelles. Seychelles ni kakisiwa kadogo, lakini tutatumia *ratios proportion* kulinganisha, mtu asije kusema Seychelles ni wachache, hapana ni suala la *statistics ratios*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Seychelles kwa sababu ndiyo Taifa tajiri namba moja Afrika, *GDP* yake ni zaidi ya dola 20,000, hivyo ni vigezo vya *World Bank* na *IMF,* lakini kuna kigezo cha pili ambacho hatukitumii sana, *HDI* yaani *Human Development Index*. Sasa nikianza kueleza hiki muda wangu wote utaishia huku. Kwa kifupi ni kwamba, hiyo ndiyo inatoa kipimo cha maisha bora ya kila Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Seychelles ni nchi pekee kwa Afrika ambayo ipo ngazi za juu, *HDI* yake ni *0.802*, Tanzania ni *0.532* na Kenya wanatuzidi wao ni *0.601*. Sasa angalia mtindo wao wa elimu, wao wana sita, tatu, nne, nne *(six, three, four, four)* maana yake ni hivi, *primary school* wanaenda miaka sita, *lower primary school* miaka mitatu, *upper primary school* miaka minne na chuo kikuu ni miaka minne. Kwa hiyo, unaona ni karibu tunalinganalingana na mabadiliko ambayo Wizara ya Elimu imetuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoacha Bara la Afrika nikaenda Bara la Asia ambalo limeendelea, Asia imeendelea kwelikweli, kule nimechukua *South Korea*. *South Korea GDP* yake *per capita* ni zaidi ya dola 32,000, *HDI* yake ni *0.717*. Sasa angalia mtindo wake wa elimu, *South Korea* ni sita, tatu, tatu, nne; maana yake ni kwamba, kama mtu anaenda moja kwa moja, *elementary school* ni miaka sita, *middle school* ni miaka mitatu, *high school* ni miaka mitatu na chuo kikuu ni miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo ambao hawaendi chuo kikuu wanaenda kama sisi *VETA,* wao wanaita *junior colleges,* hao wanaenda kwa miaka miwili mpaka mitatu. Kwa hiyo, kwa kulinganisha Afrika, nasema kwamba, Tanzania mabadiliko yetu ni sahihi. Sasa natoa ushauri, kwanza ni lazima tukajipime kimataifa kwa haya tunayoyafanya, maana tunaweza tukajisifia sisi wenyewe tu, lakini twende huko tukajipime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo cha kwanza naomba Tanzania ishiriki kwenye kitu kinaitwa *PISA,* siyo *pizza.* Maana yake ni *Program for International Student Assessment,* hii inapima watoto wenye miaka 15 kama mambo waliyojifunza shuleni

yanaweza kutatua matatizo yanayowazunguka duniani, twende huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo cha pili ni *TIMSS,* yaani *Trans International Mathematics and Science Study*. Hii inachuka watoto walioko kwenye *grade* ya nane, wanaangalia ujuzi wao na maarifa waliyopata shuleni. Sasa haya ni mashindano yanayofanywa Kitaifa na Tanzania, naomba baada ya miaka miwili mitatu, Mheshimiwa Profesa aende kule *PISA* na *TIMSS* ndiyo tutajua kwamba, tuko sahihi, vijana wetu wa miaka 15 wakapambane kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili ni juu ya mambo yote tunayofanya. Naomba Mheshimiwa Profesa kwa sababu, hivi vitu unavifahamu uende ukafufue *professional societies* ambazo zimekufa kwa sababu, haya matatizo ya hisabati tungewapatia Chama cha Hisabati cha Tanzania. Matatizo ya *chemistry,* huwezi ukajadili tu mambo ya *chemistry,* wapatie hicho chama. Kwa hiyo, Waziri akafufue hizi, tena ni *the cheapest consultant bodies. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa tatu ambao kusema kweli, naomba kusema ni kwamba, sikuafiki sana, ni haya ya tahasusi za *form five* na *form six* yaani *combinations*. Nimeangalia Profesa anazo 65, *combinations* 65 kwenye *high schools* na nimejaribu kuzichambua; Sayansi ya Jamii *combinations* tisa, ni 13.8%; Lugha *combinations* 11, ni 16.9%; Biashara saba, ni 10.8%; Sayansi saba, ni 10.8%; Michezo saba, ni 10.8%, Sanaa/*Arts* 16, ni 24.6%; na Elimu ya Dini ni nane, ni 12.3%. Kwa hiyo, ukichukua haya mapendekezo hizi *combinations* walizozifikia ukichukua vyumba viwili vya *science* na *arts,* hapa hatutayarishi Taifa kwenda kwenye *science*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wengi watajaa chuo kikuu, tutakuwa na wanafunzi wengi kwelikweli chuo kikuu, lakini katika hao ambao watakuwa wanasoma *real science* ni asilimia 10 tu. Kwa hiyo, kama tunataka kwenda kwenye *science* na *technology* ni lazima tubadilishe hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni la chuo kikuu, muda hautoshi. Vyuo vikuu vyetu, ndugu zangu, Mheshimiwa Profesa siyo kazi yako. Mtu akiitwa Profesa inafaa ajitegemee, ajitume, atafute fedha mwenyewe, lakini akishindwa inabidi tumlee, lakini vyuo vyetu vikuu vya sasa hivi vimekuwa *nationalistic,* yaani ni vya Kitanzania mno, havina afya kitaaluma. Havina afya kwa sababu, huwezi kukuta Maprofesa wametoka nchi nyingine kama *visiting professors* wapo kwenye vyuo vyetu, huwakuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kuhusu *External Examiners.* Nilivyokuwa bado mwanafunzi alikuwa anatoka *Cambridge,* Uingereza. Sasa hivi hawa wa madini, nadhani *External Examiner,* wanaweza kwenda kumchukua mchimbaji mdogo mdogo Musoma? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia juu ya *exchange programs. Exchange programs* kwa wanafunzi ni lazima ziwepo na mwisho ni *training schools,* hii ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo namalizia na wala sitakuomba muda. Nachukua jinsi nilivyojifunza *geology* miaka mitatu hapa hapa Tanzania na sasa hivi *geology* ni miaka minne. Nilivyokuwa mwanafunzi kila Jumamosi tulikuwa tunaenda *field* halafu tulivyomaliza mwaka wa kwanza, tukazunguka maeneo mbalimbali tunafanya *mapping*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa pili, nilienda kufanya mazoezi Zambia, tukaandika ripoti. Sasa Mheshimiwa Profesa tatizo lingine ni hii ya wanafunzi kujitegemea, ni lazima uwekeze hela nyingi ili wanafunzi wakafanye *professional training,* ndiyo maana wanafunzi wa wakati huo, hata wanafunzi wangu, wameenda kufanya kazi Ghana na Australia wanakubalika, lakini wa sasa hivi hawawezi kukubalika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo. Kabla hatuajendelea na mchangiaji ambaye

nimemtaja, tuna Tangazo moja hapa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa nje ya Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kikazi kuanzia tarehe 8 Mei, 2024, kwa hiyo, wakati hayupo Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum ndiyo atakuwa anakaimu nafasi hiyo mpaka atakaporejea au atakaporejea Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nilimtaja Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Naomba nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake uliotukuka ambao sote tunashuhudia mafanikio makubwa katika sekta zote muhimu za ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza kwa kutoa dira ya mwelekeo wa mageuzi katika Sekta ya Elimu. Alitoa dira hiyo katika Bunge lako Tukufu wakati alipolihutubia tarehe 22 Aprili, 2021. Hotuba hiyo ndiyo ambayo imezaa Sera Mpya ya Elimu, Toleo la Mwaka 2023 na mitaala mipya ambayo imeanza kutekelezwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa hakika anafanya kazi nzuri, msaidizi wake Mheshimiwa Kipanga, Katibu Mkuu Profesa Nombo pamoja na watendaji wote. Hakika wanafanya kazi nzuri ya kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Taasisi ya Elimu ambayo ndiyo imefanya kazi ya kusimamia mabadiliko haya ya mitaala ambayo yameanza kutekelezwa ambapo wameanzisha

na mkondo wa elimu ya amali. Ufanisi katika utekelezaji wa mitaala unahitaji mambo mengi ikiwa ni pamoja na mwanafunzi mwenyewe, mwalimu, mazingira ya shule, vifaa vya kujifundishia pamoja na mfumo wa ufuatiliaji na udhibiti wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekeze mchango wangu upande wa walimu kwa sababu, natambua kwamba, mwalimu ndiyo nguzo na nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa mitaala. Naipongeza Serikali kwa hatua ambazo imezichukua kuwapitisha walimu na kuwapa mafunzo kuhusu mtaala mpya, lakini mafunzo hayo bado hayajatosheleza. Naomba mafunzo hayo yawe endelevu kwa sababu, mtaala huu mzunguko wake ni wa miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi elimu msingi ya lazima imekuwa ni miaka 10, ambapo ni miaka sita ya elimu msingi na miaka minne ya sekondari. Kwa hiyo, ufanisi wa utekelezaji utategemea uimara na umahiri wa walimu katika utekelezaji wa mitaala, kwa hiyo, mafunzo kazini yawe ni endelevu kwa upande wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iangalie shule ambazo zina uhaba wa walimu, lakini naipongeza imekuwa ikiajiri walimu na tayari kuna tangazo la kuajiri walimu wengine. Kwa hiyo, Serikali iendelee kuajiri walimu wengi zaidi na kufanya msawazo wa walimu ili shule zile ambazo zina uhaba wa walimu ziweze kupata walimu wa kutosha na hasa ukizingatia hapo alipomalizia Profesa aliyekuwa anachangia, Mheshimiwa Muhongo kwamba, elimu inataka mafunzo kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kufanya mafunzo kwa vitendo ni lazima uwe na walimu wa kutosha, uwe na vifaa vya kutosha na uwe na rasilimali za kutosha katika kutekeleza mtaala katika mkondo wa amali. Kwa hiyo, ufanisi katika utekelezaji wa mtaala huu unategemea sana umahiri wa walimu na uwepo wa vifaa vitakavyowawezesha wanafunzi kufanya mafunzo yao kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa elimu pia, tuangalie suala la udhibiti ubora. Wadhibiti ubora ndiyo jicho la Serikali katika kuhakikisha kwamba, elimu inatolewa kwa viwango ambavyo vimewekwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wadhibiti ubora waangaliwe kwa jicho la kipekee. Natambua na napongeza jitihada ambazo Serikali imezifanya katika kuwawezesha wadhibiti ubora, kuwajengea ofisi wale ambao walikuwa hawana ofisi, karibu halmashauri zote wamejengewa, kuwanunulia magari na kuwanunulia pia, vitendea kazi, vifaa vya ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wawezeshwe kufika katika shule ili waweze kufanya ukaguzi na kujiridhisha kama mitaala hii mipya ambayo imeanza kutekelezwa Januari, 2024, inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mageuzi haya ni makubwa kwa hiyo kusipokuwepo na usimamizi na ufuatiliaji wa makini malengo yaliyokusudiwa yanaweza yasifikiwe. Kwa hiyo, niombe sana Idara ya Udhibiti wa Elimu iwezeshwe ili iweze kufanya kazi zake kwa kuzingatia mpango kazi uliowekwa, lakini kubwa niombe ushauri unaotolewa na wadhibiti ubora wa shule ufanyiwe kazi, maana mara nyingi wamekuwa wakikagua, wakiandika *report* zao, lakini zinakuwa tu ni kama kitu cha kawaida ambacho hakipewi uzito ambao unastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye huu mtaala kuna mkondo wa elimu ya amali. Tunatambua kuna changamoto kubwa ya uhaba wa walimu wa mafunzo ya amali. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iwe na mpango mahsusi wa kuandaa walimu kwa ajili ya mkondo wa elimu ya amali kwa sababu tunafahamu kwamba shule za ufundi hapa katikati kulikuwa na utaratibu ambao ulizifanya zikawa hazifanyi kazi. Kwa hiyo, walimu wengi walikuwa wameshaondoka wamekwenda kufanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mipango madhubuti na hasa ukizingatia hotuba ya Waziri inaonesha kwamba katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 wana mpango wa kujenga shule 100 za ufundi na Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba

anategemea shule 26 zitaanza kufanya kazi mwaka 2025. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri awe na mipango thabiti ya kupata walimu kwa sababu kama nilivyosema walimu ndio nyenzo na nguzo muhimu katika kuhakikisha ufanisi wa mitaala ambayo imewekwa na hii pia inaenda katika vyuo vya ufundi stadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonesha kwamba chuo pekee kinachotoa mafunzo ya ufundi stadi cha Morogoro katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, kimedahili wanafunzi takribani 352 ambayo ni sawa na 53% ya lengo. Sasa kama tunaongeza *VETA*, tumekamilisha kujenga *VETA* 29, ambapo 25 ni za wilaya na nne za mkoa. Pia tunaendelea na ujenzi wa *VETA* 65. Ni dhahiri kwamba kama udahili hatufiki hata lile lengo lililokusudiwa kuna kazi ya ziada ambayo inapaswa kufanyika ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na walimu wa kutosha ili lengo la kuwa na wahitimu ambao wana ujuzi, wana umahiri liweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusiana na elimu maalum. Elimu maalum katika nchi yetu imekuwa ikifanyika vizuri sana na tumekuwa ni mfano kwa sababu mazingira yetu ya kutolea elimu tumeendelea kuyaboresha na tumeendelea kuhakikisha kwamba tunaweka bajeti ya kutosha kwa ajili ya kununua vifaa visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, lengo la Serikali ni kuendelea kuhakikisha kwamba inatoa elimu bora kwa wote ambayo inazingatia usawa kwa watoto wote hata wale wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na hatua ambayo Serikali imechukua ya kuandaa mwongozo wa shule ya nyumbani wa mwaka 2023 ambao mwongozo huo unatoa fursa kwa watoto wenye mahitaji maalum ya kiwango cha juu kuweza kupata elimu wakiwa nyumbani. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, wataona ni namna gani ambavyo Serikali imejizatiti kuhakikisha kwamba hakuna mtoto anayeachwa kwenye elimu hata yule mwenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Wizara iendelee kuhakikisha kwamba inatangaza huduma hii ya kuweza kutoa elimu mtoto anapokuwa nyumbani kwani bado kuna tabia ya baadhi ya wazazi kuwaficha nyumbani watoto ambao wana mahitaji maalum. Hivyo basi pamoja na mipango mizuri ya Serikali bado kunakuwa na watoto ambao wanaachwa. Tuendelee kutoa elimu, tuendelee kuhakikisha kwamba watoto wote wanaenda shule na kupata elimu iliyo bora. Pia tuboreshe mafunzo kwa ajili ya walimu wenye mahitaji maalum na kuhakikisha kwamba wanapomaliza mafunzo yao wanapangiwa katika shule ambazo zina wanafunzi wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako. Waheshimiwa Wabunge kabla sijaendelea na mchangiaji ambaye nimemtaja, kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Augustino Vuma ambao hawakutambulishwa ipasavyo hapo asubuhi. Walitambulishwa kama ni wanafamilia lakini ni mke wake na shemeji yake kutoka hapa Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mke ndiyo yupi? Tunaomba tumwone mke wake Mheshimiwa Vuma. Karibu sana Mrs. Vuma katika Bunge letu pamoja na shemeji yake. Karibuni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Shally Raymond wajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, napata shida kidogo, wamezungumza maprofesa sasa naomba nami nifuatefuate mkondo huo wa maprofesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Elimu; Mheshimiwa Profesa Mkenda pamoja na Mheshimiwa Omari, Watendaji wote wa Wizara hasa

katika taasisi mbalimbali chini yake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kuna mambo machache tu ambayo bado inabidi tuyasemee katika kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaanza kwa kupongeza sana sana, suala la uboreshaji wa elimu kwa ujumla nikianza na majengo ya vyuo pamoja na maslahi kwa mikopo. Katika uboreshaji Kamati ilipita kuangalia haya majengo yaliyoongezwa katika vyuo, lakini niseme tu kwa masikitiko kile Chuo cha Nyerere Kigamboni, Unguja pamoja na Pemba bado Wizara inatakiwa iweke nguvu kwenye vyuo hivyo. Ujenzi au uboreshaji wa majengo unakwenda polepole sana, sasa sijui ni fedha bado haziendi huko, hatuelewi lakini sisi tunachotaka kuona pale majengo hayo yanaenda kwa *speed* pamoja na Nelson Mandela bado ujenzi wake haufurahishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye uboreshaji wa mikopo; Serikali imejitahidi sana kuongeza fedha za mikopo karibu shilingi bilioni 700, lakini kwenye bajeti ya elimu kuna ile shilingi trilioni 1.9. Maana yake ni hivi, kiwango kikubwa ndani ya hiyo trilioni kinakwenda kwenye mikopo. Sasa maana yake ni hivi ingawa 60% inaenda kwenye mikopo, lakini bado mikopo hiyo haitoshi, kwa hiyo zinazobaki zinakwenda kwenye maendeleo. Ndiyo maana tunasema Serikali inabidi iongeze fedha za maendeleo kwenye Wizara ya Elimu lakini pia fedha za mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo mikopo tumeweka ni sheria, hao wanafunzi wana haki ya kupata hiyo mikopo. Kwa hiyo, sisi tunasisitiza kwamba Serikali itafute mbinu, Bodi ya Mikopo itafute mbinu ya kuongeza fedha kiasi ambacho kisaidie watoto wetu wote wanaostahili wapate mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala ambalo nimelizungumza toka naingia Bunge hili 2020, wakati tunaanza Bunge 2021, kuhusu suala linalohusu *teaching hospitals.* Vyuo vyote au nchi zote *universities* zikiwa na *teaching hospitals* ndio zinazofanya vizuri sana. *Teaching hospitals* pamoja na *military hospitals* yaani hospitali za kijeshi pamoja na hizo *teaching*

*hospitals* za *university* ni katika hospitali zinazofanya vizuri sana. Ninachoshangaa mpaka leo, hivi kuna mvutano gani kati ya Muhimbili na Mloganzila? Kuna mtu mmoja tu pale sijui niseme ni Mkurugenzi, hataki kuwapa Mloganzila *University* waichukue kama *teaching hospital.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kigugumizi gani hapo ni suala la maslahi au ni nini? Leo hii mwalimu aliyekuwa anafundisha hapo *UDOM,* Mhadhiri aliyekuwa anafundisha *UDOM* ndiye yule aliyesaidia kugundua upandikizaji wa uti wa mgongo, tunaita uboho, uboho mnisikilize vizuri, aliyesaidia ni huyo Mhadhiri kutoka *UDOM*. Sasa leo wanaposema hatuwezi kuziachia hospitali vyuo vikuu wakati wataalam ndiyo wanatoka kwenye hivyo vyuo, haileti afya kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watakapokuja hapa waniambie Wizara ya Elimu wana shida gani na Wizara ya Afya. Kwa nini wasikae pamoja wakaangalia? Tulikwenda pale Mloganzila kuna mambo nusu yanafanyika na *MUHAS,* nusu wamewaachia hiyo *University* yaani wala havieleweki. Niombe suala hilo la *teaching hospital* sasa lifikie mwisho. Kama wamewanyang'anya Mloganzila, kama wamewanyang'anya Benjamini, basi wajipange sasa, Waziri wa Mipango yuko hapa, wajipange watuambie au wanawajengea *teaching hospital* zao wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye maslahi na hilo nimelizungumza, hawa wakuu wa vyuo…

**MHE. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. Taarifa, Mheshimiwa Dkt. Bashiru.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa kwamba kwenye Ilani hii ya Chama Cha

Mapinduzi tumeahidi *teaching hospitals*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Serikali wajipange ama wawarudishie hizo hospitali zilizopo au wawajengee hospitali za mafunzo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, ahsante sana daktari mbobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nije kwenye maslahi; nimezungumza kuhusu maslahi ya wakuu wa vyuo. Hawa watu wanakaa wanaangalia watoto pamoja na kufundisha, wanaangalia na *discipline* katika vyuo vyetu. Sasa hivi Waheshimiwa Wabunge watanikubalia kwamba vyuo vikuu vimetulia na kazi kubwa wanaifanya hao wakuu wa vyuo. Leo hii kuna mmoja aliongea hapa wiki iliyopita, aliongea kwamba hata ukiangalia sijui hizo *per diem* yaani maslahi yao wanalipwa chini, halafu kuna walimu pale pale wanafundisha nao. Hivi kweli kutakuwa na kuheshimiana kweli? Hebu tuangalie haya maslahi. Waliniambia kwamba hili suala tumelichukua tunalipeleka, tunalichukua tunalipeleka, leo wanalichukua wanaliweka wapi? Naomba suala hili walichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wametulia tu wenyewe hawa ma-*VC*, maprofesa wametulia hawana kelele, wamekaa lakini wanaumia moyoni, hatuwatendei haki. Profesa anajua, hatuwatendei haki, wapo wametulia lakini wanaumia. Hamjasikia wanaandamana wala wanagoma, wanaenda wanafanya kazi zao, hebu leo hilo suala lifike mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naongea kama wenzangu pia nasisitiza umuhimu sasa wa kuona tunaongeza muda wa ku-*retire*. Leo wanalalamika hapa yaani Tanzania nzima tuna maprofesa 93 *imagine* na tunatakiwa tuwe na maprofesa 516, lakini *full professors* hao tunao 93 tu. Hebu wafikirie, halafu wakifika miaka 70 wanasema waondoke wengine hawajawajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko mimi nilifanya *study* yangu, wakati na-*study*, profesa aliyekuwa ananisimamia mimi alikuwa na miaka 85 *and he was very good upstairs*. Waongeze *retirement* halafu wahakikishe kwamba wanawaleta na maprofesa kutoka nje kama alivyosema Profesa Muhongo. Tuna maprofesa hapa ukifika Chuo Kikuu unakuta Profesa Komba, Profesa Kiwia, Profesa sijui Haule. Tunataka ukifika unakuta mchanganyiko wa maprofesa, Profesa Hoffman, Profesa sijui San Chan, lazima tuwape uhuru *universities* waajiri maprofesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri tu maprofesa au Waziri kwamba hata vyuo vyetu jamani *exchange programme* siyo lazima uende nje. Mtu anakaa anasoma pale *UDSM* miaka minne, hebu tutengeneze *exchange programme* za hapa ndani. Aende hata pale *MUST* kijana anakaa pale anasoma mambo, anatembelea *UDOM* yaani wanabadilishana *within our universities*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nililisema kwamba hebu kila *university* ijitahidi kulea jiji au halmashauri ili tuone ule utafiti wanaofanya uonekane kule…

*(Hapa kengele ililia kuashira kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nusu dakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimwombe Mheshimiwa Waziri, sasa hivi tunasema watoto, hawa watoto pia ni watoto wake. Wizara ya Elimu ihakikishe kwamba unafuta kabisa haya mambo ya watoto kupelekwa kuchezwa au unyago wakiwa wadogo. Haya mambo yanaharibu, hawa ni watoto wake, wao wasome shule siyo watoto wadogo, darasa la kwanza mpaka la tatu wanapelekwa kuchezwa hasa mikoa hii ya kusini. Watoto wanachezwa, hawa ni watoto wake awalinde Mheshimiwa Profesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mheshimiwa Shally Raymond na Profesa Patrick Ndakidemi ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie kwenye hili jambo ambalo ni la msingi. Ni sekta ambayo inagusa kila mtu katika nchi hii na hata nje ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaothubutu kutekeleza mambo magumu ni wachache sana hapa duniani na naomba niseme kwamba Mheshimiwa Rais wetu kweli ana uthubutu…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba tutulie, tumtazame na tumsikilize Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze sana kwa kukubali kutengeneza sera mpya na mitaala mipya ambayo itaenda kubadilisha kabisa mfumo wa elimu nchini. Mfumo siyo kitu rahisi sana kubadilisha ni kitu kigumu na ni kitu ambacho ni nyeti, ni kitu ambacho lazima kweli twende kwa usahihi wake. Profesa Muhongo alituelimisha hapa lakini nataka niseme kwamba ni kitu cha msingi sana, kwa hiyo tukichezea tutakuwa tumeharibu sana shughuli zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Profesa Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Omari na Timu yake yote kwa kazi ambayo wanafanya, tunaiona. Najua ni ngumu lakini kama anapata usingizi, basi naye ni mtu anayethubutu sana, lakini ukweli ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sitaki kuingia kwenye viatu vya wale maprofesa walioanza kuzungumza. Nianze kwenye jimbo langu, kule kwenye jimbo langu nina wakazi 255,000 na hatuna Chuo cha Ufundi cha *VETA*, ina maana kwamba mwanafunzi aliyemaliza shule ya msingi au sekondari akitaka

kupata mafunzo ya ufundi lazima atumie shilingi elfu nne mpaka elfu kumi kwenda Moshi Manispaa ambako ndiko karibu vyuo vyote vya *VETA* vimewekwa. Sasa naomba sana kwamba kusema kweli hili halitatufikisha mbali, naomba sana Serikali ione namna gani ya kutupa fedha tuweze kujenga angalau chuo kimoja cha *VETA* kwenye Jimbo langu la Vunjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna shule moja pale kwenye kata ya Mwika Kaskazini inaitwa Shule ya Lole ilikuwa shule ya awali, msingi na ufundi wa *VETA* lakini kuanzia mwaka 2000 shule hii haijatoa tena masomo ya ufundi kwa sababu imekosa walimu na karakana zake zimekuwa ni chakavu sana. Pia, majengo yale hayafai yanastahili kupata ukarabati ili tukipata na walimu basi tunaweza pia kuanza shughuli ya kuanza kufundisha vijana pale. Hayo ni ya Vunjo, ya Vunjo yako mengi lakini ngoja niseme hayo mawili ili niweze kuzungumza na mengine ambayo nafikiri ni ya muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Muhongo, lakini kitu ambacho hakukisema nafikiri ni ile nadharia ya *education for Self-reliance* ilikuwa inalenga sera hii hii ambayo tunataka kutengeneza sasa hivi, isipokuwa kwa namna moja au nyingine tulitekeleza bila kuwa *consistent* na bila maandalizi ya kutosha. Kwa hiyo ikaonekana baadaye tuka-*abandoned* ule mfumo wa *education for self-reliance* ambapo watu walijifunza nadharia, lakini na vitendo pia vilikuwepo. Nakumbuka tulikuwa tunalima sana, lakini hatukuibuka kuwa wakulima wazuri kama tulivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema kwamba tumejaribu lakini tukashindwa, tukaacha tukarudi kule kule, kwa sababu mfumo ni vigumu sana kutekeleza na unahitaji rasilimali nyingi ya fedha na watu. Kwa hiyo, nasema kwamba, sidhani kama bajeti ambayo imetengwa na hata hii nimekuwa naiangalia, haitatosheleza. Kama kweli tunataka kwenda na kasi ambayo Mheshimiwa Rais anaonesha, anataka kwenda nayo na Wizara inataka kuonesha kwamba inaweza kwenda nayo, basi ni lazima tutenge fedha za kutosha kutengeneza miundombinu

ambayo inastahili hususan kwenye mkondo wa amali ili watu waweze kujiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya sasa siyo ile ya zamani, naona wanazungumzia masuala ya seremala na masuala ya ufundi uwashi, sasa hivi kwenye mkondo wa amali tunahitaji kwenda na teknolojia ili tujue kwamba kama ni ufundi wa magari siyo yale magari ambayo unachochea, ni magari ambayo yanatumia umeme na mfumo wa kidijitali ambao ni wa kisasa, hivyo hawa vijana lazima waandaliwe na vifaa kwenye zile karakana ni lazima viendane na mahitaji hayo ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kama tutaenda kujenga ili mradi tunajenga madarasa na kuweka vifaa vya zamani ambavyo ni vizito sana, hatutafika mbali, *by the time* tunafika kule utakuta wale vijana hawatapata kazi na hataweza kujiajiri kwa sababu hakutakuwa na mahitaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inaonekana haitoshi, kwa sababu gani? Ukiangalia *data* zilizo kwenye randama, kwa mfano, nalenga tu kwenye upande huu wa mkondo wa amali. Katika mwaka uliopita wameongeza uandikishaji wa wanavyuo lakini kwa upande wa *technical education training* utakuta kwamba shule ziliongezeka na ndizo zilizoongeza wanachuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shule za *TET (Technical Education Training)* zilikuwa 465 Mwaka wa Fedha 2022/2023, zikaongezeka zikafika jumla ya vyuo 474, vimeongezeka vyuo tisa kwenye huo mwaka ambao tunatekeleza bajeti yake, kati ya hivyo Serikali haikuongeza chuo hata kimoja, vyuo vyote tisa vimetokana na *private sector*. Sasa, kama kweli tunajenga huo mkondo tutaujenga bila kuongeza vyuo na tutategemea *private sector?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo katika *VETA*. Vyuo vya *VETA* jumla vilikuwa 687 ilipofika Juni, 2023. Katika miezi hii tisa vimeongezeka 145 na kufikia 830. Kati ya hivyo nyongeza ya 145 Serikali imeongeza chuo kimoja tu na vyuo vingine 144 ni vya sekta binafsi. Sasa najiuliza kwamba, je ni kweli kuna nia ya

kwenda na kasi hiyo ambayo inastahili? Tunataka 2027 tuanze kutekeleza *full-blown?* nafikiri tunahitaji bajeti sana kwenye suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba *strategy* bila kuwa na *execution* inakuwa ni ngumu sana kufika mbali. Kwa hiyo, nafikiri lazima watu wajipange zaidi na pengine tujaribu kuiga ili kuona hawa wenzetu wamefanyaje katika nchi zile. Seychelles ambayo ameitaja Mheshimiwa Muhongo iko juu sana, kwa Afrika ni namba moja kwa mfumo bora wa elimu. Kwa hiyo, tujaribu kujifunza ni kitu gani na wametekelezaje ili tusije tukarudia makosa na nafikiri kule tulikotoka tungeweza kwenda *incrementally* tukaboresha ile Sera ya *Education for Self-Reliance,* halafu tukaiongezea vitu vingine ambavyo havikuwepo hususani kuboresha namna karakana ambazo zilikuwa zinatumika, zile *workshops* kwenye shule zetu zilizokuwepo *middle schools,* tungeenda vile pengine tungekuwa tuko mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, nilimtaja Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mungu kwa kuwekwa hapa leo na kuweza kuzungumzia Wizara hii ya Elimu, niseme kwamba imekuwa vizuri Profesa Mkenda ametuletea hotuba yake ambayo inajadilika na imewekwa kwenye kitabu kizuri sana hata hii niliyoshika ni randama tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema tukajua kwamba mtu anaweza kukuibia kila kitu *tangible* au *intangible* lakini hawezi kukuibia elimu yako kwa sababu imefichwa na Mungu ndani ya ubongo kwenye *medulla oblongata*. Unakuwa nayo wewe mwenyewe na unaimiliki wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Profesa Mkenda kusimamia Wizara hii na timu nzuri sana, toka jana tunazungumzia maprofesa, Katibu Mkuu naye ni Profesa ina maana kuwa elimu kwao imetua na imebarikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshika hiki kitabu cha randama, kuna mambo ambayo naomba uniruhusu ninukuu. Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yameainishwa katika hati idhini iliyotolewa tarehe 7 Mei, 2021 *(GN. 385)* na marekebisho yalitolewa tarehe 24 Januari, 2022 *(GN. 57b)* ambapo Wizara imeelekezwa kutekeleza majukumu yafuatayo, yako pale majukumu kama 17. Ni mengi lakini siendi huko kote, mimi leo nimesimama kuzungumzia jukumu moja tu, kusimamia maendeleo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia elimu, tukienda Serikali za Mitaa kuna elimu na kila mahali, mimi nimekwenda kwenye kusimamia maendeleo ya elimu ya juu nikiwa na maana ya vyuo vya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetamkiwa safu ya maprofesa walisoma wakapata *PhD* zao wakawa madokta na baadaye wakaandika wakawa ma-*professorial* ambacho sasa hicho ndicho kiwango cha juu ulimwenguni. Tunao na wanaendelea kufundisha watoto wetu. Kwa nini nimependa kuwazungumzia? Kwa sababu nimeona kwamba kuna eneo ambalo watu hawa wanapunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi *Cooperative University* wakati imetoka chuo cha kutoa *Diploma* na mengineyo na bado ikashirikishwa na kile Chuo cha Sokoine *University then* ikapewa kuwa *University*, walichukuliwa maprofesa pale, wengine wakiwa *Associates Professor* na wengine *full Professor* wakapewa *contract* wakafundisha kwa moyo mzuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameisema pia Mheshimiwa Dkt. Ntara kabla yangu kuwa Maprofesa hawana hili la kusema kugoma wala nini, walikuwepo maprofesa kama 15

wamefundisha na wengine tumefanya *Masters* pale tume-*graduate* lakini mpaka leo wanadai stahiki zao na hawajawahi kupewa. Jambo hili wakanikabidhi nikazungumza na Waziri wa Fedha, madai hayo yakawa hayajafika. Nikazungumza kwenye Wizara ya Elimu wakasema wamekwishapeleka fedha, nikarudi Wizara ya Fedha, Naibu Waziri wa Fedha akaniambia madai hayo yameshahakikiwa yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba chonde chonde, baadhi yao wameshakufa, baadhi yao wamebakia na familia zao zina-*suffer*, Wizara iwapatie Maprofesa wale stahiki zao. Pia, namshukuru Mungu leo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wetu wa Fedha nchini yuko hapa na anakisikia tena hiki kilio. Pia, wao wako kule sasa hivi wananisikiliza, maana yake waliona walipontuma nimeshaulizia swali na swali halijaja, leo niseme wazi kwamba maprofesa wanasononeka! Nisingetaka wapate *stress*, walipwe ili waendelee kufundisha. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee katika mchango mzuri unaoendelea. Hata stahiki zao za nyumba *(house allowance)* madai ni mengi, naomba na hilo katika hizo stahiki zao walipwe na *house allowance* fedha ambazo hawa maprofesa wanastahili, madai ni mengi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea sana hiyo taarifa ya Daktari, anawajua wenzie zaidi, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ameshatoa hiyo taarifa naomba hilo nihitimishe. Mwaka wa Fedha 2023/2024 hii Wizara walikuja hapa wakaomba zaidi ya 1.6, tukawapa lakini mpaka sasa hazijatoka zote. Tatizo liko wapi? Kwa sababu ukiniuliza ni Wizara gani ipewe fedha nyingi zaidi hapa nchini? Nitakwambia ni Wizara ya Elimu kwa sababu elimu ndiyo itamkomboa kila mtu. Ukiwa na elimu utajua kulima, utaweza kilimo, utaweza mifugo, utaweza kujitunza, hakuna kipindupindu. Ukishapata elimu iwe ni ya *level* ya chini ya *primary, secondary,* ukishaelimika tu unaweza kujitambua na kujisimamia. Sasa kwa nini elimu isipewe kipaumbele? Mimi leo ningesema wapewe hata trilioni tatu, lakini basi kwa vile inaingia maeneo tofauti hadi kwenye Halmashauri, mpaka wapi, nyingine huwa zinakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tu niulize kwa sababu jambo hili linazungumzwa kichini chini, ni nini kilichopelekea kufa kwa ushindani wa ufaulu wa shule za sekondari? Mpaka sasa hatujui kwamba labda walikuwa wakitolewa kwenye ushindani walikuwa wana-*market* shule nyingine? Kwa hiyo, mbona tukienda kiulimwengu tunajua kuwa kuna *best universities?* unakuta kuna *Harvard University, Oxford University* na *university* nyingi tu kutoka nje, tena bahati nzuri sasa hivi una-*google* tu, *best universities in the world*. Wizara wanafikiri hizo *university* zinakuwa *best* bila kuwa na *best brains?* Wengine hapa wamesoma huko, lakini Watanzania tuna uwoga tunaona kwamba tukisema *best students* sijui *best schools* tunadidimiza, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema wazi hapa kwamba Serikali lazima ipewe njinga njinga na *private schools,* shule za *seminary* yaani ipewe *you know* mikiki mikiki ili na yenyewe iamke. Kwa jinsi Mungu alivyotupangia akili anatoka mtoto kwenye shule ya sekondari ya Kata anawazidi wale wa hizo *private schools.* Sasa kwa nini walitoa ile na hawakutuletea na sisi tukajadili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwamba, ushindani ni kitu kizuri. Nilisoma Kifungiro na nililelewa kujua kwamba mimi ni kiongozi, toka niko *standard four* najua mimi ni kiongozi. Nikawa

*Head Girl* na kokote nilikokaa nilichaguliwa kuwa kiongozi na leo mimi ni kiongozi wa Wabunge Wanawake hapa. Najiamini na najitambua kwa sababu mimi nilijengwa kichwani kwangu kwamba, hata kama hunikubali lakini *I know it*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hilo? kwa sababu mwanafunzi yeyote lazima ajengewe *confidence*. Sasa kwa ushindani ule ndiyo ulikuwa unafanya shule za *seminary* zituoneshe sekondari za Serikali ziendeje, unafundishwa maadili na unafundishwa mambo mengi. Sasa naomba atakaposimama Profesa Mkenda, atueleze tu ni nini kilichoondoa ule ushindani? Tusiwe waoga, hakuna nidhamu ya woga kwenye mikoa hii tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba ile hela waliyoomba wapewe yote na nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliona kwamba ni vema basi mwanafunzi akipata ajali kwenye mahusiano hususani yule wa *gender* ya (KE) na hata huyu kijana akiweza warudishwe shuleni waendelee tena kujielimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri wetu wa Elimu Profesa Adolf Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Omari Kipanga, Katibu Mkuu, Watumishi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi kubwa sana wanayoifanya kwenye Sekta yetu ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa hii Wizara kusema ukweli ni mzuri sana, tunaona kuna mambo mengi mazuri yanafanyika, kuna mageuzi makubwa ambayo wamefanya na wanasimamia vizuri sana Sekta ya Elimu kuanzia shule ya msingi,

sekondari na vyuo na taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara, kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana pia Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ambayo amekuja na mikakati mitano ambayo anataka afanikishe mambo katika Wizara hii. Kikubwa pale kwenye Bodi ya Mikopo nimeona wana programu ya kufuatilia ile mikopo ambayo wameitoa, naomba waongeze nguvu pale, Bodi ya Mikopo iongeze nguvu pesa zirudi ili wanafunzi wengi zaidi wasomeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa mikopo pia turudi nyuma tuangalie zile program ambazo zamani tulikuwa tunawapa mikopo, kama vile madaktari, watu wa sayansi na mahesabu tusiache mtu pale kwa sababu hao ndiyo watakuja kutusaidia kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wizara yetu imepata kiongozi bora sana, ni mchapa kazi, msikivu sana, mnyenyekevu, ana upendo na mshikamano wa hali juu sana kwa Wabunge wenzake, hivyo Profesa Mkenda tunampa maua yake katika majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye kuboresha viwango vya vyuo vikuu hapa nchini. Nianze kwa kusema kwamba lengo la mzazi au mlezi yeyote anapompeleka mtoto wake chuoni ni kuhakikisha kwamba anapata elimu bora, ujuzi, uzoefu na mwishoni anakuwa na mafanikio kwa kuajiriwa kwenye sekta binafsi, sekta za Serikali au kwa kuwa mjasiriamali kwa kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hili lifanyike ni vema kabisa zile taasisi zote ambazo zimepewa dhamana ya kuwapa vijana wetu elimu zikawa zimekamilika kikamilifu. Pia, takwimu tulizonazo zinaonesha kwamba taasisi zetu nyingi hasa zile za Serikali na binafsi hapa nchini, hazijakamilika na zina upungufu wa hali ya juu, sitaki kurudia *data* alizotoa jana Dkt. Oscar Kikoyo, lakini alichosema ni ukweli na alitoa mfano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutokukamilika kwa taasisi zetu hizi na kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa wahadhiri, ufundishaji, utafiti na kutoa huduma kwa jamii umeathirika kwa kiwango kikubwa. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba kuna *ranking* ambazo wenzetu kule duniani huwa wanafanya kutuangalia vyuo vyetu tukoje. Kwa hiyo, vyuo vyetu havifanyi vizuri kwenye *ranking* katika ukanda wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano hapa, katika vyuo 100 bora hapa Afrika, chuo cha kwanza bora ni *University of Cape Town,* ni cha kwanza Afrika na cha 328 duniani. Nitaruka, Chuo Kikuu cha Nairobi ambaye ni jirani yetu, ni cha saba Afrika na ni cha 855 duniani. *UNISA - University of South Africa* ambayo ni kama *Open University* ya hapa kwetu, ni cha kumi Afrika na ni cha 1,074 duniani. Jirani yetu *Makerere University* ni chuo cha 13 Afrika na 1,613 duniani. Chuo chetu pendwa kikubwa cha *University of Dar es Salaam* ni cha 37 Afrika na ni chuo cha 2,475 duniani. Chuo chetu cha *SUA* ni cha 86 Afrika na cha 4,244 duniani, Chuo cha Afya cha Muhimbili ni cha 95 na cha 4,642 duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi niliofanya hawa ni *weber metric* ndiyo wamefanya hii *evaluation* na ndiyo huwa wana *evaluate* vyuo vyetu, imeonesha kwamba katika *top ten* vyuo 10 bora Afrika, saba vimetoka Afrika Kusini na kimoja kimetoka Afrika Mashariki ambacho ni Chuo Kikuu cha Nairobi. Kwa hiyo, angalau tunaringa *East Africa* tumewakilishwa na Chuo Kikuu cha Nairobi. Kwenye vyuo 100 bora duniani, 10 vimetoka *East Africa,* (saba vimetoka Kenya na Uganda na vitatu vya kwetu ambavyo ni *UDSM*, *SUA* na *MUHAS*) viko kwenye 100 bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape angalizo kidogo ili tuelewane hapa tunapokwenda. *University of Dar es Salaam* ya kwetu ilianzishwa mwaka1961 na ilikuwa ni *Campus* ya Chuo Kikuu cha London. Mwaka 1963, *University of Dar es Salaam* wakarekebisha mambo tukawa na *University of East Africa* tukawa na vyuo vya Makerere, Dar es Salaam na Nairobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo vilikuwa vinaendeshwa pamoja na vilipokuwa vinaendeshwa pamoja vilikuwa vinafanya vizuri kwa sababu mdhibiti alikuwa mmoja na vilikuwa vinafanya vizuri. Mwaka 1971, *University of Dar es Salaam* ilianzishwa kama Chuo Kikuu kinachojitegemea na kikawa kina *campus* nyingine Morogoro na kadhalika hapa nchini. Tangu wakati huo, tangu tutoke kule hatujawahi kuwa tunafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *ranking* unaona kabisa *University of Nairobi* ni ya 10, Makerere ni ya 13; hawako mbali sana bado wanaendelea kufanya vizuri, hatuwezi kuwalaumu. Kwenye *ranking* ya vyuo vya Afrika sisi ni wa 37, mwingine ni wa themanini na ngapi na wa 95. Hapa tunaona kwamba kuna vitu vimeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, niishauri Serikali iwekeze kikamilifu kwenye uendeshaji wa vyuo vyetu vikuu, vipewe pesa ya kutosha ili wahitimu wa vyuo vyetu hivyo wanaotoka kule wawe bora na siyo bora tu wahitimu, hapana. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunatoa taswira ya wasomi wetu kwamba tuna-*produce* wasomi wa uhakika ambao watakapokwenda kwenye *labor market* mahali pengine popote watakuwa na ushindani wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tuna fursa nyingi kama walivyosema wenzangu. Tuna fursa za kupokea wanafunzi kutoka nchi ambazo haziongei Kiingereza; kwa mfano Rwanda huwa wanaleta wanafunzi huku Tanzania kusoma. Sasa Rwanda, Burundi, Mozambique na Sudan wanatuletea wanafunzi. Sasa tuboreshe ili wale jamaa wanapokuja hapa watoke na kitu siyo waone kwamba wamekuja kusoma hapa Tanzania hawajatoka na kitu. Kwa hiyo, napendekeza kabisa tuwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba tunaboresha hivi vyuo ili wasomi wetu wawe wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali. Ushauri wa kwanza; tuwe na *program* ya kuwasomesha vijana wetu kuanzia *assistant lecturers* mpaka *postdoc,* tuwe na *program* nzuri ya kuwaendeleza vijana wetu. Niishukuru sana Wizara kwamba

walitenga hela ya kutosha kusomesha wafanyakazi 189 na 207 wa *PhD* au 189 wa *masters* ambapo hapo 27 walikuwa ni wa vyuo binafsi; wamefanya vizuri. Sasa hili fungu liongezewe pesa ili tuboreshe hawa vijana tuwe na *PhD* za uhakika na wapelekwe nje wasisomeshwe hapa, tusifanye *in breeding* ya kuzalisha wataalam ambao *Degree* ya kwanza wamesoma *SUA*, ya pili *SUA* na ya tatu *SUA;* hii ni *in breeding* ya hali ya juu. Wapelekwe nje wakasome wapate uzoefu wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye zile *campus* mpya ambazo tumefungua, nitatoa mfano wa *Campus* ya Musoma ya Mwalimu Nyerere. Tuliifungua mapema hatukupeleka walimu pale sasa walichelewa sana kudahili wanafunzi kwa sababu ilikuwa hamna walimu. Ushauri wangu; Serikali isifungue *campus* mpya hadi isomeshe vijana wa kutosha na kuwapeleka kule. Ukishakuwa na *pool* ya kufundisha ndiyo tupeleke wanafunzi *otherwise* tutakuwa tunafungua *campus* unamlipa *VC,* watu wote, watumishi wote na hakuna kitu kinachoendelea. Kwa hiyo tuhakikishe kwanza tumefungua, tumesomesha vijana kabla ya…

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha. *TCU* wapambane, wahakiki ubora. Pale ambapo wanaona *program* haitolewi vizuri, basi wafungie zile *program* ambazo tunajua hazina walimu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, sekunde moja tu. Ile *publication incentive* ambayo wametoa ni kitu chema sana wamewapa watafiti 47. Naomba sasa wasimpe mtu binafsi zile pesa. Hizi hela ikiwezekana zipelekwe kwenye *account* ya chuo, mtu asiende kunywa bia na zile pesa. Zipelekwe kwenye *account* ya chuo huyu mtu azitumie hizo hela kufanya utafiti, kununua vifaa vya utafiti, kusomesha vijana wengine, kuhudhuria makongamano ili apate uzoefu wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato,

Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma wajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. Awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuangalia na kujali sana Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara ya Elimu. Kazi inayofanyika katika elimu inaonekana, inatambulika na tunaona kabisa kasi ya kuwa na wasomi waliobora katika nchi yetu hii inaonekana. Kazi tunayofanya sasa hivi kama ni nyumba tuna mwaga maji juu ya bati ili kubaini wapi kuna matundu. Kwa hiyo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajielekeza kwa vyuo vyetu vikuu. Wameongea wachangiaji wengi na jambo linapojirudiarudia linamaanisha kwamba hapo kuna changamoto; nianze na mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo Mheshimiwa Waziri ni changamoto. Mikopo hii wanafunzi wenye stahiki wengi hawapati. Mwanafunzi ana vigezo vyote, dirisha la kwanza hapati masomo yameanza anaambiwa subiri dirisha la pili. Anasubiri hana raha kisaikolojia anaathirika dirisha la pili bado anaambiwa subiri dirisha la tatu, kuna shida gani? Kama ana vigezo vyote Mheshimiwa Waziri na timu na Afisa Mikopo leo yuko hapa kuna tatizo gani wanafunzi wenye vigezo kupata mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi wanafunzi wanapata mikopo nusu. Kuna chuo kimoja jana niliongea na Mshauri, wanafunzi wawili; mmoja yeye amepata mkopo wa chakula pamoja na malazi, lakini ada hajapata, hawezi kufanya *registration* hawezi kusajiliwa. Akachukua ile hela ya chakula na ile ya malazi akapeleka kwenye ada. Sasa anakula mlo mmoja wa jioni tu. Huyu ni daktari hapati chai asubuhi wala mchana hapati chakula, anakwenda kwa huyu Mshauri akilia. Jamani

hawa wanafunzi wa vyuo vikuu ni watu wazima. Mtu mzima anakwenda ofisini analia hajapata fedha amepata nusu kuna changamoto gani tukiwapa kwa sababu huu ni mkopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwingine siku hiyohiyo ya jana yeye amepewa ada hajapata hela ya malazi, hajapata chakula. Anakwenda vilevile akilia analalamika. Sasa ataishije ameishia kubaki kwenye mikopo ambayo binafsi inatia uchungu kama uchungu wa masuala ya kausha damu. Mwanafunzi huyu atasoma nini? Anakuja kuwa daktari vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kulingana na muda niseme tu kwamba ofisi za wahadhiri. Ni kweli juhudi ni kubwa, inaonekana ofisi zinajengwa katika vyuo vikuu, nipongeze sana Wizara kwa kazi hiyo, lakini hizi ofisi mpangilio wake ni kuwa wahadhiri wawili kukaa katika ofisi moja. Wahadhiri pia ni walezi wa wanachuo na hawa wanachuo ni watu wazima, wengine wametoka makazini, wameoa na wana familia. Kuna nyakati wanahitaji kuongea na wahadhiri kuhusu labda maendeleo yao ya kimasomo au mambo yao binafsi, wanahitaji faragha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi ina wahadhiri wawili, mwanafunzi akifika akakuta wahadhiri wawili hawezi kuongea kwa sababu pengine hataki jambo lake likasikilizwa na mtu mwingine anataka amsikilize mmoja. Sasa anagonga ofisi, akigonga ofisi akiona watu wako wawili anarudi anasema samahani nimekosea kumbe hakukosea na Mhadhiri huwezi kutoka na mwanafunzi mkakaa *canteen* haiwezekani. Tuangalie hilo kuona kwamba ofisi za wahadhiri awe peke yake. Yeye mwenyewe apate faragha ya mambo yake, lakini vilevile na wanafunzi waweze kuwaona wale wanaoweza kuwapatia ushauri wa kimasomo, binafsi na mambo mengine ambayo ni mahitaji kwa wanafunzi wetu wa vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye sehemu ya malazi. Kuna uhaba mkubwa wa malazi, kwa mfano katika Chuo Kikuu cha *MUHAS* ni 30% ya wanafunzi ndiyo wana malazi wengine 60% wanajitafutia. Chuo Kikuu cha *MUHAS* kiko katikati ya jiji, wanafunzi wengi wanapata malazi sehemu mbali kwa

sababu hawawezi kulipia yale majengo yanayozunguka na hali kadhalika na vyuo vikuu vingine. Tuangalie kuwapatia hawa wanafunzi malazi japokuwa juhudi ipo, lakini hiyo juhudi iende kwa kasi angalau kutoka kwenye 30% ipande juu ili wanafunzi wetu wapate muda mzuri wa kujisomea na nafasi nzuri ya kuishi badala ya kutumia muda mwingi barabarani na kero za mitaani itawafanya kutokuzingatia masomo yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende kwenye jambo moja ambalo limekuwa ni kero, hili ni suala la mafunzo kwa vitendo. Mashirika mengine siyo yote hawawakubali wanafunzi kwenda kufanya mafunzo katika taasisi zao. Kwa nini? Hawa wanafunzi wanasoma masomo Fulani, hawa wanachuo wanataka kwenda kufanya *attachment, placement* au kufanya mafunzo kwa vitendo katika taasisi fulani, taasisi ile inawakataa sababu gani kuwakataa hawa wanafunzi? Tunaposema tukitoka pale waive, yaani wawe wabobezi watakuwaje wabobezi kama hawafanyi kwa vitendo na hawajifunzi kwa vitendo? Ushirikiano na hizi taasisi ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atoe tamko kwa taasisi angalau zote ziwakubali wanafunzi wa vyuo vikuu wanapotaka kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo na kuwasaidia ili tuweze kupata *product* bora ya hawa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la TEHAMA kuna mabadiliko sasa ya teknolojia. Badala ya ile kukaa *library* muda wote kuna kutumia maendeleo ya teknolojia. Mheshimiwa Waziri hili suala liangaliwe katika maeneo kama madarasani kuwepo na mitandao. Wanafunzi watumie madarasa yao kujisomea, kutumia TEHAMA katika maeneo ya mabweni na mazingira wanayotumia kujisomea, hebu TEHAMA au *internet* na huduma hizo ziwe zinapatikana katika vyuo vyetu vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niongelee suala la wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hawa wanafunzi wapo, tunaomba wapewe vipaumbele na mahitaji maalum yako tofauti tofauti. Miundombinu kweli jitihada ni kubwa, lakini kuna mahitaji

mengine ya binafsi ambayo huenda ni ya mtu mmoja mmoja hebu yaangaliwe. Haya yatakapogundulika, wakaletewa, yazingatiwe ili wanafunzi hawa nao waweze kupata elimu sawasawa na wengine ikiwemo mikopo 100% na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono Wizara hii na kuipongeza sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato. Nilimtaja Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Yustina Rahhi wajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake kwenye Bunge hili ambayo yamepelekea mabadiliko makubwa kwenye sera, lakini na mfumo mzima wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia zoezi hili kikamilifu. Kwa kweli naweza kusema sisi kama Wabunge tumeshiriki kwenye maeneo mbalimbali, alitupitisha pamoja na Kamati yake Maalum ambayo ilikuwa inashughulika na namna ya kuboresha mtaala. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake nzima bila kuwataja kwa sababu ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusu kuandaa mpango wa kuboresha shule za msingi. Katika nchi hii ukienda katika halmashauri zetu ukakuta namna ambavyo tumejenga shule za sekondari ukamtazama mwalimu wa sekondari, mwanafunzi wa sekondari, shule ilivyo nzuri na inavyopendeza, lakini ukatembea kilometa mbili ukaenda kwenye shule za msingi, ziko shule za msingi madarasa yako *abandoned,* ziko shule za msingi ofisi ya walimu ukiingia huwezi kutamani yule mwalimu akafanye kazi pale, imechakaa kiasi cha kutisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa nimefurahi kuona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wanakwenda kuandaa mpango. Nimwombe jambo hili, nadhani lipewe kipaumbele kikubwa, shule za msingi zimechakaa sana na shule nyingi ni za zamani sana. Huko ambako wanatoka watoto wa shule ya msingi wanaenda kusoma sekondari, shule zimechakaa sana. Unakuta kuna darasa moja jipya ambalo limejengwa pengine kwa fedha za Mheshimiwa Rais zilizokuja juzi au kwa *P4R* ndilo linagombaniwa na walimu kuwa ofisi au linagombaniwa kuwa shule za watoto wale wa awali. Madarasa mengine yote yamechakaa, hayana *floor,* hayana madirisha yamechakaa kiasi cha kutisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri jambo hili siyo tu litolewe mwongozo, nadhani kama Serikali tunahitaji kutafuta fedha hata nje ya bajeti hii kuhakikisha kwamba zoezi hili linafanyiwa kazi haraka na linakamilika. Nataka nitumie fursa hii pia kuzungumza kwenye eneo hili la utekelezaji wa mtaala mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kama nilivyosema. Naungana na wanaosema tuanze pamoja na mapungufu yaliyopo, tuanze na kuanza kutatuambia wapi tuna mapungufu gani na tuyafanyie kazi gani. Lazima tukubali kwamba tunaanza tukiwa hatujajiandaa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza tukiwa hatuna walimu wa kutosha na pengine tunaanza hata vyuo vyetu sasa hivi ambavyo bado vinazalisha walimu kwa mfumo wa zamani. Sasa lazima tukubaliane tuna *transition* hapa ambayo tunatakiwa kuifanyia kazi na tuwekeze kwa nguvu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa ushauri kwenye eneo hili. Jana kuna mzungumzaji mmoja alizungumza kidogo hapa kwamba shule nyingi Tanzania zina uhaba wa walimu. Shule nyingi za *primary*, za *secondary* sasa hivi tumejenga hazina walimu lakini tuna walimu wengi wanaomaliza vyuo vya kati na vyuo vikuu ambao wako mtaani, wako *stranded* na wamekuwa wakinyimwa au wakiomba na kukosa nafasi za kwenda kufanya

mazoezi au kujitolea. Sasa nikafikiri kwamba huu ni muda muafaka kwanza tufanye maboresho haya tuliyoyaleta ya mtaala kwenye vyuo vyote. Hawa wanaomaliza sasa hivi wote wawe tayari wana hizo taaluma mpya ambazo tunataka ziende zikafundishwe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitokee sasa hivi mwaka huu anamaliza mwanachuo ambaye atakwenda kuanza kusubiri ajira huko nje, halafu baadaye arudi tena kwenda kwenye *short course* kwenye semina kuja kufundishwa wakati bado yuko chuo. Kwa hiyo hawa walioko vyuoni wapate faida ya kukutwa na mtaala huu mpya, wafundishwe wakiwa vyuoni, waandaliwe tayari kwenda kusubiri soko linalokuja, lakini Mheshimiwa Waziri ajue hapa tumetengeneza tatizo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maelfu ya walimu huko nje ambao wanasubiri ajira lakini wataachwa nje na mabadiliko ya sera na mabadiliko ya mtaala. Nadhani mwaka jana zilipotangazwa nafasi za kazi zilikuwa 7,000 au 8,000 na walioomba ni 120,000. Maana yake huko nje ya soko wapo wahitimu walimu 200,000 ambao hawana ujuzi na mtaala mpya unaofundishwa ambao wanasubiri kuajiriwa. Pia, tuna maelfu ya walimu ambao watamaliza mwaka huu na mwakani ambao watakutwa na mtaala mpya ambao watakuwa na sifa za kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafanya nini ili hawa walioko nje wanaodaiwa na Bodi, ambao watakuwa hawana sifa ya kuajiriwa, ambao wataingia kwenye soko wajikute hawawezi kuajiriwa kwa sababu, hata mwajiri binafsi hawezi kuajiri mtu ambaye tayari Serikali imebadilisha mtaala na huo mtaala yeye hana. Nafikiri hili tunahitaji kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumaliza tatizo la sifa kwamba *okay,* ulikuwa unajitolea wapi? Tuweke utaratibu mahususi kwa mfano wapo watu wanatoka kwenye vijiji vyao na kwenye kata zao waende *straight* kwenye halmashauri zao wakajitolee kwenye hizi shule mwaka mmoja au miaka miwili baada ya hapo mfumo kama ajira zitawakuta wapate ajira kama hakuna watakuwa

tayari na hiyo sifa ya kujitolea. Kwa hiyo, hatutahangaika tena kwenda kumtafuta mwalimu ili amwandikie mtu barua ili aweze kupata sifa ya kujitolea. Hili litolewe mwongozo kati ya Wizara hii na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu, nashukuru kwamba Chuo cha *VETA* cha Geita kimeanza kufanya kazi. *Of course,* kimejengwa kwa takribani miaka sita au saba; tunashukuru sana kimeanza kufanya kazi. Kimeanza kufanya kazi kwenye aina mbili za taaluma, *electrical* na *plumbing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri anakumbuka vizuri wananchi wa Geita wao wame-*capitalise* na shughuli za madini. Shughuli za madini ndiyo biashara kubwa lakini ndiyo ajira kubwa ya vijana wa Geita. Matarajio yangu ni kuona chuo kile kinaambatanishwa na tahasusi ambayo itakwenda kushughulika na taaluma ya madini tangu kwenye utafiti ngazi ya chini, uchimbaji, uchenjuaji na kwenye kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hatapata shida kule Geita kwa sababu tunao mgodi ambao Profesa Muhongo amesema hapa, kwamba watu wanaotaka kujifunza wanaweza kujifunza masaa yoyote kwa sababu ni mgodi mkubwa na umekuwa ukitoa ushirikiano huo wa kutoa taaluma kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe, hizi kozi ambazo zimeanza, tunamshukuru tumeanza, si haba, sasa atuletee walimu na vifaa, lakini pia tufanye maandalizi ya kufanya hicho ambacho wananchi wa Geita tulikuwa tunapigia kelele kama chuo cha mkoa. Vijana wengi katika eneo lile wangetamani kupata taaluma inayoambatana na kazi asili inayozunguka eneo lile. Sisi kule hakuna mtu utamlazimisha kufanya kazi, kila mtu anafanya kazi kwa sababu wanajua umuhimu wa kazi. Kinachotakiwa ni kuwaongezea taaluma. Tuwaongezee walimu na tuwekeze kwenye chuo kile. Kile ni chuo kikubwa sana lakini hakina *fence;* na Waziri anafahamu, chuo cha Serikali hakina *fence*, walinzi wawili. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kama inawezekana tutenge bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ni kwenye eneo la mikopo. Wazungumzaji waliotangulia wamezungumza vizuri sana. Napata tabu sana na hii *means test.* Miaka yote niliyokaa hapa Bungeni kila mwaka anayestahili ndiye anayekosa. Inawezekana siyo kosa la wale waliotengeneza huo mfumo, lakini nafikiri huu mfumo hauna sifa ya kumtambua mwenye shida. Nina mfano wa watoto watatu ambapo mmoja hata kwa kuambatisha vielelezo vya mzazi wake amekatwa miguu yote; huku mama yake akiwa ni mama wa ndani; ameweka vigezo vyote kwenye mfumo lakini mfumo unamtema; na yuko chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya vyuo vyetu vyote viwe vya Serikali au viwe vya binafsi ni kama vya wafanyabiashara. Anafahamu kabisa kwamba huyu mtoto, *okay fine,* ameomba dirisha la kwanza amekosa, la pili amekosa lakini bado wanamfukuza shuleni. Nimehangaika sana na Mkurugenzi wa Bodi aliyekuwepo na wa pili aliyefuata na huyo ni mtoto mmoja. Nadhani iko sababu ya kupendekeza jambo kama tumeongeza idadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu, nimalizie. Tumeongeza wanufaika, kwa maana ya *diploma* na hivyo tumeongeza mzigo kwa Serikali. Inawezekana Waziri hatapata fedha nyingi lakini wahitaji vyuoni ni wengi. Niombe, kama mwanafunzi amepata sifa ya kuwa *enrolled* kwenye chuo tutafute mfumo mwingine ambapo aliyeomba awe na haki ya kupata *flat rate* kwanza, angalau *minimal amount, flat rate* kwa watu wote kwa kuanzia, ili nyingine mzazi wake aweze kupambana kuliko unaweka vigezo ambavyo mfumo hauwezi kuwatambua wanaohitaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine Kanyasu. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuata Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Michael Kembaki na Mheshimiwa Jumanne Kishimba wajiandae.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Elimu. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Kipanga, Katibu Mkuu Profesa Carolyne Nombo pamoja na wafanyakazi na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli wanaitendea haki Wizara ya Elimu. Wameleta mabadiliko makubwa, tunawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa bajeti kubwa ya elimu aliyoitoia ambayo ni shilingi trilioni 1.96; kwa hiyo tunampa pongezi. Natoa ushauri kuwa, ingawaje bajeti ni kubwa, naomba iendelee kuongezeka mwaka hadi mwaka kwa sababu bado haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada, naomba niongelee kuhusu mikopo ya wanufaika wa vyuo vikuu, elimu ya juu. Bajeti imekuwa ikipanda mwaka hadi mwaka. Nawapongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hata hivyo bado wanufaika ni wengi kufuatana na vigezo na nashukuru wamepandisha, kweli wengi wamepata lakini bado wanaopaswa kupata ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri na naomba hiyo bajeti, kama swali nililouliza hivi majuzi kuhusu mikopo ya vyuo vikuu; naomba iwaangalie vizuri kusudi na ambao wanastahili kupata waweze kuendelea kupata. Chukulia mtoto amesomeshwa na mama yake ambaye ni mama ntilie (Mama Lishe); ni mama anayeuza chapati au mbogamboga na ameweza kumsomesha mtoto wake kwenye *secondary schools* za *private* lakini bahati mbaya amekosa vigezo vya kupata mikopo. Naomba utafutwe mfumo ambao unaweza kuwasaidia watoto wengi ambao wanaomba mikopo ili waweze kupata mikopo na kuendelea na kutimiza ndoto zao. Maana wanapokosa mikopo wanarudi nyumbani kwao. Wengine wanakuwa tayari wamekwishakwenda vyuoni; lakini kwa sababu ameshindwa kulipia, amekosa mkopo

anarudishwa nyumbani. Hivyo ndoto yake inakuwa imeishia hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba itafutwe jinsi ya kuangalia hawa wanafunzi ambao wana ndoto ya kuwa marubani, ma-*engineer,* maprofesa na wahadhiri ili nao waweze kuendelea kupata mikopo. Naamini Mheshimiwa Waziri amenisikia na naamini alinijibu. Hata hivyo, bado naendelea kukazia hapo hapo kuwa mfumo wa jinsi ya kuwapatia mikopo hawa wanafunzi ambao ni wahitaji uangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye vyuo vikuu. Napongeza, ni kweli *campus* nyingi za vyuo vikuu zinafunguliwa lakini ziangaliwe. Kwanza, tuboreshe vyuo vikuu vilivyopo ambavyo ni vyuo vikuu mama, kikiwemo Chuo Kikuu cha *SUA*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha *UDOM* na vingine ambavyo ni vyuo mama. Tusizalishe sana *campus* nyingi, si lazima kila mkoa uwe na *campus* za vyuo vikuu, badala yake tunaweza tukaboresha hivi vyuo vikuu vilivyopo vikaweza kuwa na mikondo mbalimbali na *degree* mbalimbali ambazo zinaweza zika-*cover* wale wengine kwenye vyuo vikuu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na napongeza ukarabati unaoendelea. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Sokoine. Naipongeza Serikali kwa sababu imeweza kujenga maabara nzuri sana ya Kimataifa ambayo ipo hapo. Kwa hiyo, naamini kuwa hata vyuo vikuu vingine ukarabati na ujenzi unaendelea, lakini kama wenzangu walivyosema, kwamba *hostel* (mabweni) bado ni tatizo. Kwa hiyo hawa watoto waangaliwe. Wengine ni watoto wadogo, wametoka nyumbani kwao hawajazoea kukaa nje nje. Kwa hiyo wakijengewa mabweni itakuwa ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tafiti, naomba tafiti za vyuo vikuu nazo ziangaliwe. Wahadhiri ambao wanafanya utafiti waweze kupewa fedha za kutosha kwa sababu kwenye sayansi na teknolojia lazima uweze kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mafunzo kwa vitendo, nashukuru kwamba kuna vyuo vingine ambavyo

vinafanya mafunzo kwa vitendo hapo hapo kwenye kampasi zao; kwa mfano pale *SUA*. Namshukuru Mkuu wa Chuo cha *SUA* ameweza kuwawezesha wanafunzi wanafanya vitendo pale pale, wanalima pale pale na watoto wengine wanakuja chuoni hata jembe hawalijui; lakini angalau sasa hivi wanaweza wakafanya. Kwa hiyo mafunzo kwa vitendo *(field practicals)* yaweze kuongezewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ajira; vyuo vikuu vina maprofesa, madokta na wahadhiri. Wahadhiri wana-*retire* (wanastaafu) maprofesa wengi wamestaafu. Kwa mfano Chuo Kikuu cha *SUA* wastaafu wengi ni maprofesa. Kwa hiyo ionekane jinsi ya kuajiri wahadhiri wapya ambao wataweza kuchukua nafasi ya hawa wanaostaafu, kwa sababu wakistaafu hakuna mwingine ambaye anaweza akafundisha hayo mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa stahiki za wahadhiri na hasa maprofesa; kama alivyosema Mheshimiwa Shally, kwamba kuna maprofesa wengi wa Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)* wanadai stahiki zao baada ya kustaafu. *List* ni kubwa sana. Wameshaleta maombi yao mpaka utumishi. Naomba sana waweze kuangaliwa kwa sababu wanadai. Ni kweli kwamba mtu ukidai stahiki yako ni vizuri ukalipwa na si kudai mara kwa mara. Kwa hiyo, naomba hiyo ya kuhusu vyuo vikuu iweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa elimu ni miundombinu pamoja na walimu. Ukweli ni kwamba kuna upungufu wa walimu, hasa walimu wa sekondari. Sekondari nyingi hasa za pembezoni utakuta kuna walimu wawili na wana wanafunzi kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba. Hebu fikiria kwamba sasa la saba huendelea mpaka *form four* lakini unadhani kuwa ni nani atawafanya wafaulu vizuri? Ni vyema wapate walimu wa kutosha hasa walimu wa sayansi, Wizara itafute mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wako wengi ambao nawajua, ambao Waheshimiwa Wabunge wanawajua, ni wengi. Wamechukua mafunzo ya sayansi na wako mitaani hawajapata ajira. Wanaomba mara kwa mara, vigezo wanavyo lakini bado

hawajaajiriwa ilhali shule zetu hazina walimu wa kutosha. Muda bado, hivyo, naomba niendelee kidogo. Kwa hiyo naomba Wizara wawaajiri hao walimu ili waweze kufundisha watoto wetu; kwa kweli walimu wa sayansi wanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mafunzo ya amali, nimalizie hapo hapo. Naunga mkono kuhusu mafunzo ya amali na mtaala mpya; hasa mafunzo ya amali. Wakipata vitendea kazi na ujuzi ambao zamani ulikuwepo; kulikuwa na *needle work,* yalikuwepo mambo ya *domestic science;* hayo mafunzo ya amali yatawafanya wanafunzi hawa waweze kujiajiri wenyewe na hivyo kupunguza matatizo ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hayo machache niliyochangia na Mwenyezi Mungu akubariki na aibariki Wizara ya Elimu, fedha ziongezeke na bajeti iweze kuongezeka na waweze kuwapatia walimu, wahadhiri waweze kupata stahiki zao na madai yao kwa sababu wamedai kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Nilimtaja Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mheshimiwa Michael Kembaki na Mheshimiwa Jumanne Kishimbwa wajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na kwa kuielekeza Wizara ya Elimu ili iweze kurejea na kuweza kuleta mfumo mzuri wa mitaala ambayo itakuja kuwasaidia vijana wa Tanzania kuweza kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa sana kwa vijana. Wanashindwa kwenda kuyakabili maisha kwa sababu ya kukosa ujuzi, maarifa na elimu. Ukianglia kwanza demografia ya Tanzania ya idadi ya watu utaona kwamba imekaa kama *pyramid*. Kwa maana hiyo vijana wengi wa Tanzania au idadi kubwa ya Watanzania ni tegemezi. Kwa nini tegemezi? Nguvu kazi ya vijana wa Tanzania miaka 15 mpaka 40 zaidi ya 50% ni wategemezi kwa sababu hawajaandaliwa kwenda kujiajiri wenyewe kwa sababu ya kukosa ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kuna wimbi kubwa sana sasa hivi la Watanzania wenzangu kwenda kuwapeleka pengine watoto shule hizi za *english medium* na *international schools* ambapo ukiangalia vijana hao wanaandaliwa kwenda kuwa watawala lakini pengine kwenye *white colour jobs* ambazo kiukweli hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba kwa Tanzania karibu kila mwaka kuna watu takriban 800,000 hivi ambao wameshahitimu na wanatakiwa waingie kwenye ajira. Kwa hiyo kwa hili nampongeza Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na namshukuru sana kwa kuja na wazo hili, kwamba sasa tuweke mtaala mzuri. Kwa upande wa amali tuna hakika kabisa kwamba wanafunzi wakifikia sehemu fulani wanaweza kujiajiri wenyewe, watakuwa na ujuzi wa kutosha na wanaweza kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli tumeona jitihada nyingi sana za Wizara na mwelekeo ni mzuri kwenye jitihada hizo, kwamba tunaweza kwenda na mifumo hiyo ya mkondo wa amali, lakini bado tutaendelea na mkondo mwingine wa taaluma; na jitihada zao wamezieleza kwenye bajeti. Wana mpango wa kujenga miundombinu kwenye shule 100 za sekondari kuanzia mwakani na 26 zitaanza kudahili. Kuna vyuo 65 vinakwenda kuanzishwa. Kuna wanaoendelea kusajili hizi *vocational training schools;* wanaendelea kusajili *technical schools* hizi ili kwamba angalau mwakani basi wachukue idadi kubwa ya wanafunzi wajaribu kwenda na hiyo mikondo miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna nia thabiti kweli kwamba hizi sasa ndizo *solution* kwa ajili ya Taifa letu na vijana wetu, hatuna budi kukubaliana kwamba Wizara hii ipewe fedha nyingi za kwenda kuwekeza huko. Tumeona kweli, hata mwaka jana nilisema, kwamba bajeti kubwa ya *development* ya Wizara ya Elimu kila mtu amesema 60.3% inakwenda kwenye mikopo. Ni jambo jema, lakini nashauri tu kabisa, kwamba huko kwenye mikopo sijui kwa nini inaitwa *development;* kwa sababu tunaweza tukafikiria Wizara ina fedha nyingi. Tumeona bajeti yao ya *1.9 trillion shillings* tukafikiri zote ndiyo zinakwenda sasa kwenye miamala na kwenda kuboresha elimu; kumbe nyingi zinakwenda huko kwenye mikopo ambayo kwa vyovyote vile ingekuwa ni *revolving fund;* kwa sababu inakopwa na kurejeshwa, au ingekuwa kwenye *capacity building* kiasi kwamba kama haitarudi kwenye marejesho, basi iwasaidie Watanzania kwenye *capacity building.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tunaona kwamba fedha zinazokwenda sasa kwenye kuboresha elimu na miundombinu ya kwenda kupambana kuwezesha hii mikondo ya amali itakuwa ni kidogo. Kwa sababu hiyo sasa, hofu yangu ni kwamba kwa huu utaratibu *coverage* itachukua hata zaidi ya miaka 10 ili kuona kwamba sasa Tanzania nzima tume-*stable* kwenye mikondo miwili kwa sababu sasa tunakwenda taratibu kutokana na bajeti. Hili lazima kama Taifa tulione.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage mwaka jana alisema kwamba tunawafanyia majaribio watoto wa Tanzania. Mimi pia nasema, kweli kwenye hili tuwe makini; kwa sababu naona tu kwamba, tunawaweka wanafunzi waingie mikataba ya maisha na hii mikondo. Hivi ukimchukua mtoto wa miaka sita ukamweka kwenye mkondo wa amali ambao atakwenda nao na elimu ya lazima ni mpaka *form four.* Miaka kumi amesoma amali akitoka hapo kwenda chuo au kwenda *form five* bado anaendelea na mkondo wa amali mpaka chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano hapa katikati pengine hatukumjengea mazingira mazuri, amesoma kwenye sehemu ambayo hapakuwa na karakana nzuri ya kumfundisha

na hapakuwa na walimu wazuri; hivi kum-*correct* huyu mtoto unafanyaje? Anakwenda kuanza darasa la kwanza au anakwenda kuanza *form one*? Kwamba sasa pengine upande huu amefeli, hakufanya vizuri sasa aanze kusoma upande wa taaluma. Hiki kitu lazima tuwe makini sana, vinginevyo wazazi na walimu waelimishwe kuhusu namna ya kuwachagua hawa Watoto, kwamba ni nani anatakiwa kwenda upande wa amali na nani anatakiwa kwenda upande wa taaluma; vinginevyo *commitment* ya Serikali iwe kubwa sana, ama sivyo tunakwenda kuzima ndoto za hawa watoto. Watafika mahali watakuwa *useless* mitaani. Kwa hiyo hili lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kwa sababu hiyo basi maandalizi ya walimu na karakana ni muhimu sana. Mtoto asije akaenda tu kufundishwa habari ya *automobile engineering* akaenda labda kwenye mambo ya *carpentry* au usanii na hana namna ya kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwanzo ni mgumu, kuna karakana za mitaani zina mafundi, *local artisans,* mafundi uashi wazuri sana. Serikali labda ingeanza basi kwenye karakana zetu na iwaajiri wale wa mitaani wanao-*perform* vizuri. Kuna fundi wa mtaani akikufungia injini ya gari wala huwezi kuona shida na hajasoma hata kidogo. Tena wako vizuri kuliko hawa wakwetu wanaosoma *vocational training* na wengine. Kwa hiyo basi, Serikali ianze nao wale waliobobea. Kuna mafundi cherehani wa mitaani wanaoweza ku-*design* vizuri, wachukuliwe na kama tayari tutakuwa tumeshajenga karakana na miundombinu ya kutosha, waanze kuwafundisha vijana wetu. Kwa hiyo, kwenye hilo la amali naliunga mkono, naona linaweza kuwa ni muarobaini kwa watoto wetu, wakimaliza kusoma wajue tu kwamba kuna kujiajiri. Kwa sababu hiyo, Serikali iangalie na iwezekeze fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine unaenda kwa walimu, kuna changamoto za aina mbili kwa walimu; kwanza, kuna upungufu mkubwa wa walimu, lakini kuna ubora, umahiri na ubobezi kwa walimu. *Indicator* ya kuona kwamba tunafanyaje ni *performance* ya wanafunzi, jana

ameeleza Mheshimiwa Getere hapo, alikuwa anaangalia *skillness* ya wanafunzi wanaoishia pengine *Division Four* na *Division Zero*, ile ni *image* na *indicator* ya walimu wanaowafundisha wanafunzi. Kama walimu hawata-*perform* vizuri tusitegemee kwamba wanafunzi wetu watafanya vizuri na wataenda ku-*compete* kwenye soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wanafunzi wengi wanaofeli ni wanaochukua masomo ya sayansi na ndiyo maana wanakwepa. Yaani, mwanafunzi anaona kuliko umpeleke darasa la *Physics*, *Chemistry*, Hesabu akaenda kupata sifuri ni afadhali aende kwenye upande wa *arts* pengine Historia na Jiografia ambayo anaweza akajisomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kwenye dunia inayoenda kwenye sayansi na teknolojia, lazima tuwe na walimu wa sayansi, kwa sababu kuna *gap* kubwa ya walimu wa sayansi, tuwekeze kwenye ualimu, tuajiri walimu wa kutosha kwenye sayansi. Kwa sababu sasa tumeenda kwenye mtaala mpya, tuhakikishe kwamba tuna walimu wa kutosha wanaoenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna kusajili walimu kwenye bodi ya taaluma ya ualimu, hili jambo ni jema sana, walimu watambuliwe na waone *training needs*, waone *gap* za walimu ziko wapi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:**…ili siku hizi *TRC* ambazo tumezijenga walimu wafundishwe mara kwa mara, *training* na nini, kuwakumbushia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile udhibiti na ubora wa elimu…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi, naona huweki *full stop*, ahsante sana. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Michael Kembaki, Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Japhet Hasunga, naomba wajiandae.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika elimu ambayo ndiyo msingi wa ukuaji wa uchumi katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amefanya kazi kubwa katika Jimbo letu la Tarime Mjini na ametuwezesha kupata zaidi ya shule nne katika Jimbo letu la Tarime Mjini ambazo ni; Shule ya Sekondari Nyakisese, iliyoko Nyandoto; Ikohi sekondari iliyoko Turwa; Regicheri iliyoko Nkende. Ameboresha sana Shule ya Sekondari ya Tarime. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanatarime naomba nichukue nafasi hii kuelezea umuhimu wa elimu katika Taifa letu la Tanzania. Elimu ni zaidi ya kusoma, kuandika na kuhesabu, elimu ni muhimu katika nyanja zote katika maisha ya binadamu, elimu ni mojawapo ya uwekezaji mkubwa ambao Serikali inaweza kuwekeza kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi unakua, elimu husaidia watu kufanya kazi vizuri na unaweza kuunda fursa za ukuaji endelevu wa uchumi wao wenyewe pamoja na watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, elimu imeonekana kuwapa watu ujuzi muhimu na zana za kuwasaidia kujikimu wao wenyewe katika maisha yao. Utafiti uliofanyika umeonyesha kwamba nchi za Australia, Marekani na Japan ni mojawapo ya nchi ambazo zina elimu nzuri sana na watu walioelimika. Watu binafsi, mtu mmoja mmoja, katika nchi hizo wanaishi juu ya mstari wa umaskini. Kwa takwimu hizo tunaweza kujifunza kwamba elimu ni sehemu ya ukuaji au ustawi wa uchumi katika nchi yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ikoje katika nchi yetu ya Tanzania? Yametokea mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara ambayo yamesababisha ukosefu wa utulivu wa mitaala katika Taifa letu la Tanzania na hivyo kusababisha elimu inayotolewa katika nchi yetu isikidhi mahitaji yanayohitajika katika kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika miaka ya 90, mtaala ulibadilika ambapo toka wakati huo elimu yetu imekuwa siyo nzuri sana. Haiwajengi wahitimu kujiajiri wenyewe au kujisimamia wenyewe, wamekuwa ni watu wa kutegemea kuajiriwa peke yake. Mwaka 2004 yalifanyika mabadiliko ya mtaala, miaka ya 2010 pia yalifanyika mabadiliko ya mitaala, tena mwaka huu 2024 yamefanyika mabadiliko ya mitaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme, tayari mtaala mpya umeanza kufanya kazi na umeanza kazi Januari, lakini hakuna maandalizi yanayowezesha walimu kufundisha mtaala mpya. Wadhibiti ubora wanapita mashuleni kuhimiza walimu wafundishe mitaala mipya lakini hakuna maandalizi ya kutosha. Walimu hawa hawaujui huu mtaala mpya ni nini, hawaelewi mtaala mpya unafanyaje kazi kwa sababu waliopewa semina ni wachache kulingana na idadi ya walimu waliopo katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, mwanafunzi ambaye anafundishwa na mwalimu ambaye hajui kile anachokifundisha, tunatengeneza watoto wetu wawe wa aina gani? Hivi nikienda kufundisha mtu arushe ndege na mimi sijui kurusha ndege si unategemea ajali? Kwa hivyo, hii tunatengeneza ajali ya kielimu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu zaidi vitabu ambavyo walimu wanategemea kufundishia havipo katika shule zetu, maana yake nini? Mwalimu atoe vitu kichwani afundishe huu mtaala mpya ambayo ni hatari sana katika kuelimisha watoto wetu ambao wanasoma katika shule zetu. Sisi wote hapa watoto wetu wanasoma katika shule zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanategemea kwamba mtoto anapokwenda shuleni aweze kuwa mtu ambaye amepata ujuzi wa kujiendesha baadaye akiwa mtu mzima. Kwa miezi sita sasa toke Januari, mpaka leo mtaala mpya unafundishwa. Jana, katika jimbo langu ndiyo nilisikia walimu wakuu wanaenda kufundishwa juu ya mtaala mpya. Walimu wakuu hawa ndiyo wasimamizi wa mtaala mpya, sasa walikuwa wanasimamia nini katika shule zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hapa kuna mchezo ambao siyo mzuri, kulikuwa na dharura gani na haraka gani ya kupeleka mtaala huu uanze kabla ya maandalizi ya kutosha katika shule zetu ili watoto wetu wanapofundishwa waelewe kile wanachofundishwa. Mchezo huo ambao ulifanyika miaka ya 90 ndiyo unafanyika tena mwaka 2024, kweli? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge tuliangalie hili na watoto wetu wanafundishwa huko huko, wanafundishwa kitu gani kwa miezi hii sita ambayo wamefundishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu vya mtaala mpya viko kwenye *softcopy*, hivi mshahara wa mwalimu ambao analipwa shilingi laki tatu, laki nne pamoja na mikopo hii ambayo tunasema hapa ya kichefuchefu, mwalimu atatoa wapi hela aweke kifurushi aweze ku-*download* kitabu aweze kufundisha? Mheshimiwa Waziri hii si sawa na hii ni kurudisha nyuma elimu yetu, haikubaliki kabisa kwamba mwalimu atumie fedha yake ku-*download* kitabu na siyo kwamba hawezi kuki-*print* kile kitabu, unasomea pale pale. Hii kwa kweli naona kwamba udharura huu uliofanyika haukuzingatia hali halisi ya nchi yetu na namna tunavyohitaji elimu iwe katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuhusu upatikanaji wa vitabu katika Taifa letu, ukienda katika *bookshops* unatafuta kitabu kwa kweli vitabu havipatikani. Siyo sasa hivi, hata wakati uliopita bado vitabu havitoshelezi kwenye *bookshops*, pia, hata mchanganyiko uliopo unachanganya, Serikali inahimiza tutumie

vitabu vya *TIE* na *TIE* ukiangalia vitabu vyao viko *very shallow*, haviendi *deep* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kiti chako kitoe maelekezo kwa Wizara iruhusu sasa vitabu…

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Kembaki kuna taarifa, taarifa inatokea wapi?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Hapa.

**MWENYEKITI:** *Okay*, Mheshimiwa Dkt. Thea.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika, napenda kumpa taarifa msemaji, vitabu vinavyotungwa, vinavyotengenezwa pale *TIE* vinatengenezwa na wataalam, wasomi wa kila somo. Kwa hiyo, vile vitabu haviko *shallow* kabisa, vitabu vinatengenezwa au vinaandikwa na walimu ambao ni wabobezi. Wataalam wote wanavipitia, kwa hiyo, vitabu vyetu vya *TIE* haviko *shallow* kama anavyosema msemaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kembaki unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa kwa sababu mlaji ndiyo anajua kama chakula ni kitamu au siyo kitamu. Kwa hivyo, kama yeye ni sehemu naomba niseme sijapokea taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni langu ni hili, kwamba nchi yetu iruhusu wazalishaji wengine wa vitabu waweze kuingia sokoni washindane kwa ubora. Kusiwe na *limitation* ya kitabu, kama

kitumike kitabu kimoja, hapana, kuwepo na uhuru kama zilivyo sekta nyingine ili vitabu vipatikane kwa wingi, walimu waweze kuwa na machaguo kadha wa kadha kwa ajili ya kuongeza uelewa wa ufundishaji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Michael Kembaki. Nilimtaja Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Japhet Hasunga, ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naungana na Wabunge wenzangu, kuipongeza Wizara hii ya elimu ya juu. Pia, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa suala zima la maboresho ya elimu pamoja na Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge kazi yetu ni kuangalia maeneo ambayo bado yana matatizo mengi sana. Suala hili la elimu naona kila anayeamka anaendelea kulizunguka sana. Naweza kuungana na mchangiaji aliyemaliza, Mbunge wa Tarime, hapa tunayemkwepa ni mtu wa muhimu sana, huyu anayetutayarishia kitabu watoto wetu wakasome huwa anapatikanaje na ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa suala kwamba amesoma, ana kitu gani kingine cha umaarufu alichonacho ili tumpe huyu akatuzalishie kitabu watoto wetu wajifunze? Kwa nini nasema hivyo? Nimepitia vitabu viwili vitatu vya shule za msingi, kipengele kimoja tu ambacho kimeniuma sana, lakini ukikiangalia kipengele hicho ndicho hata Wizara inachofanya. Mwalimu kwenye maelezo yake anaeleza kwamba mwanafunzi ukiwa unasoma, ameandika vizuri sana, ukimaliza shule acha kujenga nyumba yako hii ya wazazi wako ya tope na nyasi, utajenga nyumba ya bati nzuri ya *block*, siyo vizuri kuwa na ng'ombe uza ng'ombe jenga nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, huyu mtoto mimi nakaa naye, tunakaa nyumba ya nyasi, nyumba ya tope, tumejenga na tunao

hao ng'ombe, wewe unaanza mwanzoni kumfundisha mwanangu kwamba hii nyumba yangu siyo sahihi na ni vizuri tuuze mifugo ili tujenge nyumba, *automatically*, mgogoro unaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tupo makabila 125, hatuwezi kuishi haya maisha wanayoyasema humu ndani ya Ulaya, nani ataweza kwenda kuishi maisha ya kizungu? Haiwezekani! Mwanafunzi aelezwe maisha ya wazazi wake, kwamba hii nyumba ya nyasi na tope na ng'ombe mlizonazo nyumbani ni mali halali; ni sahihi; ni nyumba sawasawa kabisa na nyumba nyingine, kwa sababu hata kama tutabisha, nyumba za nyasi au nyumba za tope tukasema hazifai, hizo nyumba za watalii kule *National Park* si za nyasi? Si wanalipa shilingi milioni moja kwa siku? Unamwambiaje mtoto wangu kwamba ni haramu hizo nyumba na unataka sisi tuuze ng'ombe tukajenge nyumba, inawezekana kweli? Mimi niuze ng'ombe nikajenge nyumba, usingizi unaletwa na nyumba? Inawezekana kweli? Mimi usingizi wangu na maisha yangu yanapatikana kwa ajili ya ng'ombe siyo kwa ajili ya nyumba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu tu kulipima na kuliona kwamba, inawezekana tunazunguka kote, tatizo kubwa liko hapa. Huyu anayeandika vitabu lazima awe mtu ambaye anayajua maisha ya Watanzania ili mimi mtu wa Kahama ninaposoma kile kitabu nikiwa mdogo niyaheshimu maisha ya nyumbani; kwamba haya maisha hata nikishindwa kumbe naweza kuishi, kuliko sasa hivi inavyoonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda kwenye maonyesho ya Mheshimiwa Waziri ya watoto wenye vipaji. Kilichonishangaza, Mheshimiwa Waziri bahati nzuri alikuwepo, kila unapokwenda lile banda la watoto wenye vipaji, unakuta ametengeneza redio hajakamilisha, katengeneza mita ya maji anahitaji msaada, haijafanya kazi. Sasa Mheshimiwa Waziri ina maana kipaji cha binadamu, kwa nini kusiwe na kipaji cha kulima? Kipaji cha kukamua maziwa, wenyewe hawaruhusiwi? Kipaji cha kuchunga hakiruhusiwi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Waziri kwenye kipaji cha kulima kama mtu ana kipaji cha kulima akalima heka moja kwa siku moja si ni shilingi laki moja? Siyo kipaji? Shilingi laki moja maana yake kwa mwezi si shilingi milioni tatu? Je, ni sahihi kuwafundisha judo, sarakasi, mabaunsa, mwisho wa yote watakuwa nani sasa? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tunaongea hapa kwamba je, tunatarajia kuwa wazungu? Yaani inawezekana Tanzania nzima watu milioni 70 tutakuja kuwa wazungu na tuishi kabisa kweli yaani tuondokane kabisa iwezekane? Ingawa pamoja na yote nimefuatana na Waheshimiwa maprofesa kwenye michango lakini sioni kwa nini hatutaki kabisa yale maisha *original*? Hatuwezi kuwa na elimu ya Kiafrika na yenyewe ikafundishwa darasani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna somo la kutafuta pesa na kutunza pesa, kwa nini kwenye mitaala ya elimu halimo? Mheshimiwa Waziri wote hapa wanaeleza kwamba nataka mwanangu asome akawe daktari, akawe nani ili afanye nini? Si apokee mshahara? Sasa kwa nini tunakataa somo la kutafuta pesa? Lifundishwe kutoka darasa la kwanza. Mheshimiwa Waziri litakuwa kosa gani na madhara yake yatakuwa nini? Yaani kutafuta pesa na kutunza pesa madhara yake yatakuwa nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana wenzetu wa mitaala lazima wakubaliane kwamba suala la pesa liongelewe wazi kwa sababu ndiyo suala la mwisho. Kote huko kusoma, kufanya nini, mwisho wa yote tunaenda kuangukia kwenye fedha, sasa kama hatutaki hela tufanyeje? Profesa Muhongo ameongea vizuri sana, lakini je, tutafanya nini bila hela? Huyu mtu ana ng'ombe kumi anaweza akasoma mpaka Ujerumani, anafanyaje sasa hebu watuambie. Je, wote wataondoka kweli Watanzania wote wataondoka huko vijijini? Haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, najaribu tu kumweleza Mheshimiwa Waziri afikirie kwa mapana sana. Leo hapa biashara

inayoongoza na bahati nzuri yeye ni mwenyeji wa Moshi, biashara inayoongoza Tanzania nzima ya kwanza ni ya maduka. Je, tunao mtaala wa maduka kwenye vyuo vyetu na kwenye *VETA*? Mnataka tuwe na mabilionea, haya, bilionea anatokea wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maduka yote yaliyopo hapa Dodoma waliyolipia ni hawa wafanyakazi wa Serikali. Wamelipia kodi shilingi milioni moja, si wameyaweka nguo hapo, wamelipa shilingi milioni moja, wanataka nini? Si biashara ya maduka? Sasa biashara ya maduka wanakaataje isiende kwenye mitaala ya shule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu watu wote huanzia kwenye magenge wakaenda kwenye maduka, kwenye maduka ndiyo wakaenda kwenye viwanda. Akishakuwa anakiuza kitu ndiyo anajua kumbe hiki ninachokiuza naweza kukitengeneza, kinatengenezwaje? Ndiyo anaanza kufikiria. Sasa huku kwingine tunazungukaje kwenye sehemu ambazo ni za msingi. Nataka tu nilieleze ili kusudi kulitolea mwanga zaidi maana yake naona bado linaendelea kutusumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea hapa suala la matatizo ya sekondari na *university*, mimi sina tatizo, lakini labda nimuulize Mheshimiwa Waziri, mimi mtoto wangu anatakiwa kupata *degree* kwa miaka minne, ameishia miaka miwili, mimi nimekosa hela ameshindwa amerudi, huyu tunamwitaje? Kwa nini asipewe nusu *degree,* wamwandikie nusu *degree* kwa sababu anayeamua *degree* siyo Waziri, anayeamua *degree* ni mwajiri. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha.

**TAARIFA**

**MHE. *ENG.* MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Kishimba kwamba, katika *Competence Based Education Type*, mwanafunzi anaposoma akishindwa kufika mwisho, pale katikati anapewa ile *NTA Level 7*. Inakuwa siyo *degree* kamili, bali hapa nyuma kuna cheti ambacho anapewa kabla hajakamilisha ile *degree* yake. Hiyo iko hapahapa Tanzania, ukienda *DIT* wanatoa *competence based*, unasoma unapewa kitu kinaitwa *Higher National Diploma* ambayo una…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer*, natamani Mheshimiwa Kishimba akuelewe unachokisema. Mheshimiwa Kishimba unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kwa sababu, huyu mwajiri siyo Mheshimiwa *Eng.* Ulenge, ni mtu wa Kariakoo. Unamwambia mimi nilikuwa nasoma miaka minne, nikakosa hela nikaishia miwili, anakuulizaje? Hayo maneno ya *competence* hayajui, anakwambia unayo nusu *degree*, si ndiyo? Wewe niandikie mimi hayo maneno yote yalete, hapa chini andika nusu *degree,* ili tajiri ndiyo atoe maamuzi. Maana haya mengine yote mnayoongea ni utapeli, eleza kabisa kwamba, mimi nina nusu *degree*. Najaribu kueleza kitu ambacho kiko kwenye *field* ya maisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu nimalizie. Mheshimiwa Waziri, kulikuwa na suala hili zuri sana la watoto kula shuleni. Sasa hivi limetuletea mgogoro sana kati ya sisi na walimu, linatuchonganisha. Tunaomba Wizara itoe tamko kwamba, kiwango cha chakula ambacho wazazi wanatakiwa kuchangia pale shuleni kiwe ni chakula gani na kwa kiasi gani? Kwa sababu, sasa hivi unaambiwa mtu alete kilo nne za mchele kwa mwezi na kilo tatu za maharage, lakini ni shule gani inayokataa mchicha? Hawataki mchicha wala matembele, itawezekana namna gani? Si ndiyo? Sasa maharage ni shilingi 4,000 si ndiyo? Shilingi 12,000, wewe una watoto sita, utaweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuandikieni hapahapa, Serikali itoe waraka kwamba, chakula kinachotakiwa ni hiki. Kama tajiri ana hela zaidi, yeye hahusiani na tatizo hata nyama atatoa ili hawa maskini tuwatendee haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kishimba. Namtaja Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Nusrat Hanje wajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Jambo la kwanza, natumia nafasi hii kuipongeza sana Serikali pamoja na Wizara kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya. Pia, natumia nafasi hii kuzipongeza taasisi na vyuo vilivyo chini ya Wizara kwa kazi nzuri ambazo vinafanya, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Wizara imekuja nalo, la mabadiliko ya mitaala, ni katika kutekeleza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu, suala la elimu ni suala la Kikatiba. Ukichukua Ibara ya 11(1) inazungumza kwamba, kila Mtanzania, kila mtu ana haki ya kufanya kazi na kila mtu ana haki ya kujipatia elimu. Ibara Ndogo ya (2) inasema, "*Kila mtu anayo haki ya kujielimisha na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayopenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, elimu ni suala la Kikatiba ndiyo maana hata tulipotayarisha Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2000 – 2025, katika malengo matano tuliyoyaweka, mojawapo ya lengo ilikuwa ni kuwepo kwa jamii iliyoelimika vyema na inayoendelea kujifunza. Ipo kwenye Dira ya Nchi yetu, lakini kama hiyo haitoshi, mwaka 1961 wakati tulipopata uhuru, Baba wa Taifa alitambua na alitangaza kwamba, wapo maadui watatu wa nchi yetu, maadui hao ni ujinga, umaskini na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yote tangu tumetoka huko mpaka leo na hawa maadui watatu bado wanaendelea kutusumbua katika Taifa letu. Ndiyo maana hata viongozi mbalimbali, wadau wa elimu na wadau wa Maendeleo wa Afrika walipokutana Kampala, Uganda mwaka 1991, walikuja na kitu kinaitwa *"The Kampala Document"* ambayo walikubaliana maazimio kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo waliyokubaliana ni umuhimu wa elimu kwa Vijana wa Afrika. Wakasema, Vijana wa Kiafrika wafundishwe juu ya elimu, juu ya Maadili ya Kiafrika, juu ya Utamaduni wa Kiafrika na wajifunze teknolojia itakayolisaidia Bara la Afrika katika kuleta maendeleo. Kwa hiyo, utaona haya yote ni masuala ambayo tumeanzia kwenye Katiba, tumekuja kwenye Dira na tumekuja kwenye Sera, yote yanazungumzia elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na pia, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuja na mabadiliko makubwa kwenye Sera ya Elimu. Hayo wanayotekeleza ni Katiba na ukiangalia Mheshimiwa Rais amekuja na mabadiliko makubwa, lakini pia ameongeza rasilimali fedha kwenye Wizara na kwenye taasisi, tunampa hongera sana. Sasa, tulikotoka kumetufikisha hapa tulipofika, hali ikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023, *FinScope* wamefanya utafiti. Walipofanya utafiti wamekuja na matokeo ambayo yanatuambia hivi, kwa mwaka 2023 Watanzania ambao wana umri wa miaka 16 na kwenda juu, ambao wana elimu ya kuanzia *tertiary* na kupanda juu, ni asilimia tano tu ya Watanzania wote, lakini 26% ya Watanzania ni wale ambao wana elimu ya sekondari. Hii ndiyo elimu ambayo wameifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizo zinatuambia, Watanzania ambao wamefikia kwenye elimu ya msingi tu peke yake mpaka sasa hivi ni 56%, lakini kuna Watanzania ambao hawana elimu kabisa, hao sasa hivi wamekuwa ni 13%. Hizi takwimu na huu utafiti unatupeleka wapi? Ukiangalia haya matokeo yanatupeleka mwaka 2023 ambapo Watanzania

wenye uwezo wa kuongea na kuandika Kiswahili ni 79% tu, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kama ni 79%, hao wengine hawana uwezo wa kusoma wala hawana uwezo wa kuandika Kiswahili. Ukienda kwenye lugha ya Kiingereza, utafiti unaonesha Watanzania wenye uwezo wa kuongea na kuandika Kiingereza vizuri ni 30%, lakini Watanzania 61% na kuendelea, hawana uwezo wa kusoma wala kuandika Kiingereza. Sasa, hii inatupelekea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunahitaji kufanya mabadiliko makubwa kwenye elimu yetu ili kuwaandaa Watanzania na hili ndiyo Wizara inakuja nalo na ndilo linalofanya kazi na ndiyo maana tunawapongeza, lakini ili tuweze kufanikiwa kwenye mabadiliko tunahitaji walimu ambao ni mahiri, tunahitaji wahadhiri ambao ni mahiri, ambao ni *competent,* watakaoweza kutupeleka huko tunakotaka. Ili tufikie hayo ni lazima maslahi ya walimu yaangaliwe na motisha iwepo. Mwalimu hawezi kuwa anasononeka halafu ukategemea kwamba, atatoa maarifa mazuri kwa Watanzania. Kwa hiyo, maslahi yao yaangaliwe na utaratibu wao uangaliwe vizuri, hii itawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni utafiti kwenye vyuo vikuu na ushauri wa kitaalam ni muhimu mno katika maendeleo ya nchi yetu. Tunahitaji watafiti waisaidie nchi, sasa tunahitaji uwekezaji wa kutosha katika eneo hilo ili tuweze kufikia hapo, lakini zaidi ya hapo, tumesema na watu wamechangia kuanzia jana, taasisi inayosimamia ubora wa elimu ya shule za msingi na sekondari tunafikiri sasa umefika wakati iwe ni taasisi au awe wakala anayejitegemea, ili aweze kusimamia ubora ule unaotakiwa. Hili ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo kwa sababu, elimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi ndiyo maana kule Mbozi, Vwawa, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri anatujengea Chuo cha *VETA*, lakini bado hakijakamilika. Tunamwomba aongeze kasi, ili kile chuo kikamilike, tupate wataalam, tupate vijana ambao watakuwa wamesomea aina mbalimbali za ufundi.

Pia, tunahitaji tawi la chuo kikuu angalau kimoja, Mkoa wa Songwe hauna tawi hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale tuko mpakani, tunataka Wazambia, Wamalawi, Wazimbabwe na watu wengine waje kusoma Tanzania watatuletea fedha za kigeni. Kwa hiyo, tunahitaji kujenga matawi na kuwatengeneza walimu wetu watoe elimu iliyo bora ili tuvute watu wa nje, tupate fedha nyingi, hii itatusaidia sana Mheshimiwa Waziri. Sasa katika hali hii tuliyonayo, tunapohitaji walimu wenye maadili, walimu ambao wamesomeshwa, pia, tunahitaji wapate elimu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukasoma mwaka 1980 ukaendelea kufundisha ukasema inatosha, ni lazima uendelee kujifunza kama Katiba inavyosema. Kwa hiyo, wawe na programu za kuwaendeleza walimu, si tu wa vyuo bali hata walimu wa shule za msingi na sekondari. Iwe kila mwaka, kila mwalimu akafundishwe, apate semina kidogo, angalau anazaliwa upya, anakuwa na uwezo wa ku-*deliver* na kuweza kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tunahitaji vifaa vya kisasa vya kufundishia ili haya mabadiliko ya taaluma yatuwezeshe kuwaandaa Watanzania, tuondokane na hizi takwimu ambazo zinaonesha Watanzania wengi bado hatuna uwezo. Nchi inahitaji wataalam, tunahitaji watu wenye fani mbalimbali, wanahitaji kujielimisha, wakomae, wawe mahiri, wawe ni *competent* katika maeneo yote kwa kuwa na elimu, kwa kuwa na maarifa na kwa kuwa na ujuzi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Nusrat Hanje ajiandae na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula atamalizia.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha elimu kwa Watanzania. Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu Mheshimiwa Profesa Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Kipanga pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. Pia, natumia fursa hii kuwapongeza walimu wote wa shule za msingi, shule za sekondari, shule za awali pamoja na wa vyuo vikuu nchini Tanzania, wanafanya kazi kubwa sana ya kuwaelimisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nakwenda kuchangia kadiri ya wasilisho la Mheshimiwa Waziri. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali kwa kuja na mtaala mpya. Mtaala mpya ni mzuri na wazo ni zuri, lakini una mapungufu. Mapungufu hayo napenda kuyataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala tumeupokea, lakini katika upokeaji wa mtaala, hatukuwa tumejiandaa. Kwa nini nasema hatukuwa tumejiandaa? Nasema hivi kwa sababu, walimu wanaokwenda kufundisha ule mtaala, hawajaandaliwa. Wizara ya Elimu inasema imeandaa walimu, lakini walimu iliowaandaa ni imechukua walimu wawili kutoka kwenye shule; nafanya kama *sampling*, kwa mfano, Shule ya Nsemulwa, Mpanda, wamechukua walimu wawili wakaenda kufundishwa, lakini zipo shule nyingi ambazo wamechukuliwa walimu wawili wamefundishwa ili na wao wakawafundishe walimu wenzao. Nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walimu wawili waliochukuliwa kwenda kufundisha walimu wenzao, ina maana kama hawajaelewa kile kitu, basi na wao watakwenda kukifundisha vilevile. Hilo naona ni pungufu. Ni nini ushauri wangu? Ushauri wangu ni kwamba, ni kwa nini wasifundishe wakufunzi, wakawaita *let say* wakaenda pale Wilaya ya Mpanda, wakawaita walimu wote wakawafanyia hayo mafunzo? Suala la

kuchukua walimu wawili kwenye kila shule na kwenda kuwafundisha, kuwafanya ndiyo wakufunzi, naona kama bado hapo kuna tatizo kwa sababu, wale ni walimu, hawawezi wakaenda kuwa wakufunzi, japokuwa wamewafundisha. Pia, wale walimu wengine wangependa wafundishwe kwa utaratibu unaofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pungufu lingine ni vitabu na vitendeakazi. Kweli, mtaala umekuja, lakini vitendeakazi hakuna. Unakuta shule ina kitabu kimoja wanaambiwa watoe *photocopy,* lakini ukiangalia maisha ya vijijini hizo *photocopy* hakuna. Je, hizi shule za vijijini zitatoaje *photocopy* kwa ajili ya mtaala huu? Naona hilo nalo ni pungufu kwenye kutekeleza mtaala huu vizuri. Suala ambalo naliona hapa ni tulitakiwa twende taratibu, ili kutekeleza huu mtaala uweze kuwa vizuri. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu huwezi kufanya *test* kwa wanafunzi. Unafanya majaribio ya mtaala wakati hujaandaa vifaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo sahihi. Ilitakiwa vifaa, kwa maana ya vitabu na kila kitu viandaliwe na walimu waandaliwe ili mtaala uanze. Hakuna mtu ambaye anakataza mtaala usianze, yote haya tunayapongeza ni juhudi nzuri, lakini tatizo ni ule utekelezaji, tulitakiwa twende taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumza hapa ni hizi shule za amali. Shule za amali hakuna kilichobadilika ni zile shule za ufundi za zamani ni kwamba, zimebadilishwa jina tu. Hizi shule za ufundi zilikuwepo na vitendeakazi vilikuwepo. Je, tumejiuliza kitu kilichoua zile shule za amali ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kilichoua zile shule za amali ambazo sisi tulisoma zamani ilikuwa ukifika, ukienda darasa la *needle work,* unakuta vyerehani vimekaa pale, ukienda darasa la *cookery room* unakuta majiko yamekaa pale, majiko ya gesi; kule mnafundishwa kupika, mnafundishwa usafi. Je, mnapoanzisha hizi shule za amali ni kitu gani kimebadilika? Vitendeakazi vimenunuliwa kwenye hizi shule za amali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo shida ninayoiona hapa kwa sababu, hizo shule zipo ni jina tu limebadilika, badala ya kuita shule za ufundi zimeitwa shule za amali. Tukienda kwenye shule za *technical college*, tulikuwa na shule nyingi za *technical college*, kuna *Moshi Technical*, kuna Mkwawa, nyingi tu, lakini kitu kilichofanya zile shule zikafifia, ni vitendeakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ninalojiuliza ni tumeanza mtaala huu tangu Januari, je, hivi vitendeakazi vimeshafika hukou kwenye hizi shule? Jibu litakuja ni hapana. Hili naona kama ni suala ambalo tunakwenda kufanya *test,* kuwa-*test* watoto wakati tayari tukiwa tumeanza mtaala tangu Januari. Napenda Wizara ya Elimu kama ingelichukua hili jambo taratibu, liende taratibu, ifundishe walimu na pia iandae hivyo vifaa ili mtaala huu uweze kukamilika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia hapa ni lugha ya kufundishia. Wazungumzaji waliopita hapa wamezungumza suala la lugha kwamba, huwezi kuachanisha Kiingereza na Kiswahili, ni lazima viende sambamba. Ili mwanafunzi au mtu aende kufundisha Kiswahili Marekani ni wajibu wake ajue Kiingereza, ili aende kufundisha Kiswahili China, sijui Japan, Australia, ni lazima ajue Kingereza. Sisi tuna matatizo ya walimu wa Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, sijui hili umejipanga vipi ili kutoa hili tatizo la elimu kwa watoto wetu, hasa kwenye hizi lugha mbili, Kiswahili na Kiingereza kwa sababu, ndiyo lugha *international* ambazo zinaenda kwa pamoja. Hizo lugha nyingine ndiyo zipo, lakini tunaangalia Kiingereza kinazungumzwa kwenye nchi ngapi? Kinazungumzwa almost duniani kote kwa sababu, Kiingereza ndiyo lugha ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watoto wetu wengi wamekuwa wakienda kwenye *interview,* siyo kwamba watoto hawana akili, wanaelewa hayo mambo, lakini wanavyoenda ku-*compete* kwa sababu, hatujawaandaa vizuri, tunaonekana kwamba hatuna vijana wengi ambao wanafanya kazi kwenye hizo *international organizations* sababu ya lugha. Ningeomba Mheshimiwa Waziri

suala la walimu wanaoenda kufundisha Kiingereza lichukuliwe kwa umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni marupurupu na stahiki za walimu. Walimu hawa ndio tunawategemea, kuna mwalimu unakuta anafundisha zaidi ya masomo matatu, lakini mwalimu huyu mshahara ni ule ule, anavunjika moyo wa kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie madai ya walimu walipwe, lakini tuangalie ni jinsi gani tunawaongezea *incentives* wale walimu ambao wanafundisha zaidi ya masomo matatu. Kwa sababu haiwezekani mwalimu anachukua masomo matatu au manne, lakini bado mshahara ni ule ule, hamna anachoongezewa, anavunjika moyo. Nilitaka hili Wizara ya Elimu iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Wizara ya Elimu ndiyo msimamizi wa Sera ya Elimu hapa nchini Tanzania. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, leo wakati anakuja kuhitimisha hoja yake ya Wizara ya Elimu, atupe msimamo wake juu ya hawa walimu ambao wanalipwa na Serikali halafu wanakwenda kufundisha shule za *private* ambazo zimejengwa na Halmashauri zetu nchini, kwenye baadhi ya halmashauri na manispaa, ili tuelewe tunaendaje? Je, ni sahihi huyu mwalimu ambaye analipwa na Serikali kwenda kutumika kwenye shule ya *private* halafu ionekane kwamba mapato yametengenezwa na halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo. Nilimtaja Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu. Nawapongeza sana Maprofesa; Profesa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda ambaye ndiye Waziri wa Elimu na *QS* wetu; Naibu Waziri, Mheshimiwa

Kipanga na wasaidizi wote wa ofisi yetu mahsusi ya masuala ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni Mjumbe wa Kamati, na kwa nukta hiyo, maana yake nakubaliana na mapendekezo ya Kamati. Nimeshiriki kujadili kwa pamoja na kwa kweli tumefanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya kuhakikisha tunatoa ushauri ambao Serikali ikiufanyia kazi, tuta-*move*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Elimu nitachangia hoja mbili na nafasi ikibaki nitachangia hoja ya tatu. Kipekee kabisa nilikuwa napitia hapa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 Sura ya tatu. Ieleweke tu kwamba huwa tunapitia ilani pia kwa ajili ya kuhakikisha tunajipima tumetoka wapi? Tulipanga nini? Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika ukurasa wa 124 hapa nilikuwa napitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, wameeleza katika huduma za jamii Sura ya tatu, nitanukuu: "*CCM inatambua kuwa rasilimali watu ndiyo nyenzo muhimu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, CCM inaamini kuwa elimu bora ndiyo nyenzo muhimu ya kujenga, kulea, kuendeleza rasilimali watu.*" Nami nakubali kwa sababu nilishawahi kusema mara moja na ninarudia tena mara ya pili leo na pengine tutaendelea kujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiizungumzia Tanzania katika mambo tunayozungumzia katika sekta za uzalishaji zote ambazo tunazijua: madini, viwanda, biashara, kuna masuala ya *logistics,* kuna masuala ya utalii, zote ni sehemu ya sekta za uzalishaji, lakini miongoni mwa vitu ambavyo ni nyenzo ya kufanikisha, hivyo vyote ni rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiizungumzia Tanzania, ukapanga mikakati yako yote, ukatengeneza mipango ya maendeleo ya miaka kumi, mipango ya maendeleo ya miaka mitano, mipango wa maendeleo ya miaka 50, lakini usizungumze kipengele cha rasilimali watu, maana yake hakuna utayekuwa umempangia. Ndiyo maana lazima tuzungumzie rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema nafurahi kuona kwamba ilani imezungumza hivi na wameipa hadhi, kwa sababu ni ukurasa wa 24, 25, 26, 27 mpaka 30 kote wamezungumza elimu peke yake. Sasa tukienda kwenye *details,* huko kuna vitu vingi, bado tunaendelea, bado miaka haijaisha. Kwa kuzungumza tu hivi, kwa kuipa hadhi kubwa hivi, kwa sababu ilani ina mambo mengi, elimu maana yake tumeona wame-*consider*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo langu la kwanza katika hili hapa na ndiyo maana nimenukuu ni ubora wa elimu, kwa sababu CCM wame-*specify* kabisa kwamba inaamini katika ubora wa elimu. Nitaanza kwa kuuliza, na leo natamani tutafakari kwa pamoja. Nimechukua vitabu cha *history* hiki hapa cha *advance (History One* na *History Two)* halafu nina vitabu vya *geography* na *biology*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kufanya *sampling.* Kwa hiyo, nimechukuwa masomo matatu; *biology, history* na *geography*. *Geography* na *biology* nimechukua vitabu vya Taasisi ya Elimu na naomba niwaambie waliyosema, sijui wako *shallow!* Hawako *shallow*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu wamefanya kazi kubwa, inawezekana changamoto ikawa sehemu nyingine na ndiyo vitabu vyao ambavyo nitavifanyia *reference* leo na najua siyo kosa lao, kuna changamoto nyingine. Hivi vingine ni vya waandishi wengine, kwa sababu bahati mbaya *TIE* hawajatoa kitabu cha *History Two*. Kwa hiyo, kuna *History One* peke yake, wanajua sababu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika ubora wa elimu, nataka kutafakari, hivi elimu yetu baada ya kuwa tumerekebisha mitaala, baada ya kuwa tumerekebisha sera, baada ya kusema sasa hivi tunashauriana hapa tutafute fedha tuandike upya sheria ya elimu kwa sababu imepigwa viraka sana; Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 tuiandike upya na Wizara ipo tayari kufanya hivyo; na kuna miongozo, kuna taratibu, kuna maandishi na kadhalika. Ni kitu

kizuri, lakini hivi tumejiuliza kwenye hivyo vitabu kuna nini nasi tunataka ku-*achieve* nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mpango wetu ni kutengeneza kizazi cha watoto ambao watakuwa wafanyakazi wa watu wengine ni sawa. Ila kama tunatengeneza kizazi ambacho tunajua *Africa is taking over,* na kama tunajua Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika ambazo kuna *paradigm shift* kubwa sana ya *global history* (historia ya dunia), watu wanaoamini katika *spirituality* na sizungumzii dini, watu wanaoamini katika imani, wanajua hiki ninachokielewa. Tuko katika mhamo *(shift)* mkubwa sana wa kihistoria na kiimani wa dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tunaendelea kuwaandaa watoto wetu wawe wafanyakazi wa watu wengine, tafadhali nisikilizeni na tutafakari wote tunafanyaje? Kwa sababu hii picha ya nje tumeifanya vizuri na ninawapongeza mno Wizara, lakini *the content,* nimechambua, nitaanza hapa kwenye *geography*. Hiki ni kitabu cha Taasisi ya Elimu na kitabu cha *Form Four,* hiki hapa na watoto wanasoma, nimeweka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna *topic* humu zipo nyingi sana, lakini *topic* ambayo nimeona ni *relevant* na ninaomba nianze kuwapongeza kwa hilo, ni *topic* inaitwa *Environmental Issue and Managements*. Wamezungumza vitu ambavyo kwa kweli wamefanya kazi na ni *current*. Kuna vitu vingi ambavyo ni *current* nitavi-*challenge* tu kidogo. Kuna baadhi ya vitu hawajaviweka, sijui tunaogopa kuwaambia nini watoto wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye *climate change,* kwa sababu mimi ni mdau wa *climate*, tumezungumza, lakini hatujasema kwamba sisi Afrika hata *percentage* ya *emission* ni ndogo, lakini *the industrialized countries,* nchi zilizoendelea ndiyo wanaosababisha athari ya *climate* ambapo sisi ni waathirika wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima watoto wetu wajue tangu wanasoma ili wawe wanajua tuna vita ya *Global North and*

*Global South*. Ndiyo maana nauliza, au sisi ni viranja? Sisi nchi za Afrika ni viranja? Au kuna watu wengine ambao wametupa sisi kazi na wanatukagua tunaandika nini, ndiyo maana hatuandiki vya ukweli? Kwa hiyo, nawa-*challenge* hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine humu humu kwenye *geography* kuna sehemu nimepa-*note* kabisa pamenisikitisha. Hiki kitabu cha Tanzania wanasoma watoto wa Tanzania, lakini hapa kuna sehemu kwenye *list* huku ukisoma kitabu utaona nime-*note, temperature and rainfall distribution for* Bulawayo Zimbabwe; *Temperature and rainfall distribution for* Brazil; *temperature and rainfall distribution for* Manila Philippines; *temperature and rainfall distribution for* Salaa Algeria; *temperature and the list goes on* Lima Chile, Namibia, Chile, Greece, Tokyo – Japan, *U.S.A the list goes on*. Sijui tunataka tu-*achieve* nini? Bado tunaendelea kusoma haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni sehemu moja. Hiki hapa pia cha *biology* ni cha *Form Four*. Sasa labda mtatusaidia ambao ni watalamu zaidi. *Do we still need to label flower plant parts*? Nini *parts* zile za ua? *Hibscuss flower,* tuna *label* pale juu tunakuwa tunataka ku-*achieve* nini? Samahani sana, mimi nilifikiri *geography* ilipaswa ituambie katika nishati, katika mifugo na uvuvi, *content* za Maafisa Ugani zilitakiwa ziwe kwenye vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri watu wa Wizarani na sekta za uzalishaji, jambo la kunenepesha mifugo linatakiwa liwe kwenye *geography* ya *Form Four* kwa sababu watoto wengi tukiita hapa nje wako…

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa…

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi?

**TAARIFA**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa…

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia hoja ya mwisho ya vitabu…

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji…

**MWENYEKITI:** Ngoja nimpe hiyo Taarifa mara moja. Mheshimiwa Kembaki, taarifa.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kumbe amekubaliana na hoja yangu kwamba *TIE* inatengeneza vitabu ambavyo viko *shallow* sana, havizingatii hali halisi ya Mtanzania na nchi yetu kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei, na mwanzo nilisema hivi, Mheshimiwa Waziri ni Profesa na yupo na jopo la wataalam. Tunapaswa tujadili, kwa sababu, ngoja nikwambie, *TIE* wamepewa *terms of reference,* wanaenda kuandika nini kwenye vitabu. Labda tunatakiwa sisi tujadili tunataka tusomeshe watoto wetu nini? Tunataka kua-*achieve* nini ili *TIE* wakaandike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIE* wanaweza kuandika chochote ambacho watapewa *terms of reference*. Kwa hiyo, siyo jambo la *u-shallow* wa *TIE,* na tafadhali, kwa sababu tunataka *TIE* waandike vitabu vyetu, tunataka *uniformity* kwa ajili ya watoto wetu waweze kusoma vitu vinavyoeleweka na siyo *issue* ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nitazungumza sehemu moja kwenye *History Two; k*atika hizi *topic* saba ambazo ziko hapa mbele, kuna *The Raise of Capitalism in Europe, topic* ya kwanza; ya pili, *The Raise of Democracy in Europe; Imperialism and World Division; Raise of Socialism;* na *Super Power. Topic* ya mwisho tu ndiyo *relevant.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri kwamba hizi *topic* zote tuziweke kwenye vitabu vya ziada. Vitabu vya watoto wetu kusoma darasani, tuwafundishe watoto wetu *Neo Colonialism and The Way Europe underdeveloped Africa*. Tafadhali sana, hatutaki kuona watoto wetu wajinga. Samahani na *with due respect,* sizungumzi kwa ubaya kwa sababu mjinga ni mtu asiyefahamu na akifahamishwa ataelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tufundishe watoto wetu jinsi ambavyo tulikuwa matajiri na *something went wrong somehow somewhere,* ndiyo maana leo tuko hapa. Kitabu kizima kilitakiwa kijae ukoloni mamboleo (*Neocolonialism*) na namna ambavyo nchi za Wazungu zilisababisha sisi tukawa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kote tunajadili, nitasoma sehemu moja tu, kwa heshima yako na samahani sana, nataka tu niwatie hasira. Najua Mheshimiwa Waziri pia hafurahii. Kuna sehemu humu napata shida kupapata, lakini kumeandikwa Camp David. Tunafundishwa hapa tunaona Camp David Marekani, Jimmy Carter. "*The Camp* David *Accord September* 1978, *Camp David in Military Camp in the U.S.A where President* Jimmy Carter…"

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wake umeisha anamalizia. Kwa hiyo, hamna taarifa.

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** …*History two,* nitazungumza hili kwa ajili ya Muungano na ninaomba kama mna…

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanaongea ovyo kuhusu Muungano, ni kwa sababu

inawezekana kuna vitu hatujavipa hadhi ya kutosha kuelezea faida za Muungano.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa ni *History One* na mnavyojua *History One* huwa imeelezea historia ya nchi. Sisi hapa Tanzania kwa waliosoma *history*, *topic* ya saba karibia na mwisho mwisho ukurasa wa 264 ndiyo imezungumza *political and economic development in* Tanzania *since independence*. Karatasi moja na nusu ndiyo imezungumza kuhusu Muungano, wameweka mpaka picha ya Nyerere. Tafadhali andikeni, chukueni nyaraka za waasisi wa Muungano.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat. *(Kicheko)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tengenezeni vitabu watoto wajue, wasome, watu waache kudharau Muungano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat. Tunamalizia na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo nimeipata. Kulingana na muda, naomba niwapongeze sana Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Prof. Mkenda na timu yake pamoja na watendaji kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita katika *point* mbili tu kwenye yale majukumu ya Wizara. Jukumu la kwanza, naomba ni-*quote: "Kutunga na kutekeleza Sera ya Elimu, Utafiti, Huduma, Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji Mafunzo na Ujuzi."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ya pili ya Kusimamia Elimu ya Msingi, katika Sera ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 inaruhusu watoto wa elimu ya msingi kwa shule binafsi kuweza kuhamia

katika shule za Serikali, lakini sera hiyo hiyo hairuhusu watoto wa sekondari kuhamia kutoka *private* kwenda shule ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichokuwa nataka kuomba, kuna mazingira ambayo yanachangia mpaka wazazi kutaka waombe watoto wao watoke kwenye *private school* kurudi kwenye shule za Serikali. Unaweza ukakuta ni wazazi kutengana, wazazi kufa, walezi kuishiwa uwezo wa kumwendeleza mtoto. Awali alifikiri atamsomesha katika shule ya *private,* lakini amejikuta mahali fulani hawezi tena kuendelea. Sasa kwa sababu sera yetu ya elimu inayazungumzia masuala haya, basi tuone namna bora ya kuweza kubadilisha. Kama tunaruhusu *primary,* basi na kwa sekondari turuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la mafunzo na ujuzi. Moja ya vipaumbele ambavyo Wizara imeelezea ni suala la Wizara kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali kwa shule zetu za sekondari na vyuo vya ufundi. Sasa changamoto ninayoiona hapa, katika elimu ambayo tayari wameshaitoa kwa maana ya walimu kuwapa elimu ya hii mitaala mipya wamekwenda katika shule 181,777. Kati ya hawa, shule za msingi ni 155,476, lakini wale walimu wa shule za awali ambao wamepata haya mafunzo ni walimu 7,454, sawa na asilimia nne, ukilinganisha na wale wengine wa darasa la kwanza mpaka la saba 148,019 sawa na 86% na hawa wengine ni asilimia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto ninayoipata hapa, msingi wa mtoto unajengwa akianzia kwenye shule ya awali, lakini ukiangalia idadi ya walimu waliopata mafunzo hayo ni wachache, lakini ukienda pia hata kwenye suala la uandikishaji ambalo linafanywa mara nyingi na TAMISEMI, wanaoandikishwa kwenye shule za awali ni wachache ukilinganisha na wanaondikishwa katika darasa la kwanza. Maana yake ni kwamba kuna watoto wengi wanaingia darasa la kwanza bila kupitia shule za awali ambako ndiko upo msingi mtoto anatakiwa kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, nilikuwa naona, kwa sababu tunahitaji kila mtoto apitie katika shule ya

awali, uandikishaji uwe kwenye shule ya awali tu na wataendelea hivyo, kusiwe na uandikishaji mwingine kwenye darasa la kwanza, kwa sababu lengo letu ni kuona mtoto anajengewa mazingira mazuri akiwa bado mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukimwandikisha awali, unaandikisha tuseme 100,000; darasa la kwanza unaandikisha 200,000. Maana yake ni kwamba kuna 100,000 pale hawakupitia yale mafunzo ya awali ambayo wanatakiwa kujengewa msingi watoto wadogo. Kwa hiyo, niliona hili tuone namna bora ya kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la watoto wenye ulemavu (wenye mahitaji maalum), tunazo shule zetu ambazo walimu 920 wamepata mafunzo na shule tulizonazo ni nyingi. Bado wasiwasi wangu ni ule ule, je, walimu hao watakidhi mahitaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua mfano tu, kwenye Jimbo langu la Ilemela tunazo shule 10 na ni shule nyingi, lakini walimu waliopo ni 15. Ni wastani wa walimu wawili kwa shule moja labda, maana huwezi kusema mwalimu na nusu. Sasa nashauri hapa kwamba tuone namna bora ya kuwajengea mabweni na kupunguza utitiri wa hizo shule ili waweze kupata mazingira mazuri ya kujifunzia na kufundishwa kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufanya hivyo, tutakuwa na shule nyingi, lakini walimu hawatoshelezi. Waliopata mafunzo katika huu mtaala mpya ni wachache, matokeo yake bado watoto wale watakuwa wanakwenda bila kufikia hatma ambayo pengine tunahitaji katika kuwajengea ujuzi tunaotaka kuufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali katika ujenzi wa shule 100 za ufundi. Tunakwenda kuwajengea watoto wetu mazingira mazuri. Rai yangu kwa Serikali, kwa sababu tumeelekea uelekeo huo, naomba sana watoto wale wanapomaliza shule, kwa sababu ni shule za sekondari za ufundi, basi wanapomaliza wapewe mitaji ya vifaa vya kutendea kazi.

Kwa kuwa wamepata ujuzi, wanatakiwa pia kama hawataendelea na chuo kikuu na mambo mengine, wanatakiwa kwenda kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta mtoto amemaliza sekondari, kapata ujuzi, lakini ujuzi ule hawezi kuutumia, nasi tunataka kupunguza tatizo la ajira katika nchi yetu. Kwa hiyo, lazima tuangalie namna bora ya kuwawezesha vitendea kazi ili wanapomaliza shule waweze kuendelea na maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naishukuru sana Serikali kwa sababu, moja ya shule za ufundi zitakazokwenda kujengwa na Wilaya ya Ilemela imebahatika. Namshukuru sana Waziri kwa sababu wananchi waliamua kutoa eneo lao la ekari 50 ili waweze kupata fursa hii. Nashukuru katika orodha ambayo iko katika watakaopata, na wilaya yangu itapata. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana pamoja na timu yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kushauri, vyuo vyetu vingi vya kati vilipandishwa hadhi na kuwa vyuo vikuu. Tunapokwenda maofisini, kule kuna changamoto na matatizo ya kiutendaji, watu wengi pale wamekaa kama mabosi kwa sababu kila mmoja ana *degree,* ana *masters,* ana *Ph.D*. Hakuna wale watendaji ambao tunaweza kuona kwamba wanaweza kuwa ni *technical clerk* katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, katika suala zima la urejeshwaji pengine kwenye vyuo vyetu vya kati vya ufundi tuweze kuona vilivyopo visipandishwe tena hadhi, lakini tuendelee kuongeza vingine ili tuweze kupata wananchi au wanachuo wenye ujuzi ambao wataweza kufanya kazi hii vizuri katika utendaji na katika shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia katika uwezeshwaji wanafunzi ni kwenye chakula. Sasa hapo kuna changamoto moja ambayo pengine naomba Serikali itusaidie kwa maana ya Wizara. Ukiangalia fedha zinazotengwa kwa ajili ya watoto walioko shule ya bweni, kwa chakula wanatengewa shiling 1,500/=, lakini aliyeko chuo cha ualimu chakula anatengewa

shilingi 5,000/=, aliyeko chuo kikuu chakula anatengewa shilingi 10,000/=. Sasa hawa ina maana na aina ya vyakula ni tofauti, kwa maana ya mahitaji, kwamba mwingine anahitaji labda chakula ambacho kina bei kubwa sana na mwingine bei ya kawaida! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri pia tuangalie namna ya ku-*review* upya, pamoja na kwamba hii ya shule za bweni inawezekana ikawa TAMISEMI au namna gani, lakini ningeweza kuishauri Serikali hebu tu-*review* pia *rate* za vyakula ambazo tunawapa watoto walioko bweni na wale ambao wako vyuo vya Ualimu na Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa wa mwisho mwisho, unakuta mambo mengi yamezungumzwa. Nizungumzie suala la mikopo wanayopewa wanafunzi wetu, kuna kuchelewa sana kupata na kunamfanya mwanafunzi pia achelewe kuwa *registered* katika shule yake. Matokeo yake sasa watoto wengi wanaanza kuhangaika, na wengi wanakuwa kama ombaomba, maana hawana uhakika na *future* yao kwenye elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana katika hili, basi iwe inatoka mapema kama ambavyo Mheshimiwa Dkt. Paulina aliongelea. Maana kunakuwa na ucheleweshwaji sana; kuna awamu ya kwanza, ya pili sijui, kwa maana ya madirisha kidogo nayo yana changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwa na bweni katika maeneo yao, mtoto wa mwaka wa kwanza anawekwa hosteli; akiingia mwaka wa pili anatakiwa atoke, kule mitaani ndiko wanakoharibikia. Naomba sana tuone namna bora ya kuongeza idadi ya hosteli katika vyuo vyetu. Mtoto wa mwaka wa kwanza na wa pili bado ni kijana mdogo, bado anahitaji pia kuwa katika maadili ndani ya chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, badala ya kuwa-*phase out* kwamba huyu amemaliza mwaka wa kwanza aondoke aingie mwingine, bado kule anaenda kutangatanga. Ndiyo unakuta watu wanaolewa, yaani anatafuta kwa kila hali ili

aweze kumudu maisha, lakini bado ni wadogo sana. Naomba sana hili, tuone namna bora ya kuwaweka watoto wetu chuoni na tusiwapeleke kwenda kupanga nje ya chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo imeendelea kutenga fedha za maendeleo katika Wizara hii ya Elimu. Mwaka 2023/2024 walitengewa shilingi trilioni 1,137 na *point* lakini fedha ambazo wameweza kupewa mpaka Aprili 15 ni shilingi bilioni 979.1 sawa na 87%. Kwa hiyo, hii kidogo inatia moyo. Tuna imani ya kwamba mpaka kufikia Juni pengine zitakuwa zimekamilika ili vile viporo alivyokuwa anavisema Mheshimiwa Dkt. Ntara katika ujenzi wa mabweni vitaweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kwa kuongeza hiyo bajeti ya shilingi trilioni 1.9, bado ni ndogo kwa elimu, lakini basi kama itatoka iweze kutoka yote. Hii Wizara ina mambo mengi ambayo yanajenga msingi wa maendeleo katika nchi yetu. Bila elimu ambayo imekaa vizuri, ambayo imewezeshwa tunaweza tukajikuta tunakwenda katika mambo ambayo siyo sahihi sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa bajeti iliyotengwa, iweze kutoka yote na waweze kupanga na kutekeleza majukumu yao waliyoyapanga ili tuweze kwenda vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda, basi naunga mkono hoja na natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais ambaye dira yake katika Hotuba yake ya Aprili hapa 2021 ndiyo imefanya pia Wizara ya Elimu waende vizuri. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula. Huyo ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa asubuhii hii au mpaka mchana huu. Tutakuwa na wachangiaji kama tisa jioni, nitawataja watatu wa mwanzo, Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava na wengine wataendelea.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, tuna tangazo la wageni ambao wapo muda huu. Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ni Viongozi wa *TAHLISO,* watalamu wanaopitia Mfumo wa Takwimu ya Elimu Tanzania na Watafiti wa Utekelezaji wa Waraka wa Elimu Na. 2, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 35 wa Mheshimiwa Ally Jumbe, Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoa wa Mbeya. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mungu kusimama mahali hapa jioni ya leo. Kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye suala zima la elimu nchini. Sitaki kurudia kusema yapi yamefanyika, siyo tu katika miundombinu, Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira kuhakikisha tunakwenda katika elimu ambayo inaitika katika mahitaji ya jamii, mahitaji ya mazingira na mahitaji ya wakati wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha elimu inakuwa bora kuendana na Mipango ya Taifa na mahitaji ya kitaaluma, nawapongeza sana Mawaziri mnaofanya kazi katika Wizara hii. Naomba niwatie moyo, wakati ni sasa, wala tusisubiri kufanya baadaye eti ili tuwe tunafanya kwa ukamilifu. Kwa hakika tumeshachelewa, tuanze kufanya sasa hata kama hatujakamilisha, *along the way* tunapunguza upungufu wetu na mwisho wa siku tutafikia ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba niseme kwamba, nimeisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza vizuri hatua mbalimbali iliyochukuliwa na Serikali katika kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali na mafunzo ya ufundi stadi, amezungumza vizuri ongezeko la vyuo vetu vya *VETA,* pia amezungumza suala zima la ongezeko la wanafunzi wa *VETA,*

vilevile amezungumza suala zima la *INTEP program (Integrated Training for Entrepreneurship Promotion)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiona dhamira na mwelekeo, naona tunapokwenda. Niwatie moyo, nimeona suala zima la *VETA* kwa kushirikiana na vyuo vya nje, vilevile naona zile *VETA* 64 ambazo zimeanzishwa, yote haya yanaonesha dhamira ya Wizara hii ya kuhakikisha elimu yetu inaitika katika mahitaji ya jamii ya mazingira na wakati wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, matumizi ya sayansi na teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda, ninashauri Serikali ifanye yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ninaishauri Serikali, wenzangu wengine wamesema hapa, *VETA* iweze kufanya tafiti katika Wilaya zetu na maeneo yetu, kubaini rasilimali tulizonazo na itengeneze mitaala kulingana na rasilimali zilizopo katika maeneo yetu ili kuongeza thamani ya vitu vilivyopo na kuibua ubunifu na ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale kwetu Mkinga tumeanzishiwa *VETA*. Pale Mkinga kuna madini ya kutosha ya *Tanga Stone,* tunaomba *VETA* ihakikishe inashirikiana na vile vyuo vya kuongeza ubora na thamani ya madini, kuhakikisha tunapata mitambo kuwezesha vijana wa pale, kuhakikisha tunazalisha ajira na ubunifu na ku-*add value* katika madini yale kwa mustakabali mpana wa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninaishauri Serikali ione namna ya kuhamasisha kuanzishwa kwa *professional bodies* ili tuweze kupunguza mianya kati ya wanachuo wanaotoka shuleni na waliopo mtaani. Lazima isimamiwe *professional bodies* zianzishwe. Tunajua mtaani kuna wanataaluma wazoefu na wenye viwanda waweze kuunganisha nguvu kwa pamoja kuondoa *gap (academic gap)* kwa wanafunzi wanaotoka vyuoni ili jamii iweze kupata tija kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwanafunzi yeyote, awe ni *mechanical engineer* au *electrical engineer,* anapoingia chuoni, akisajiliwa kama mwanafunzi au mjumbe wa bodi ya *mechanical engineers* Tanzania, itawezesha mwanafunzi yule anapofanya tafiti zake, kwenda kutengeneza makongamano kwenye hizi bodi huku mtaani na kuweza ku-*share* kile anachokifanya na hawa huku wazoefu mtaani ili kuondoa lile *gap* na ku-*share* maarifa yale. Hii itasaidia kuibua *the state of art technology. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesema, ili elimu yetu iwe bora kuendana na mipango ya Taifa, maana yake elimu ni *cross cutting issue*. Kwa hiyo, ni lazima tuone ni kiasi gani Wizara hii inakuwa *pro-active enough* kugundua *gaps* zilizopo mtaani na namna ya kuhakikisha zinazibwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile najua bodi hizi huwa zinakuwa ni bodi binafsi, kama vile Taasisi ya Wahandisi Nchini ni bodi binafsi, lakini kwenye taasisi ile utakuta wahandisi wote tuko ndani ya *umbrella* moja, lakini tukigawanywa kwa mujibu wa taaluma zetu na tukishirikiana na vyuo vikuu vyetu na Maprofesa wale wakiweka kwa pamoja mipango ya kuanzishwa makongamano ambayo yatasababisha kufanya tafiti, tafiti zao zinakuja huku mtaani kwa wataalamu na baadaye zinakuwa *published*. Itasaidia sana kupata *the state of art technology* ambayo inakuja kusaidia ukuaji wa taaluma, ajira na ubunifu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wameweza kushirikisha *VETA* na nchi nyingine tano kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri, vilevile tunaweza kupata uzoefu kutoka kwenye nchi mbalimbali ambazo zina hizi *professional bodies.* Zipo nchi ambazo mpaka sasa zinafanya makongamano ya miaka 60 ya *Technical Engineers* labda, au miaka 60 ya *Electrical Engineers.* Muda wote huo wamekuwa wakikusanya taaluma mbalimbali kwa kushirikiana na vyuo na zile *professional bodies.*

Mheshimiwa Spika, nafikiri nasi tukajifunze pia kutoka kwenye nchi za wenzetu ili tuweze kuanzisha hizi bodi kupunguza *gap* la elimu nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ili kuchochea tafiti ni lazima tuanze na maktaba kwenye maeneo yetu. Hebu tujiulize huko kwenye Wilaya zetu, maktaba zetu zipo katika hali gani? Utakuta maktaba hazipo. Kuna majengo tu yamewekwa hayana vitabu. Hatuwezi kuhakikisha tunafanya tafiti za maendeleo kama watoto huku chini hawajengewi utamaduni wa kujisomea katika maktaba zetu ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, maktaba ya Tanga imeanzishwa mwaka 1958, lakini ni chakavu kupitiliza, na ipo Tanga Mjini. Hapo tunaibua vipi mambo ya kufanya tafiti. Hata walimu waliopo kwenye Mkoa ule hawaoni haja ya kuwasogeza watoto kwenye maktaba zile ili kujenga utamaduni wa kujisomea na kuweza kuibua tafiti. Tafiti unazipataje kama hufanyi *literature review?* Unazipataje tafiti kama hujui wengine wamefanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Makamu wa Rais wetu, alipokuja Tanga nililiibua hili na ninashukuru sana Prof. Franklin, nimeambiwa hatua ambazo amezichukua kuhakikisha kwamba vitabu vya kiada vimekwenda na Maktaba yetu ya Tanga inarekebishwa. Naomba sana maktaba zote katika Wilaya zetu ziweze kutengenezewa uwezo wa kuwa na vitabu vya kutosha na walimu waone dhamira ya dhati kuwapeleka vijana karibu na maktaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maktaba siyo magofu ya kumbukumbu, maktaba ni mahali ambapo wanafunzi wanapaswa kwenda kuwekwa karibu na kujisomea. Walimu wanapaswa kuwa na hamu hiyo kuwajengea uwezo, la sivyo kama huku chini hawajapata hayo, hawezi kwenda chuo akasoma *reference books.* Atakuwa anatoka kwenye vitini vya walimu mle, mwisho wa siku anakuja mtaani mnasema wanafunzi wa vyuo vikuu wapo *shallow,* kumbe kule chini hawajajengewa utamaduni wa kuanza kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kusema yafuatayo: Naomba nizungumzie kuhusiana na Tume ya Mionzi Tanzania *(TAEC)*. Kuna mradi wa *Multipurpose Food Radiator* ambao uko pale Msakuzi. Mradi huu utatugharimu *almost eight billion.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naona umekaa sawasawa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, Nami naungana na wenzangu kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu, na kwa ujumla wake, viongozi wote wa taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hii. Kwa kweli wanajitahidi sana na tunazidi kuwatia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imepata wachangiaji wengi ambao wanaonekana kuifahamu vizuri Wizara hii na shughuli zake, wanatoa hoja ambazo kimsingi ndizo zinazoendelea katika maisha yetu ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, leo napenda kutoa mchango wangu katika maeneo hayo ya kawaida kwa sababu pengine ndiyo nitaeleweka kiurahisi zaidi. Suala la umuhimu wa kuimarisha elimu msingi, hilo kwa kweli halina ubishi, kwa sababu Wizara hii ndiyo inayosimamia udhibiti wa ubora wa elimu, hilo lazima tuendelee kulisisitiza.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tuliona jinsi mitaala yetu inaonekana kuwa haiko sawa, tukafanya jitihada ya kukaa pamoja na kushauriana nini kifanyike, vivyo hivyo, ningetamani sasa suala la wanafunzi au watoto wanaotoka kule vijijini, kwenye Majimbo hasa ya vijijini ambayo hayana wafanyakazi au watumishi wa kutosha, hususan walimu kwa kweli lifikie mahali lipate jibu.

Mheshimiwa Spika, sioni kwa nini Wizara iwe na furaha ya kuendelea kutoa mtihani mmoja kwa wanafunzi wote wakati

wengine hawana walimu. Mimi naona hiyo siyo kuwatendea haki na hapo mwishoni na pengine tutashika shilingi, watufahamishe ni namna gani wanawasaidia hawa wanafunzi, hasa ambao hawako vijijini, kwa sababu wanakosa hiyo elimu iliyo sahihi na bora.

Mheshimiwa Spika, pia inavyokuja kwenye kupata nafasi za kuendelea juu wanazikosa; na inapokuja kwenye fursa za ajira watazikosa. Kwa hiyo unakuta kuna maeneo ambayo yataendelea kuwa maskini na duni, wakati tumeshasema kwamba elimu ndiyo msingi wetu wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, napenda kuona katika haya mabadiliko tunayoendanayo ni kuona sasa hizi shule za amali zinatusaidia katika kulitoa Taifa hili kuondokana na ukosefu wa ajira. Sasa nataka nijue, tumeshasema kwamba tutajenga shule za kutosha zaidi ya 100 kwenye maeneo, tumejipanga vipi? Kwa sababu naogopa. Mwaka 2016/2017 nilitembelea Shule ya Ufundi Mtwara, nikakuta ile shule karakana zake zinatumika kwa ajili ya mfanyabiashara mmoja wa ufundi na magari yake, pale hakuna mwanafunzi anayechukua hiyo fani.

Mheshimiwa Spika, nikaenda Ifunda, nikakuta mambo ni hivyo hivyo. Nilipoenda Bwiru nikakuta mfanyabiashara kapewa karakana ile, anaitumia kwa mambo yake. Sijui wapo wanafunzi 0wawili watatu wanaenda kujifunza wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia imeenda mpaka Chuo cha Ualimu kilikuwa pale Mkwawa ambacho kilikuwa kinafundisha masuala ya ufundi, nikakuta kinafundisha mambo tofauti. Sasa hofu yangu ni kutokujidanganya kwamba tunaanzisha hizo shule nyingi ambazo zitahitaji vifaa vingi vya ufundi, halafu tusiviweke na tuseme kwamba tayari tumeshaanza, kwa sababu kwenye ufundi haya mafunzo ya amali hayana uwongo, lazima tu ufanye lile ambalo linafanana na kumwezesha huyu mwanafunzi kufahamu inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwamba, pamoja na jitihada hizi ambazo tayari zimeshafanyika na tunazoendelea

kuzifanya, basi tusiwe waoga katika kufanya maamuzi ya kuzisadia hizo shule au hivyo vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano pia mwaka 2023 tulikuwa tumeona kwamba wale wanafunzi wanaochukua *diploma* za kawaida kwenye vyuo vya ufundi, wasaidiwe nao kupata mikopo. Wanafunzi hao ndio tunaotegemea watakuja wengi sasa kutoka kwenye hizo shule za amali ambazo tutazianzisha, lakini waliopata mikopo ni wachache mno.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *DIT* wanafunzi kama 116, kule Mbeya *MUST* wanafunzi 114, na vyuo vingine, hiyo idadi ni ndogo sana. Kwa misingi hiyo inakuwa kama vile maamuzi yetu tunaenda nayo kwa uwoga fulani hivi. Naomba tuliangalie eneo hili ili tuwawezeshe wanafunzi wengi zaidi kuhitimu wakiwa wamepata hizi fursa za kiufundi vizuri na waweze kwenda kulisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nashukuru sana Mheshimiwa Mhandisi mwenzangu ameyazungumza vizuri tu kuhusiana na masuala haya ya kusaidia *practical.* Ukishakuwa kwenye maeneo ya ufundi, lakini maabara zake haziwezeshwi (siku hizi tunasema kuna *teaching factory,* ziweze kumsaidia huyu mwanafunzi kulingana na mazingira yale ambayo ameshasema hapa, tupate suluhisho la tatizo fulani), itakuwa haisaidii.

Mheshimiwa Spika, mimi naona kwamba, vyuo vyetu vimekuwa vikijitahidi sana kubuni mambo mazuri ya kuweza kusaidia nchi yetu, lakini inapokuja kwenye kuviwezesha, mara nyingi utoaji wa fedha umekuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa inawezekana fedha zetu ni kidogo, basi niombe taasisi zetu na vyuo vyetu vikuu ambavyo vinafanya tafiti mbalimbali, siyo tu katika kugawana hivi vilivyopo, tuongeze jitihada katika kubuni vyanzo vya mapato ili sasa tunaposema tunaenda kwenye haya maeneo ya kuimarisha na kuboresha, basi fedha isiwe ni tatizo tena; kwa sababu tutazungumza lakini fedha hatutapeleka.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, nashauri sana, vyuo hivi viweze kusaidiwa, vipewe fedha za kutosha, vijengewe maabara za kutosha, vijengewe viwanda vya kujifunzia vya kutosha, ili sasa mwanafunzi anapotoka hapo awe amekomaa na aweze kwenda kuonesha kwa vitendo kazi zake. Hata mwajiri atakuwa na furaha kumwajiri, kwa sababu anamwona kabisa huyu sio kwamba nachukua mzigo, bali anakuja kunipa faida. Mwajiri yeyote yule anampenda mtu anayemsaidia kumpa faida. Hampendi mtu wa kumlea kama mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, nasema hivi kwa sababu nimefuatilia, kwa mfano Chuo cha Mwanza cha Ufundi *(DIT), w*ale waliamua kuona kwamba eneo la Mwanza kuna faida ya wanyama wengi, kwa mfano ng'ombe wako wengi, basi tuanzishe mitaala yetu na kazi zetu zitakazoendana na kutoa jibu au suluhisho la matengenezo ya ngozi mpaka viatu. Kweli wale wanafunzi wanafanya kazi nzuri sana na mlezi wao ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza. Hiyo sasa iendelee katika maeneo mbalimbali.

Mhshimiwa Spika, kila chuo kinyang'anyane, kiseme kwamba mimi naenda mkoa fulani kulingana na ile kazi ambayo wao wanaifundisha pale kwao. Hatutaki tena kuendelea kuona tunatafuta fedha kupeleka kwenye vyuo. Vyuo vyenyeye havituridishii fadhila, ni lazima vipeleke fedhili ya moja kwa moja, ukiacha ile ya ujumla kwamba tumesomesha wanafunzi kadhaa, lakini sasa iwe hata mwananchi wa kawaida anaona matokeo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kwenye kile chuo kule Chondiem, kile chuo kinatoa suluhisho kubwa sana katika masuala ya uhandisi, ni kikubwa mno. Ikitokea kuna jambo lolote lile, mfano sijui watu wanataka kupeleka *cable,* kwa mfano hizi *marine cables* kuvusha labda kupeleka sehemu fulani, utakuta kile Chuo ndiyo kinaenda kufanya tafiti, kinatoa suluhisho za aina mbalimbali. Kwa hiyo, hata sisi hapa Tanzania inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo *workshops* zetu nyingine nzuri tu, kwa mfano pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hivi

tunawatambua vipi? Tunawasaidia vipi ili kuweza kusaidia jamii zetu inavyowezekana? *(Makofi)*

*(hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, basi ninashukuru lakini naona kwamba, kama ambavyo tuliujadili mtaala huu, basi hata namna ya kuutekeleza tutengeneze utaratibu maalum wa kushauriana ili twende vizuri pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, na Mheshimiwa Ally Makoa ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii na kibali cha kuweza kusimama na kuweza kuchangia hotuba hii. Nawashukuru sana Waziri, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nawapongeza wafanyakazi wote wakiwemo walimu katika nchi yetu ya Tanzania kwa kazi kubwa ambayo wanakuwa wanaifanya kuhakikisha kwamba elimu inaboreka katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa bajeti hii na moja kwa moja ninaiunga mkono. Kwa nini ninaiunga mkono? Ni kwa sababu Wizara hii imekuwa ikitekeleza majukumu yake. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, imeweza kutekeleza miradi ya

maendeleo kwa 68% na fedha ambayo iliidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa 68%. Kwa hiyo, naweza kusema kwamba wametekeleza kwa jinsi ambavyo waliweza kupatiwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bajeti ya mwaka huu tumeona ongezeko kubwa la Bajeti ya Wizara hii ya Elimu. Zaidi ya 13.74% imeweza kuongezeka. Ukiangalia kwa mtiririko, kwa miaka mitatu zaidi, Wizara hii imekuwa ikiongezewa fedha. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka 2021/2022 Wizara hii ilitengewa shilingi trilioni 1.446 lakini mwaka 2022/2023 ilikuwa shilingi trilioni 1.493, mwaka 2023/2024 ilikuwa shilingi trilioni 1.675 na mwaka huu 2024/2025 wameweza kutengewa bajeti ya shilingi trilioni 1.905. Kwa kweli haya ni maendeleo makubwa sana kwenye sekta yetu ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona katika bajeti hii Wizara imekuwa na vipaumbele. Katika mojawapo ya vipaumbele ambavyo wamevitaja ambavyo wanavifanyia kazi ni huduma ya maji na usafi wa mazingira. Katika kipaumbele hiki, cha kushangaza ni kwamba, fedha za ndani hawakupanga fedha yoyote isipokuwa kwa fedha za nje wamepanga shilingi bilioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza, kipaumbele hiki cha huduma ya maji na usafi wa mazingira ndicho kipaumbele ambacho kwa asilimia kubwa shule zetu hasa za msingi na sekondari zinaguswa moja kwa moja. Sasa kama fedha ya ndani hatuoni umuhimu wa kutenga bajeti, tunategemea vyoo wanavyotumia watoto wetu tupate msaada, je, tutafika?

Mheshimwia Spika, napenda Mheshimiwa Waziri aje aniambie hapa atakapohitimisha, ni kwa nini katika kipaumbele ambacho ninyi wenyewe kama Wizara mmekiainisha lakini hamkupanga fedha za ndani, mnategemea fedha za nje? Je, ni kweli tutakidhi takwa la kuhakikisha kwamba wanafunzi wa shule

za msingi na sekondari wanapata vyoo safi na salama kwa fedha hii ambayo wamepanga kwa kutegemea wafadhili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ina maana mfadhili asipotoa hii fedha watoto wetu hawatakuwa na vyoo, wala hawatakuwa na maji salama. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kipaumbele kingine ambacho mmesema mtaimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi ngazi ya msingi, sekondari na huduma za maktaba. Katika kipengele hiki mmetenga fedha za ndani shilingi bilioni 1.5. Tunashukuru kwa kutenga hiyo fedha, lakini najiuliza, hii shilingi bilioni 1.5 kwa mikoa tuliyonayo Tanzania na kwa maktaba ambazo tunazo na mna-*plan* kujenga maktaba nyingine, hii maktaba itakuwa Makao Makuu ya Mkoa; yule mtoto anayetoka Mwashilugula kule Shinyanga, anayetoka Mwakitolyo, ataweza ku-*afford* kuja mkoani hapa kwa ajili ya kutafuta huduma ya maktaba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huyu mtoto atahitaji rasilimali fedha, je, mzazi ataweza kumpa mtoto wake fedha atoke kijijini aje mjini kwa ajili ya kufuata maktaba? Kwa nini fedha hizi msizielekeze kwenye suala zima la kuchapisha vitabu ili kila shule iweze kuwa na vitabu vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, kwenye taarifa yenu mmesema kwamba mmeshaanza uchapishaji wa vitabu na kuna baadhi ya vitabu takribani kama 9,000 ambavyo vimeshaanza kusambazwa, lakini kuna vitabu ambavyo kwa taarifa ambazo ninazo mnavituma *online*, mnatuma kwa *softcopy*. Sawa, mmewapa walimu vishikwambi, je, ni walimu wangapi ambao wanaishi kwenye mitandao ya *internet*? Ni walimu wangapi ambao wanaweza waka-*afford* ku-*download* hivyo vitabu na kuweza kuvi-*distribute* kwa wanafunzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni kwamba inazidi kuongeza mzigo kwa walimu hawa ambao wanaishi katika mazingira magumu ambao kwa kweli hawana hata motisha ya kazi ngumu

wanayoifanya ya kuelimisha watoto wetu? Kwa nini tusichapishe vitabu vya kutosha badala ya kufikiria kujenga?

Mheshimiwa Spika, maktaba siyo mbaya, siyo mbaya kabisa, tunahitaji watoto wetu waweze kusoma, lakini mazingira ya hizo maktaba ndiyo shida. Unakuta maktaba iko mkoani, sidhani kama kuna wilaya ambazo zina maktaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, kama maktaba mnajengea mkoani, hao watoto wa vijijini watafanya nini? Kwa nini msije na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba mnachapisha vitabu vingi vya kutosha halafu mnavisambaza kwenye shule? Kwa sababu, mkiendelea kusema mjenge maktaba, sawa ni wazo zuri lakini mwatumie walimu vitabu kwenye vishikwambi vyao ili wao wavizalishe, tunawapa kazi ambazo sidhani kama wataweza kuzitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumeona kuna sheria ambayo inasimamiwa na Wizara hii, Sheria Na. 25 ya Mwaka 1978 imekuwa ikifanyiwa marekebisho madogo madogo mara kwa mara. Mimi ninachokiona, kwa sababu sheria hii na kanuni na miongozo imekuwa ikikinzana na matakwa ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023, unakuta kwamba anayesimamia mipango, hata fedha ambayo tutaipitisha leo, fedha nyingi itaenda TAMISEMI, haitabaki Wizara ya Elimu. Itakwenda TAMISEMI ambako ndiyo wana elimu za sekondari, wana elimu za msingi na *VETA* sasa hivi ziko huko, na kuna vyuo ambavyo viko kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kuna umuhimu wa kufanya marekebisho na mapitio ya sheria hii ili sasa kusiwe na mkanganyiko, kusiwe na sera ambazo zinakinzana, kwa sababu kumekuwa na miongozo mbalimbali ambayo inatolewa. Unajikuta wakati mwingine hiyo miongozo ambayo inatolewa inakinzana na sheria iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtekelezaji ni TAMISEMI, lakini elimu anasimamia ubora wa elimu, anahakikisha kuna vitabu, anahakikisha mitaala ipo, inafuatwa vizuri, lakini *REO* na *DEO*

wako chini ya TAMISEMI. Yaani pale mkoani anasomeka kama mwakilishi wa Kamishna ambaye Kamishna yuko Wizara ya Elimu. Mimi ninaona kama kuna mkanganyiko, kuna vitu ambavyo vinaingiliana.

Mheshimiwa Spika, basi ni wakati mzuri wakae chini; najua wamejaa maprofesa na madaktari, nafikiri kuna umuhimu sana wa kuboresha hii Miongozo, Kanuni na Sheria ili kusiwe na mwingiliano. Shule nyingi ziko kule; shule za msingi, sekondari, vyuo, kusiwe na mwingiliano ili basi mipango hii mizuri ambayo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaipanga, iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Ooh!

Mheshimiwa Spika, nimeshaunga mkono hoja. Naomba sana, sana, sana kufuatilia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Makoa, na Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Elimu. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwamba ameendelea kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu, hasa kuanzisha mitaala mipya ambayo ninaamini kwamba Watanzania wote wanaunga mkono maboresho haya ambayo Mheshimiwa Rais ameruhusu yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Profesa na wenzanke wanafanya kazi nzuri, akiwepo mwalimu wangu wa *Chemistry, first year, University of Dar es Salaam*, Prof. Mdoe, *CH 100*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni Wizara muhimu sana, ni *software*. Tunatengeneza Watanzania wa miaka 100 ijayo. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri hata anapokuja kujibu na kuhitimisha hoja, yaani inabidi achukue hoja za Wabunge kwa umakini mkubwa. Kuna mengine yanahitaji majibu ya moja kwa moja akayafanyie kazi kwa maana ya kuboresha *with time,* kwa sababu, maboresho haya hayachukui muda mwingi, hapa huwezi kuimarisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *target* ya Serikali hapa ni kwamba tuna changamoto kubwa sana ya ajira. Kwa hiyo, tunatarajia baada ya kuanzisha mitaala mipya tupunguze vijana wa Kitanzania ambao wamesoma na hawawezi kujiajiri. Kwa hiyo, aweze kuajiriwa, lakini pia aweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo kuna hoja nyingi sana. Kuna upinzani kwamba kwa nini leo unawaambia watu wakajiajiri wakati ninyi mmepata ajira ya Serikali? Kwa hiyo, unahitaji kufanya kazi kuwafanya watu waelewe tunalenga kitu gani? Lazima wakubali kwamba wakati ni ukuta, kwamba, kuna muda ambao Serikali iliweza kuajiri watu, kwa sasa wasomi wote hawawezi kuajiriwa na Serikali. Yaani wakubali hivyo, *then* tutengeneze namna bora ya kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zimetangazwa hapa tahasusi 65, zimeongezeka mpya 49. Nikajaribu kuangalia hapa tunalenga nini? Kwa mfano, tahasusi ambazo zinahusika na mambo ya kijamii zipo tisa, zinazohusiana na lugha zipo 11, zinazohusiana na biashara zipo saba, sayansi zipo saba peke yake na dunia ya sasa inatawaliwa na sayansi, lakini michezo zipo saba, sanaa zipo 16 na dini zipo nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukimwuliza Profesa kwamba katika tahasusi hizi kwanza mlikuwa mnataka kulenga kitu gani? Pili, mna vitabu vya kutosha kwa haya masomo mapya ambayo mmeleta? Vimechapishwa tayari? Mna walimu wenye ubora wa kufundisha masomo haya ambayo yanaanzishwa sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya ili kuondoa wasiwasi wa Watanzania hasa vijana ambao wanaenda kusoma, ni vizuri tuwe na majibu sahihi na hili halihitaji siasa katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba kwa baadhi ya wilaya Serikali imepeleka fedha kuanza kujenga *VETA,* nami nimepata *VETA* kule Nyamongo – Nyabichune inaendelea vizuri. Sasa naomba, katika *VETA* hizi pia, unapotaka kutengeneza ajira kwa Watanzania walio wengi, lazima u-*target*. Wamesema Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba, kama umepeleka kule Nyamongo *VETA*, kule kuna wachimbaji wadogo. Katika masomo mtakayofundisha pale, *course* hizo lazima uweze ku-*consider* uchimbaji mdogo kwa watu ambao wanazunguka eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale kuna wafugaji na kuna wavuvi; pia kuna Mto Mara pale. Kwa hiyo, tunatarajia walimu ambao wataenda pale na vitendea kazi viendane na mazingira ambayo *VETA* ipo katika eneo hilo. Ukijenga *VETA* katika maeneo ambayo watu wake ni wafugaji, maana yake utakuta wote wanapata taaluma na watapata ajira. Kwa hiyo, malalamiko mengi yatakuwa yamepungua katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hii elimu ya amali ambayo inaanza kwa *primary*, kwa maana ya kote, lakini na baadhi kwa sekondari. Pia kumekuwa na maswali katika eneo hili. Hivi Mheshimiwa Profesa anaweza kutuambia leo kwamba ameshakarabati karakana ngapi zilizokuwa za zamani kwa teknolojia ya kisasa ya dunia? Amejenga karakana zipi mpya za kisasa katika maeneo yetu? Pia ni maeneo ambayo anatakiwa utueleze. Kwa mfano, kuna *course* ya ushonaji, hivi una mashine mpya za kisasa za ushonaji? Kama ni useremala, hivi vitu vipo? Haya maswali pia na mengine yatafakariwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni sayansi ipo ya eneo fulani, kwa mfano kwenye hizi *VETA* na vyuo mbalimbali vya kijamii, kuna maabara za kisasa zimejengwa katika eneo hilo? Kuna maji ya kutumia kwenye *chemicals*? Kuna umeme wa kutosha? Kuna *standby generator in case* umeme umekatika? Umeandaa

walimu wa kutosha? Je, waliopo sasa ni wa zamani? Wamefundishwa hii taaluma ya sasa ili wakaboreshe ufundishaji kwa vijana wetu? Hayo pia ni maeneo ambayo ni muhimu sana yakazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka nichangie, kwenye taarifa ya Kamati yenyewe wameonesha wasiwasi. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hoja yake ni vizuri atueleze, Kamati wanasema wana wasiwasi na miundombinu pungufu iliyopo kwa ujumla wake, wametaja hapa kwenye ukurasa wa 14. Wanazungumza kwamba vitabu havitoshi vya mitaala mipya na huenda baadhi ya maeneo ni vichache sana. Pia wamesema hata fedha za mikopo ambazo ziliwezesha, na hii lazima litolewe maelezo.

Mheshimiwa Spika, ukiwaambia hawa watoto waliopo shuleni na wazazi, Mheshimiwa Rais ameshatamka kwamba ameongeza fedha ya mikopo halafu wanasema humu zimepungua. Lazima uonyeshe umepunguza eneo lipi katika mazingira hayo ili pia isilete taharuki.

Mheshimiwa Spika, katika tathmini, mmekuwa mkitoa mikopo 20%, 40%, 60% mpaka 100%. Hivi tathmini imefanyika? Wale watoto ambao walipata 20%, 40% halafu wazazi na wadau wakashindwa kuwasomesha wakaacha vyuo, hivi wako wapi? Hii fedha ina maslahi gani kwa Watanzania? Kuna mtu umempa 40%, mzazi au mlezi hawezi kumsomesha, ameenda ameripoti chuoni na wengine kimsingi wamechanganyikiwa mtaani. Je, umefuatilia katika maeneo hayo? Kwa hiyo, haya mambo ni muhimu sana kwenda kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Rais wa Chuo pale Mlimani mwaka 2005/2006. Katika migomo ambayo niliwahi kuendesha pale, watu ambao niliwaongoza humu ndani wapo ninawaona, wapigakura wangu wa zamani wa Mlimani wapo hapa. Tuligoma pale Mlimani Chuo kikafungwa mara mbili, mara tatu kwa sababu ya *boom*. Kwa hiyo, *boom* hii ilikuwa shilingi 2,500/= ikaongezwa shilingi 2,500 ikawa 5,000. Nilipambana nikakuta, sikuitumia ile

shilingi 5,000, ikaja mwaka 2009/2010 ikaenda shilingi 7,500, shilingi 8,500, leo ni shilingi 10,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maisha ya kawaida tungetarajia Mheshimiwa Rais ikimpendeza na kama hali itaruhusu, hawa vijana wapewe hata shilingi 20,000, itawasaidia sana kuboresha maisha yao kwa sababu mahitaji ni makubwa sana. Sasa kama kuna lugha nyingine zimetumika, na nimeona vijana wamepokea *very negative*, mimi nasema hao vijana kuwapa *boom*, mimi mwenyewe limenisaidia sana wakati ninasoma. Unaweza ukawa umekwama ukanunua vitabu. Umezungumza hapa maktaba vitabu havitoshi, kwa hiyo, tulikuwa tunachangisha kwenye chumba ili mtu anunue kitabu na vitendea kazi vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna matumizi mengi sana ambayo fedha hii inaweza kuwasaidia vijana wakawa *comfortable*. Tunachotaka ni kwamba Mheshimiwa Rais apeleke mikopo, watoto wapewe *boom* wasome. Jambo la muhimu ni kwamba waweze kufanikiwa vizuri wakaboreshe jamii zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri swali, hivi kwa elimu ya Tanzania tangu tumepata uhuru mpaka leo, ni sahihi Wabunge humu ndani kuwa na kigezo cha kujua tu kusoma na kuandika na ikatamkwa kwenye vitabu! Ni sahihi? Yaani mpaka leo kwa nchi hii ni wasomi wengi na wataalamu, lakini kwenye vitabu inasoma kwamba sifa ya Mbunge ni kujua kusoma na kuandika. Kama kuna hoja ya mtu kujua kusoma na kuandika, lakini anajua nini cha ziada? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kishimba hapa mpaka amepewa jina la Profesa, siyo msomi, lakini ukimsikiliza mambo yale ni makubwa kweli kweli kuliko hata ya ma-*doctor* wengi nchi hii. Sasa nadhani hii pia ni muhimu, maana yake ukiongea Mbunge wanafikiri wote humu darasa la saba au la saba siyo chochote. Hapana, kafanyeni tathmini, kuna mtu aliishia darasa la saba, ana nini? Kuna ile wanaita *extra curriculum*. Ni kitu gani cha ziada anakijua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu mtu ni mtaalamu kuliko hata maprofesa wengi, lakini kwa sababu tu anatakiwa vyeti, anakuwa *labelled* kwamba kujua kusoma na kuandika. Kwa hiyo, nadhani Wizara ya Elimu mambo haya ya msingi mtusaidie kubadilisha ile *mentality* ya Watanzania ili Wabunge pia wapate heshima kwamba unaweza ukawa darasa la saba lakini unajua vitu vingi.

Mheshimiwa Spika, wengine hapa wanamiliki mitaji mikubwa, wanafanya biashara, wametembea nchi mbalimbali, wana mambo makubwa ambayo wanafanya na huku wanaweza wakachangia michango mikubwa sana kuliko hata wasomi, ili tuone kwamba kumbe kusoma siyo kuwa na vyeti tu. Unaweza ukawa na elimu nzuri na bado hauna vyeti na ukafanikiwa katika maisha na ukaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaangalia hata duniani, viongozi wengi wa nchi kubwa ambazo zimeendelea wala siyo wasomi sana. Wasomi wamebaki ofisini kufikiria, kutunga vitabu na kuandika, wale watu ambao wanaweza kusimamia, wanafanya kazi hiyo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningetamani kwamba Wizara hii kwa maswali mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa na kuuliza na wamezungumza, kwa mfano tulikuwa na upungufu wa walimu hasa wa sayansi katika shule zetu. Unapoongeza wigo wa tahasusi na elimu ya amali, hivi Watanzania wajipange katika lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niunge mkono hoja. Nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara, kuna hoja yako umeianza lakini hujaihitimisha. Umesema kwamba kuna haja ya kuandika kigezo cha Ubunge kama ni kusoma na kuandika. Wewe unamshauri nini Mheshimiwa Waziri?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba ikibaki tu kwamba Waheshimiwa

Wabunge humu uwezo wetu uwe ni kujua kusoma na kuandika tutakuwa *undermined.* Maana yake kama kuna mtu amesoma elimu fulani itamkwe, hata kama ni darasa la saba, anajua kusoma na kuandika lakini anajua vitu vya ziada. Hivyo, iwepo kwenye *CV* yake, na waelezwe kwamba hiyo ni ya ziada tu, lakini unaweza ukauliza vitu vingine vya msingi sana, ndiyo hoja yangu hapo.

Mheshimiwa Spika, ukienda hata Kenya hapo wameweka masharti kwenye Bunge...

**SPIKA:** Haya umeshaeleweka. Mheshimiwa Waziri atakuwa na kazi hapo ya kuchagua kati ya ulichosema, maana kimsingi wewe mwenyewe unataka watu wenye elimu wakati huo huo unataka tena na darasa la saba. Kwa hiyo, kusoma na kuandika bado kinaendelea kuwa kigezo cha msingi kabisa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ally Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex ajiandae.

Kwa kuwa Mheshimiwa Makoa hayupo, namwita Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwa hai na kuwa ndani ya Bunge hili. Nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Mkenda na timu yote ya Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu mwanzo nimesema sijawahi hata siku moja kuwa na mashaka na Mheshimiwa Prof. Mkenda, tofauti yetu ilikuwa ni kwenye suala moja tu la *RPL (Recognition of Prior Learning)*. Bado naendelea kuomba kwamba suala la *Recognition of Prior Learning* liweze kufanyiwa kazi ili Watanzania wenye ujuzi ambao hata kama hawana sifa kubwa sana waweze kupatiwa nafasi ya kuendelea na masomo ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Amefanya kazi kubwa sana, madarasa mengi yamejengwa, vituo vya afya vingi na kazi kubwa inaendelea kufanyika katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana nilipata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Prof. Mkumbo kwa muda, nikamwambia umepata bahati kubwa sana ya kuandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa, ya kwamba unachokifanya hakitakuwepo mpaka mwaka 2050. Jambo moja kubwa nililomwomba jana, anitengenezee watoto wenye akili, watoto wenye uwezo mkubwa, watoto wenye uwezo wa kushindana katika dunia inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya uhuru wa nchi yetu, wazee wetu walituandaa sisi na tumefika hapa tulipo leo, tunafanya tunayoyafanya, lakini ni ukweli ulio wazi kwamba sisi na watoto wetu tunashindwa kushindana kwenye ulimwengu wa sasa kwa sababu hatukuandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajadili Wizara ya Elimu, swali ninalojiuliza, tunamtengeneza mtoto wa aina gani? Tunamtengeneza mtoto wa aina gani mwaka 2050 ambapo tutakuwa na ulimwengu wa kidijiti zaidi, *internet of things*, *cloud computing* na mambo mengine mengi yatakuwa yanafanyika kwa kutumia *artificial intelligence*? Je, tunamwandaa mtoto wetu aweze kushindana vizuri kwenye ulimwengu huo wa mwaka 2050?

Mheshimiwa Spika, kwangu elimu ni kama fyatulio la tofali. Kule kijijini tuna mafyatuo ya tofali tunafyatua tofali, kwa hiyo, haiwezekani kupata tofali la duara kwenye fyatulio la mstatili. Je, mtaala huu tunaouandaa au mtaala tunaoutumia unatutengenezea watoto wa namna gani kesho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini sana kwenye *educated labour force*, naamini sana na mpaka hivi sasa ninavyoongea naamini sana kwenye elimu kwamba ndicho kitu pekee kitakachomsaidia Mtanzania kutoka kwenye umaskini na kupeleka Taifa lake mbele.

Mtu yeyote asitudanganye tukapuuza elimu. Hata kama mimi sikubahatika kuipata huko utotoni, lakini bado elimu inabaki kitu cha kwanza na cha msingi kwa maendele ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnatumia fedha nyingi sana kusomesha watoto ili mtengeneze watoto ambao watakuwa faida kwa Taifa, familia na ulimwengu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Prof. Mkenda nataka utimize jukumu na wataalamu wote ulionao kututengenezea watoto wenye akili watakaoshindana kwenye ulimwengu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo matano tu ya kusema. Huo ndiyo utakaokuwa ushauri na mchango wangu kwa siku ya leo kwa Mheshimiwa Prof. Mkenda na Taifa zima. Tufanye nini ili tuweze kuboresha elimu ya Taifa letu? Mambo haya nimeyaandaa katika mfumo wa herufi tano ili iwe rahisi kwangu mimi kukumbuka na wanaonisikiliza kukumbuka. Herufi hizi tano zinamaanisha neno "*Change*", *C, H, A, N, G, E*.

Mheshimiwa Spika, *C – curriculum* (Mtaala). Nampongeza sana Mheshimiwa Prof. Mkenda, amefanya jambo jema sana kushughulika na kubadilisha mtaala wetu. Mara ya mwisho nilipozungumza hapa niligombana kuhusu mtaala, nikasema mtaala huu unatuchelewesha kwenda mbele. Hivyo amechukua hatua na amebadilisha mtaala. Nimeusoma, nimeuona umezingatia mambo yote ya msingi. Anawaandaa watoto wetu kuweza kutimiza majukumu yao. Mtaala huu ninauunga mkono ukatekelezeke ili uweze kuboresha elimu ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani mtaala ambao utabadilisha *mindset* za watoto, natamani mtaala utakaowafundisha watoto wetu *values* za nchi yao, natamani mtaala ambao utafanya watoto wetu wawe *practical* zaidi badala ya *theories*. Huko nyuma tulikuwa ni watu wa nadharia nyingi sana kuliko vitendo, lakini mtaala huu unatengeneza watoto ambao watakuwa suluhisho la matatizo ya Taifa letu. Nakupongeza Mheshimiwa Prof. Mkenda na timu nzima ya wataalam walioandaa. Hiyo ni *C*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *H - happy motivated teachers*. Tunahitaji walimu waliokuwa *motivated*, walimu ambao hawana hofu ya kesho. Hata kama una mtaala bora kiasi gani, bila walimu bora hakuna utakachofanikiwa. Walimu wetu mazingira yao ni magumu, kwa hiyo, natamani walimu walipwe vizuri, natamani walimu waishi mahali pazuri ili watamani kufundisha watoto wetu. Mwalimu ambaye anaendesha bodaboda hawezi kufundisha mtoto wangu. Maisha yao ni duni, hivyo tuboreshe maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *A – availability* ya *educational infrastructure*. Naipongeza sana Serikali yangu kwa madarasa mengi yaliyojengwa, lakini madarasa bila walimu haitasaidia chochote. Kwa hiyo, naomba tuendelee kuboresha miundombinu ya elimu katika nchi yetu ili mwisho wa siku watoto wetu wasikae chini, wasome kwenye madarasa mazuri na hivyo waweze kuwaelewa walimu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *N – navigating from using Kiswahili* kama *medium of instruction*. Siku zote nimesema, mimi sikubaliani sana na kufundisha kwa Kiswahili na ninarudia leo tena hapa ndani, nikizungumza huwa nabishiwa, naomba tuwafundishe watoto wetu kwa lugha ambayo imeficha maarifa ya dunia. Maarifa mengi yamefichwa kwenye Kiingereza, tuwafundisheni watoto wetu kwa *English.* Wazazi wengi hapa tunawafundisha watoto wetu *international schools*. Naomba sana tulifikirie suala hili, tuwafundishe kwa Kiingereza, wazungumze Kiswahili nyumbani na popote walipokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipe nafasi nimalizie. Nimemaliza 'N' na sasa nakuja *G – go do research*. Naomba tuwekeze sana fedha nyingi kwenye ufanyaji utafiti. Nchi hii haifanyi utafiti wa kutosha, kwa hiyo, tuweke fedha nyingi kwenye utafiti. *World Bank* imesema bajeti ya utafiti inatakiwa *2.7 percent* ya *GDP,* lakini kwetu sisi ni *0.5 percent* ya *GDP*. Ni fedha kidogo mno kufanyia utafiti. Kwa hiyo, tuwekeze kwenye utafiti wa elimu ili tujue matatizo yetu na jinsi ya kuyatatua na ili tuweze kuiona kesho itakuwaje kwa watafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti usifanyike tu kwa ajili ya kutimiza masharti ya kupata *degree* shuleni, hapana. Utafiti ufanyike kila siku, fedha zitumike kwenye utafiti ili kuwawezesha wataalamu wetu kugundua matatizo yetu na jinsi ya kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni *E - engage parents*. Tusiwaache wazazi pembeni. Wazazi watimize wajibu wao. Wazazi tusiwaachie walimu watoto wetu, wazazi wa nchi hii tumekuwa wavivu, hatusimamii watoto. Mzazi zima *TV* nyumbani mpe mtoto kitabu asome. Mtoto akilia kidogo anapewa simu acheze *game* ili asipige kelele. Nawaomba wazazi washiriki kutimiza wajibu wao kushirikiana na Serikali ili tuweze kutengeneza watoto bora. Kama wazazi tukikaa pembeni hata siku moja hatutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nikielekea mwisho ni bajeti, *UNESCO.* Wamesema bajeti ya elimu katika nchi yoyote haitakiwi kupungua *twenty percent* ya bajeti nzima. Bajeti hii ambayo Mheshimiwa Prof. Mkenda anataka kupitisha ni shilingi trilioni 1.9 ambayo ikizidi sana, haiwezi kuzidi *three percent* ya bajeti yetu ya mwaka mzima ya *forty-nine trillion.* Hiyo haitoshi.

Mheshimiwa Spika, tuwekeze kwenye elimu. Tukubali ku-*invest* kwenye *education* kwa sababu bila kuwekeza kwenye elimu hatuwezi kupata mafanikio. Naomba kuunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, na Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa ajiandae.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii ya kuchangia jioni hii ya leo. Awali ya yote naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima na uhai kwangu binafsi, pia na Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani ukiwemo pia na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo utajikita zaidi kwenye kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa mambo makubwa

ambayo imeyafanya kwa kundi la watu wenye ulemavu, nikiwa kama Mbunge wa kundi hili. Naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo imeendelea kuleta mageuzi kwenye elimu ya kundi hili la watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ya kuishukuru Serikali, lakini kwa masilahi ya muda, nimekuwa nayo machache hapa ambayo kwa kweli yamekuwa ni mageuzi makubwa sana kwa kundi hili la watu wenye ulemavu. Naishukuru Serikali kwa kuanzisha shule za nyumbani. Kwa nini naishukuru Serikali kwa ajili ya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa sababu watoto wengi wenye ulemavu uliozidi walikuwa wanashindwa kupata haki yao ya elimu kwa kushindwa kwenda shuleni. Kwa hiyo, uwepo wa miongozo ya shule za nyumbani unawawezesha watoto hawa kuweza kupata haki yao ya elimu. Walimu wanawafuata nyumbani wanawafundisha na hatimaye wanatungiwa mtihani, wanafanya kama watoto wengine. Haya ni mageuzi makubwa sana kwa Elimu ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishukuru Serikali kwa kuwa imeendelea kutenga fedha za kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, lakini pia kununua vifaa visaidizi kwa kundi hili la wanafunzi wenye ulemavu. Hii ni hatua kubwa sana. Kama tunavyofahamu na kama ambavyo nimekuwa nikisema mara nyingi, kwamba suala la vifaa visaidizi kwa kundi la watu wenye ulemavu ni kama chakula, yaani mtu hasemi kwamba alikula jana leo asile. Vifaa hivi ni muhimu sana, kwa sababu anapokuwa nacho leo, kesho kinaharibika, kinahitajika kingine. Kwa hiyo, ni kama chakula kwa vifaa visaidizi kwa watu wenye ulemavu. Naishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutenga fedha na kununua vifaa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishukuru sana Serikali kwa kuendelea kufanya upimaji wa usikivu kwa kundi la wanafunzi viziwi; na baada ya kufanya upimaji huu, Serikali pia imekuwa

ikitoa vifaa vya kuwasaidia kwenye eneo hili la usikivu *(hearing aids)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu wenzetu viziwi, yaani huwezi tu kununua kifaa ukampatia. Sasa hatua hii ambayo imechukuliwa na Serikali ya kuwapima kwanza na kuona ni kwa jinsi gani wameathirika na kuwapatia hivi vifaa ni hatua kubwa sana. Kwa hiyo, naishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa hatua hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali kwa kuongeza vyuo vya kudahili walimu wa elimu maalum. Kama tunavyofahamu, kumekuwa kuna upungufu wa walimu wa elimu maalum, hivyo Serikali imeongeza Chuo cha Kabanga na Chuo cha Mpwapwa ili viweze kuongeza udahili wa walimu hawa. Kwa hiyo, hii ninaamini kwamba inaenda kupunguza hii changamoto ya kuwa na upungufu wa walimu wa elimu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee tena kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuwa imekuwa ikifanya mafunzo kwa walimu wa elimu maalum lakini pia na walezi wa mabweni. Kama tunavyofahamu kwamba walimu wa elimu maalum wapo wachache, kwa hiyo, kwa kadiri ambavyo wanaendelea kupewa mafunzo ya mara kwa mara, pia na hawa walezi wa mabweni wanavyoendelea kupewa mafunzo ya mara kwa mara inawaweka kwenye nafasi nzuri ya kuliangalia kundi hili na kuwasaidia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kushukuru na kupongeza ni kuomba tena. Yapo mambo kadhaa ambayo nimekuwa nikiishauri na kuiomba Serikali kwa kundi hili la watu wenye ulemavu na ninaomba niyakumbushe tena siku ya leo. Pamoja na kwamba Serikali imeweka huu mkakati mzuri wa kuongeza chuo cha Kabanga na Mpwapwa ili kuweza kudahili walimu wa elimu maalum, ushauri wangu ambao nimekuwa nikiutoa kwa Serikali ni kwamba, ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kwamba hii elimu maalum iwe ni lazima kwa kila mwalimu anayesomea ualimu?

Mheshimiwa Spika, kwa nini? Ni kwa sababu kila mwalimu akifahamu elimu maalum, mtoto huyu mwenye ulemavu anaweza akasoma kwenye eneo lake, tofauti na ilivyo sasa hivi ambapo mtoto mwenye ulemavu ambaye anahitaji mwalimu ambaye amesoma elimu maalum inamlazimu mpaka aende kwenye shule jumuishi, ama inamlazimu mpaka aende kwenye zile shule zetu maalum. Hii inaleta changamoto kwa sababu kuna maeneo ambayo shule ipo karibu, lakini hakuna walimu ambao wanafahamu elimu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuwafanya walimu wote kujifunza elimu maalum, itasaidia kila mtoto asome kwenye mazingira aliyopo badala ya kumpeleka kwenye elimu jumuishi. Unakuta kwenye ile elimu jumuishi hakuna bweni na hakuna miundombinu ya kumwezesha kufanya vizuri kwenye masomo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiliona hili, kila mwalimu akajua *A, B, C* akajifunza elimu maalum na elimu hiyo ikawa ni kitu cha lazima, basi tutaondoa kwanza hata hii changamoto ya ukosefu wa walimu wa elimu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati Bunge lililopita zilitangazwa nafasi za walimu wa elimu maalum, zilikuwa nafasi kama 400 kama sijasahau ama kama ninakumbuka vizuri, lakini walimu hawa walikosekana, wakapatikana walimu 200 tu. Kwa hiyo, sio walimu wengi wanasoma hii elimu maalum. Naomba sana Serikali iweze kuliona hilo na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ushauri wangu mwingine, nilikuwa naiomba Serikali, pamoja na kwamba Serikali sasa hivi inakalimani vitabu vya masomo kwa lugha ya alama, lakini pia iweze kuona ni kwa jinsi gani kila mwanafunzi anajifunza. Yaani hii lugha ya alama iwe ni somo la lazima kwa kila mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumechelewa, lakini tutatengeneza kizazi kijacho ambacho kitakuwa kina uwezo wa kuwasiliana na wenzetu viziwi. Hapa hatutakuwa tena na changamoto ya wakalimani, hatutakuwa tena na changamoto

ya walimu. Kwa hiyo, Serikali iweze kuona ni kwa jinsi gani hii lugha ya alama ikawa ni somo la lazima kwa kila mwanafunzi ili tutengeneze kizazi kijacho ambacho kitaweza kuwasiliana na wenzetu viziwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa kutenga fedha na kununua vifaa visaidizi kwa kundi hili la watu wenye ulemavu. Naiomba Serikali, mwitikio wa wazazi na jamii yetu kwa ujumla kwa habari ya elimu kwa watu wenye ulemavu sasa hivi umekuwa ni mkubwa sana. Hivyo vifaa hivi vinakuwa havitoshi. Naiomba Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivi visaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba niishauri Serikali kwenye eneo la uanzishaji wa chombo maalum cha kuratibu na kusimamia elimu jumuishi nchini. Sasa hivi hakuna chombo hiki, lakini kwa nchi nyingine, naomba nisizitaje, kuna nchi ambazo tayari zimeshaanzisha hivi vyombo na vinafanya vizuri. Hii elimu jumuishi inaratibiwa vizuri na inasimamiwa vizuri, uwepo wa chombo hiki utasaidia sana kuhakikisha kwamba hii elimu jumuishi inaratibiwa vizuri na inatekelezwa vizuri kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, na Mheshimiwa Anastazia Wambura ajiandae.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, ukiongea karibu na mwishoni unakuta mengi yamesemwa, lakini naomba niruhusu niseme yale ambayo hayakusemwa. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Prof. Adolf Mkenda, kwa hotuba nzuri na iliyosheheni matokeo chanya ya utekelezaji wa sera na mikakati ya kuboresha elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye wakiwa wamekaa pamoja na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, wanaonekana kama Mapadri ambao wanatoa amani ya roho, *I mean* amani ya moyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaipongeza Wizara na Serikali kwa mambo mawili makubwa ya kimapinduzi yaliyofanywa kwenye Sekta ya Elimu katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapongeza jinsi Wizara na Taasisi zake zilivyosimamia na kuongoza mchakato mgumu wa kubadili mitaala ya elimu. Huu ni mchakato mgumu wenye siasa kali katika nchi yoyote. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kushirikisha makundi mengi iwezekanavyo na maoni mengi na kupata maoni mengi iwezekanavyo. Kwa kweli niseme hakuna anayeweza kusema hakupata nafasi ya kusema, ya kushauri au hata wale wa kubeza. Kwa hiyo, tunaweza kusema sasa tuna mtaala mzuri kuliko tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kulichukulia kwa umuhimu mkubwa suala la tafiti na machapisho katika Chuo vyetu Vikuu. Utafiti na machapisho ndiyo uhai na sifa ya Chuo Kikuu chochote. Nampongeza kwa kutenga fedha za kuwafadhili wanataaluma wetu waweze kufanya tafiti na kutoa machapisho. Hii naona imeanza kuchochea utamaduni wa kutafiti na kuchapisha. *Of course,* ninajua fedha haitoshi, lakini nilisemea sana hili kuhusu kuwekeza katika *research and development.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kuchangia masuala mawili; moja, limeongelewa nami nimesifia kuhusu kuwa na mitaala mipya katika matokeo ya watoto wetu *(education outcomes)*. Maana mitaala ni mizuri kama wengi walionitangulia walivyosema. Mitaala ikiwa peke yake haiwezi kuleta matokeo chanya au mapinduzi tunayotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuongelea kuhusu kuhuisha Vyuo vyetu Vikuu na kuvifanya viwe shindani Kimataifa. Naomba nianze na la kwanza; kwa sisi tuliozaliwa vijijini, shule na jengo la shule zuri ndiyo ilikuwa alama ya mafanikio, ustaarabu na utaifa. Pengine shule ilikuwa na majengo mazuri kuliko hata nyumba zetu. Kwa hiyo, ukienda shule ndiyo unayajua mengi, unayajua ya nchi nzima na kuanzia *Middle School* na Sekondari, kwa sisi wa zamani ilikuwa inatukutanisha na makabila mbalimbali na wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali. Kwa hiyo, shule iliakisi Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii katika hizi zama za teknolojia, habari na mawasiliano vimeifanya shule kuwa ni dunia ndani ya shule. *As they say, world in a classroom, you bring the world in a classroom through the use of technology*. Kwa hiyo, hii mitaala mipya inayochochea kujifunza, ubunifu na kujiajiri, itafanikiwa tu endapo tutafungamanisha *(integrate)* mabadiliko haya ya mitaala na uwekezaji mkubwa ambao Serikali imeufanya kwa kusambaza umeme vijijini, kusambaza mkongo wa Taifa na kusambaza minara ya mawasiliano. Kwa hiyo, mifumo hii lazima isomane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miundombinu hii na uwekezaji huu utatusaidia sasa kuwezesha mtoto aliyepo Kagera afundishwe na mwalimu aliyepo Katavi au aliyepo Marekani kwa njia ya mtandao wa *E-education*. Kwa hiyo, tunavyowekeza lazima tuangalie hii inachangia vipi katika elimu? Maana yake inakuwa kama wakati mwingine tunafanya mambo kwenye *in silos*.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kama tunavyoona katika sekta ya afya, matumizi ya *mobile clinics (E-health)* au wanaita *M-health;* Daktari yupo India, lakini anafanya opereshini hapa Dar es Salaam. Kwa hiyo, hii itawafanya watoto wetu waanze kushuhudia dunia ndani ya darasa na huko ndiyo kujenga kizazi cha utandawazi na mapinduzi ya nne ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimesema nitaongelea kuhusu jinsi ya Vyuo Vikuu vyetu vinavyopimwa kuangalia pamoja na mambo

mengine kiasi gani Chuo kinaileta pamoja dunia *(Internationalization)*. Jana tulimsikia Mheshimiwa Jesca Msambatavangu akijaribu kupata tasfiri halisi ya *Internationalization,* lakini muhimu ni kwamba, vyuo vyetu lazima virudishe ule utaratibu ambao ulikuwa unaruhusu hii wanaita *multicultural exchanges* ya *faculties,* siyo wanafunzi tu, lakini ya *faculties. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimepata bahati ya kualikwa kwenye *Chuo cha George Washington University* kama *scholar*, lakini *practitioner in residence,* na hii ilikuwa ni kutumia kuwapa uzoefu/ujuzi ulionao, na walifaidika sana. Maana yake ilikuwa niende miezi mitatu, nikakaa miaka minne kwa kuwa kulikuwa na *demand* kubwa. Kwa hiyo, mimi nataka tuwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme kuhusu umuhimu wa kutumia wana-*Diaspora*. Tumekuwa tukiangalia Wanadaispora katika *remittances,* lakini tuangalie namna ya kuwatumia wana-*Diaspora* katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru nilimwona Mheshimiwa Waziri huko Mwanga akizindua maktaba ya mwanafunzi wa kidato cha pili ambaye yupo Rwanda, lakini ameanzisha maktaba ya jamii. Huyo ni mwana-*Diaspora* na ndiyo tunataka ushiriki wa *Diaspora* wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hiyo ninaomba watumie pia Balozi zetu kwa kuanzisha vitengo vya *International Cooperation* (Mahusiano ya Kimataifa). Najua ndani ya Chuo Kikuu kitengo hicho kipo, lakini kipo kwa jina, hawatuchokozi mpaka mabalozi. Mimi nilivyokuwa ninawasiliana nao, nauliza vipi wangetaka ushirikiano upi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba watumie sana hiyo programu ya ushirikiano wa Kimatifa kuweza kuleta hizo *exchange programs,* lakini kwa walimu wanajua *capstone courses,* wanafunzi wanakuwa na kiu huko nje kuja kufanyia hizo *capstone courses* hapa. Kwa hiyo, tuwawekee mazingira wezeshi, siyo vikwazo kupata vibali vya kazi, vya makazi na wakati wa

*summer* wengi hupenda kuja kwenye nchi hii na kukaa kwenye vyuo na wengine ambao wapo *Sabbatical Leave*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuwawezeshe ili vyuo vyetu viwe *Internationalized*, maana yake mtu ambaye hatoki, kama tunavyosema kwetu, mtoto ambaye hatoki anasema mama yake tu ndio anajua kupika, mpaka anapotoka. Pia tukitumia mbinu hii tutavipa vyuo vyetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja…

**SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Sawa.

Mheshimiwa Spika, tukitumia mbinu hii, tutavipa vyuo vyetu uhai mpya na kuvijengea ushindani katika Bara la Afrika na ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika hizo sekunde 30, ni kuhusu ushiriki wa sekta binafsi kwenye kuboresha na kukuza viwango vyetu vya elimu, siyo kuanzisha shule na kuendesha shule, lakini kuanzisha. Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize, suala la *endowment fund*, kwa kweli na hiyo anayosema tafiti na machapisho na kuweza kuwa na elimu bora bila *endowment fund* itakuwa ngumu na ushiriki wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, atafuatiwa Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nitakuwa na maneno

machache ya utangulizi mafupi tu. La kwanza, mjadala wa tangu jana tunaouhitimisha sasa, umekuwa wa kusisimua. Nimepata wakati mgumu sana kujiandaa kuchangia. Mheshimiwa Prof. Mkenda, aliponikuta hapa akawa anasema, wewe unaandika *thesis* ya *Ph.D!* Maana yake tangu asubuhi aliona ninajiandaa ninaandika. Nilikuwa ninaandika ninafuta kadri wachangiaji wanavyoendelea kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kiashiria cha nini? Ni kiashiria cha kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imethubutu kufanya mabadiliko ambayo sasa katika mjadala wetu baadhi yetu tumepata hofu, baadhi yetu tuna matarajio makubwa, baadhi yetu tuna wasiwasi na baadhi yetu tuna matumaini makubwa kwamba nchi yetu sasa inaelekea pazuri. Hiyo ndio hoja yangu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili, nitumie muda mfupi kuwakumbuka na kuwaenzi viongozi wetu wawili, Hayati Mwalimu, Julius Kambarage Nyerere na Hayati Ali Hassan Mwinyi, kwa kuweka msingi mzuri sana na imara wa elimu hii tunayotaka kuiboresha. Sitaki kurejea mchango wa Mheshimiwa Prof. Kabudi na Mheshimiwa Prof. Muhongo, mimi ni Mwanataaluma na taaluma ni kama jeshi; Profesa ni kama *General,* kwa hiyo, unatii tu, lakini unatakiwa kudadisi pia na kukosoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imewekea hoja mezani hapa kwamba, tumetoka mbali na tumepata mafanikio makubwa, lakini hapa tulipo haparidhishi, lakini siyo pabaya na kwamba, tunapoelekea ni parefu zaidi, pengine ni pagumu zaidi. Kwa hiyo, Serikali isichoke kusikiliza maoni na michango ya Watanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa alitangaza vita na akasema maadui tunaopambana nao ni watatu; ujinga, maradhi na umaskini, na akaongeza kwamba, nchi yetu bado watu wake ni maskini na ili kuwakomboa watu hao maskini ni muhimu kuwapa watoto wao elimu kama nyenzo ya ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hayati Ali Hassan Mwinyi, Mungu amrehemu akasema maneno haya haya, lakini kwa namna tofauti, ninamnukuu, alisema hivi: "Umaskini na uchafuzi wa mazingira ni watoto mapacha na mama yao ni ujinga." Kwa hiyo, sasa hivi tunajadili namna ya kutokomeza ujinga unaozaa umaskini na pia unaosababisha matatizo mengi sana kama maradhi na uchafuzi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kutumia maneno haya ya utangulizi kwa kirefu kidogo, kwa sababu wachangiaji wa tangu jana na leo kwa kweli ni kama wamenifilisi. Hata hivyo, naomba nichangie maeneo mawili. Jana ulituongoza hapa kwamba, kwa sababu hii ni Wizara ya Elimu na tunatumia Kiswahili, basi tutumie Kiswahili fasaha. Nitakuomba uniuwie radhi nikichemka, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Spika, jirani yangu hayupo hapa, lakini jana alizua mjadala mzuri sana kuhusu *Internationalization* na akaitafsiri kwamba ni umataifishaji wa elimu yetu. Mheshimiwa Prof. Kabudi, akaongeza akasema, umataifashaji wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mkurugenzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tulikuwa tunatumia umataifishaji na katika lugha neno likitumika mara nyingi hata kama lina ukakasi linakubalika. Tumetumia neno makinikia, limepita tu, kwa sababu ya namna lilivyotumika kuchakachua na mambo mengine kama hayo. Sasa hoja ni hii, tunataka vyuo vyetu vikuu viwe na hadhi ya kimataifa, vitambuliwe kimataifa Mtaala mpya ni moja ya nyenzo ya kuelekea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba ili tuelekee huko itabidi Bunge hili liishauri Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, hasa maeneo ya usimamizi wa rasilimali katika taasisi nyeti na za kimkakati kama Vyuo Vikuu vya Umma. Sheria hiyo ikibadilishwa itavipa uwezo na mamlaka chini ya uongozi wa Serikali kuajiri, kufanya tathmini ya utendaji wa Watumishi wake na hasa Wahadhiri kupandisha vyeo, kusimamia nidhamu pamoja na kupima utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa hivi, kwa sheria tuliyonayo na utaratibu tulionao, vyuo vyetu ni kama Idara za Serikali. Siyo taasisi nyeti na za kimkakati zenye mazingira maalum na mahitaji maalum na nitatoa mfano. Nilipotoka Chuo Kikuu mwaka 2018, nilimwacha mwenzangu amepandishwa cheo kutoka Mhadhiri kuwa Mhadhiri Mwandamizi, nilitoka akiwa amepewa barua na chuo kilichomtambua, kwa sababu unapanda cheo kama Mhadhiri kwa kigezo cha machapisho pamoja na uzoefu wa miaka mitatu. Alikidhi hicho kigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu kikampa barua ya kutambua cheo chake, kikapeleka Utumishi kwa ajili ya kibali. Kibali chake kilitoka mwaka 2021 baada ya miaka mitatu. Baada ya miaka mitatu! Huku kakaa miaka mitatu kupata cheo hicho kwa vigezo na mwongozo wa chuo, lakini kibali cha kutambua cheo hicho kikatoka baada ya miaka mitatu. Kwa hiyo, akapata mshahara wa cheo alichokipata baada ya miaka mitatu na akakaa miaka mitatu analipwa mshahara wa cheo cha zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati utumishi wanatoa kibali mwaka 2021, alikuwa pia ametimiza vigezo kupanda nafasi ya kuwa Profesa Mshiriki. Kwa hiyo, kibali kinakuja wakati yeye amepanda vyeo hivi viwili, na ndipo alipoanza kupata mshahara huo. Tangu 2021, mpaka leo ninapozungumza, kibali cha kutambua Uprofesa wake Mshiriki, hakijatoka. Hii maana yake nini? Tunataka vyuo vyetu viwe vya kimataifa kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu hapo zinatueleza kwamba tuna uhaba wa Maprofesa na Maprofesa Washiriki. Ukienda kwenye mfumo wa utumishi, huyu Profesa Mshiriki anatambuliwa kama Mhadhiri Mwandamizi. Kwa hiyo, *data* ya Mheshimiwa Prof. Ndakidemi sijui ulikuwa unasoma ya utumishi au ya vyuoni? Alikuwa anasoma ya vyuoni, hili ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza inavunja moyo kwa sababu, kuchapisha ni kazi ngumu sana, ni ghali, na wakati mwingine gharama hizo zinatoka mfukoni mwa anayechapisha kwa sababu ya uhaba wa rasilimali, lakini sherehe kubwa katika vyuo vikuu ni mtu anapopanda nafasi baada ya kuchapisha. Kimataifa

tunatambuliwa kwa kuwa na machapisho yenye hadhi. Hii inatakiwa ibadilishwe, kama kweli shinikizo lililopo la kuvifanya vyuo vyetu viwe vya kimataifa litashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yapo matatizo ndani ya vyuo, lakini hata wakiyarekebisha, vipo vikwazo ndani ya utumishi. Mimi nina taarifa (nina wasiwasi na muda) kwamba, Msajili wa Hazina ameshatoa Waraka Namba Moja tangu mwaka jana 2023 Mwezi wa Nane, akijaribu kuainisha alichokiita mashirika na taasisi nyeti zinazohitaji uhuru wa kuendesha na kujiendesha na hasa uhuru wa kusimamia rasilimali watu. Huu waraka hautekelezeki mpaka Sheria ya Utumishi wa Umma ibadilishwe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, nakuomba sekunde chache.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho nataka kukizungumzia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kwa kweli naweza kukiita ni fahari ya Tanzania. Pamoja na matatizo mengi, Mheshimiwa Spika huruhusiwi kupiga makofi, lakini naona tabasamu linaashiria hivyo. Hapo ninajaribu kukuhonga uniongezee muda kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo kimezaa Chuo Kikuu cha Sokoine, kimezaa Chuo Kikuu cha Ardhi, kimezaa Chuo Kikuu cha Muhimbili, kinavilea Vyuo Vikuu Vishiriki vya *DUCE* na *MUCE*, lakini ndiyo roho ya vyuo vikuu vyote vya binafsi. Chuo hiki pia kimesaidia kuanzishwa kwa Chuo Kikuu kikubwa sana hapa nchini, cha Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki chuo kwa sasa ninavyoongea kina Shahada za Uzamivu *(Ph.D)* 1,000 na ukishafikia idadi hii kimataifa wewe unapewa hadhi ya Chuo cha Kitafiti *(Research University)*. Pia, kwa mwaka chuo hiki kinazalisha Shahada za Uzamivu 100 kwa wastani. Sasa sitaki kuzungumza juu ya mazao ya chuo hiki kwa sababu, nitaonekana pengine ninatia chumvi, lakini

aliyekalia kiti anatambuliwa kimataifa na ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa alikuwa ameomba dakika moja.

**MHE. BALOZI. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ukimtaja Mheshimiwa Prof. Muhongo hapa tunamtambua kama Mbunge, lakini ni mtafiti, ni Profesa mwenye heshima kimataifa. Mheshimiwa Rais Yoweri Museveni wa Uganda ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hayati, John Garang wa Sudani ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hayati Rais Magufuli ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hayati Maalim Seif ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni mmoja wa wanafunzi kutoka Idara niliyokuwa mimi ya siasa aliyefanya vizuri na rekodi yake iko hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani nitakuwa nakuvunjia heshima ulivyonivumilia. Nakushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hii ni moja kati ya hotuba za Waziri ambayo nilikusudiwa niwe nimekaa kule halafu nitoe mchango wangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Anastazia Wambura, atafutiwa na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid na Mheshimiwa Juma Kipanga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu. Kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi yake ya uhai, lakini vile vile kwa kutujalia sote afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile Mhehimiwa Dkt. Philip Isdori

Mpango, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu wake, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kazi nzuri ya kuliletea Taifa letu maendeleo katika nyanja mbalimbali. Nadhani sote ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nampongeza sana Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Naibu wake maarufu QS Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye ni Naibu Waziri. Vilevile Katibu Mkuu Prof. Caroline Nombo, Manaibu Makatibu Wakuu; Dkt. Jasson na Prof. Mdoe, pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya hasa kwa upande wa kuboresha miundombinu ya elimu na kwa maboresho ya sera ambayo wasemaji wengi wanaizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na mengi sana ya kuzungumza kwa sababu, tumeyazungumza katika Kamati. Mimi ni mjumbe mmojawapo wa Kamati hii ya Elimu na tunaiamini Serikali kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametueleza mipango mingi ya Wizara. Pia tuna imani kwa sababu ya kazi nzuri ambayo tayari imeshafanyika. Kwa hiyo, tunajua kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nitakalolizungumza ni kwa sababu ni suala ambalo ni mtambuka na Serikali nzima ipo hapa. Kwa hiyo, napenda nilizungumze na baadaye kama muda utaruhusu nitaongea masuala ambayo ni *specific* kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa tafsiri ya elimu. Elimu inatafsiriwa kama njia ya kutengeneza nguvukazi yenye ujuzi ambayo inasababisha ukuaji wa uchumi na uvumbuzi. Kwa maana hiyo, madhumuni ya elimu katika jamii ni kupata ufahamu na ujuzi ambao utawaandaa watu kuendesha maisha yenye tija na utoshelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu walitutengeneza. Miaka iliyopita walitutengeneza Watanzania au Waafrika tuwe ni watu wa kuzalisha malighafi na kuziuza kwa bei ya chini ambayo wenzetu hao wanaipanga wao wenyewe, lakini pia sisi tununue bidhaa

ambazo zinatokana na hiyo malighafi kwa bei ya juu ambayo pia, wanaipanga wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani sana tutoke hapa tulipo kwa kutumia elimu ambayo sasa hivi tunakwenda kuitekeleza, ambayo ni elimu ya amali. Ninaamini kabisa kila mmoja wetu hapa anatamani tutoke tulipo ingawa tumefungwa kwenye minyororo, lakini inabidi sisi Watanzania wenyewe tujitoe kwenye hiyo minyororo na hata ikibidi kushirikiana na wenzetu kutoka nje, ili kusudi tuweze kuimarisha uchumi wetu kutokana na hii elimu ambayo tunaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri kitu. Kutokana na kwamba, tuna wabunifu wengi katika nchi yetu ambao wanaweza wakatusaidia kukuza uchumi wetu, lakini pia tuna elimu ya amali ambayo tumeanza kuitekeleza mwaka huu 2024.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kwanza ni Serikali ikutane na wabunifu, iangalie changamoto walizonazo, ione mahitaji waliyonayo kwa kuelezwa na wabunifu wao wenyewe na kinachofuata iwawezeshe wabunifu kutekeleza au kubidhaisha bunifu zao. Ninalisema hili kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tumeona, mwaka hadi mwaka tunapata wabunifu au wavumbuzi wanaobuni vitu vizuri sana. Kuna ambao wamebuni magari, kuna ambao wamebuni pikipiki za umeme, lakini hatujaona kama kuna maendeleo makubwa katika kubidhaisha huu ubunifu wao. Isitoshe wanapewa tuzo kila mwaka. Wengine wanavumbua mashine mbalimbali, lakini kinachotokea ukiwauliza, changamoto waliyonayo wanakwambia hatuna mitaji, hatuna fedha za kutatua baadhi ya changamoto ambazo zipo kwenye ubunifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iwawezeshe hawa wabunifu ili kusudi na sisi kama Taifa, tuweze kutengeneza bidhaa tuuze katika nchi yetu na pia tuweze kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linatokana na kwamba, kuna nchi ambazo tulikuwa tunashindana nazo kiuchumi, tulikuwa tunalingana nazo miaka ya hamsini na sitini iliyopita, lakini sasa hivi tunanunua bidhaa nyingi sana kutoka kwao. Kwa mfano, bajaji tunanunua kwa nchi za wenzetu ambao tulikuwa nao sawa kiuchumi na wakati huo hawakuweza kutengeneza bajaji wala baiskeli, lakini sasa tunanunua bajaji, tunanunua baiskeli, magari na mashine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wao wamefanya nini? Wanawasaidia wabunifu na wavumbuzi wao na inafikia mahali ambapo wanadiriki hata kununua kama ni magari ama mashine zenye gharama kubwa na kuwaletea wale wabunifu wana-*dismantle* na kuweza kutengeneza. Ndiyo maana utakuta mashine ile ile utaipata nchi fulani, au nchi fulani. Ni kutokana na haya ambayo wanayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali iwasaidie wabunifu wetu ili kusudi elimu hii iweze kutafsirika katika ukuaji wa uchumi wetu. Napenda Serikali iangalie inahitaji nini zaidi, kitu au bidhaa ambazo tunaziagiza sana kutoka nje na ambazo sisi kama Watanzania tunaweza kuzitengeneza, iwa-*task* hawa wenzetu, i-*task* hizi shule za amali, i-*task* vyuo, iwaambie inataka vitu gani ili kusudi waweze kuvitengeneza kwa kutoa vivutio. Ninaamini kabisa Watanzania tunaweza tukatengeneza bidhaa nyingi sana kwa kutumia malighafi zetu na tukaziuza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, nasema tu kwamba, itasaidia kuongeza ajira na kupunguza tatizo la ajira katika nchi yetu, hususan kwa vijana na pia itainua *per capita income*. Samahani nimetumia neno hilo, yaani itainua kipato cha mtu mmoja mmoja. Pia, itaongeza fedha za kigeni na itapunguza sana ununuaji wa bidhaa za nje, na kwa maana hiyo, tutakuwa na akiba nyingi ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwamba, tukifanya hivi ina maana kweli mbili zitakuwa hazipingani, nikiwa na maana kwamba, tafsiri halisi ya elimu pamoja na elimu ambayo tunai-*practice* au tunaitekeleza zitakuwa zinaenda sambamba. Hii ni

kutokana na alivyosema mtaalamu mmoja, Galileo Galilei, Muitaliano, yeye alisema, *"two truths cannot contradict one another."* Kwa hiyo, hizi ni kweli mbili ambazo tukizitekeleza kulingana na tafsiri ya elimu ninaamini kabisa tutakwenda vizuri na tutainua uchumi wa nchi yetu kutokana na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala la upungufu wa walimu, nimelisema hapa mara kadhaa kwamba Mkoa wetu wa Mtwara una upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi zaidi ya 60%. Naomba tupelekewe walimu katika mgao wa walimu maana tulishaahidiwa kwenye Kamati kwamba kuna ajira za walimu, Mheshimiwa Waziri asitusahau.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusiana na mikopo ya vyuo vikuu. Kamati imetoa ushauri kwamba, tuwe na *revolving fund,* maana naona Waheshimiwa Wabunge wengi waliosimama hapa wamelizungumzia hili suala. Watoto wetu wanateseka sana kiasi kwamba wanafikia mahali wanatamani waache vipindi waende kufanya kazi mitaani ili waweze kupata fedha, hususan wale madaktari wa mwaka wa tatu ambao wanalazimika kufanya *field practical,* hawa wanataka kazi angalau wapate zile fedha za kwenda kufanya *field practical* katika maeneo ya nje ya chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iliangalie hili. Hawa ni watoto wetu, wanateseka, wakiwemo wasichana na wavulana. Kwa kweli, ni hali ambayo inahuzunisha sana. Kwa hiyo, naomba sana *revolving fund,* fedha zinazorejeshwa ziwekewe uzio zisitoke, na tunaambiwa zipo zaidi ya shilingi trilioni moja ambazo zimeshawahi kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi tungekuwa tumezitunza ina maana tusingekuwa tunalazimika kuiomba Serikali kila mwaka itoe fedha, zingekuwa zinazunguka hizi hizi, hata kama Serikali inaongeza, basi ingekuwa ni kiasi kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni malalamiko ya walimu wanapostaafu, wanapata shida sana. Hawapewi fedha za kuhamisha mizigo yao kutoka nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kuliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kipanga, na Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi jioni hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata nafasi ya kuweza kuchangia walau mawili matatu katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza namshukuru na ninampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Prof. Mkenda Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, hali kadhalika Waziri wetu wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mheshimiwa Leyla Mohamed Mussa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye udhamini wa masomo ya nje ambao umeasisiwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Udhamini huu unawafanya watoto wasiopungua 600 wa Kitanzania kusoma bila kukopa. Naomba nimwambie Mheshimiwa Profesa Mkenda kwamba, ni lazima vigezo na masharti ya kujiunga na ufadhili huo vizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo vinatumika ni vigumu sana kwa wale watoto wanyonge wanaoanza shule za Serikali, ninyi wenzetu huku mnaita Shule za Kata, ambao wanapambana mpaka wakafika kidato cha sita na kuweza kupata *Division One* za kuanzia *point* tano, sita na saba, wengi wanatemwa na mfumo huu kiasi kwamba, wanakosa hii fursa ambayo Mheshimiwa Rais kwa nia nzuri kaiandaa. Nakuomba sana Mheshimiwa Profesa Mkenda vigezo hivi tuvibadilishe.

Mheshimiwa Spika, sisi kwa upande wa Zanzibar tuna shule mbili, ambapo kwa upande wa Unguja kuna Sekondari ya Lumumba na Pemba kuna Sekondari ya Fidel Castro. Hizi shule ndizo shule ambazo zinafanya vizuri sana kwenye mitihani yao. Hata mitihani iliyopita ya mwaka 2023 Shule ya Sekondari ya Fidel Castro ilikuwa na wanafunzi 48 waliopata *division one*, wakiwemo walio na *point* tano, sita na saba. Pia, Shule ya Sekondari ya Lumumba kwa upande wa Unguja, nayo ilikuwa na wanafunzi 67 ambao walipata *Division One*, wakiwemo wenye *point* tatu, nne, tano, sita na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, huu mfumo ambao mmeuweka, sijui ni kwa sababu gani unawatema na wanashindwa kupata fursa hii na matokeo yake wanajiunga kwenye vyuo vikuu kwa kupitia njia ya mkopo kama wanafunzi wengine ambao wamepata daraja la pili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba huu mfumo kaeni nao vizuri, hivi vigezo na masharti aidha vipunguzwe au mfumo uwekwe vizuri ili Watanzania walio wanyonge na yatima waweze kufaidika na hii fursa ambayo kwa nia safi Mheshimiwa Rais kaitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wa Pemba niseme kuna mwanafunzi anasoma katika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, mtu anayechangia yuko upande wako huku. Sijui kama ulimwona, umekatiza katikati yake. Mheshimiwa Rashid, endelea.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa upande wa Pemba tunao wanafunzi waliopata *point* tano, sita, na saba lakini mfumo haukuweza kuwachukua wakaweza kupata fursa hii. Kadhalika Lumumba wako wanafunzi walio na *point* nne, tano na sita nao wamekosa hii fursa.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Profesa na wataalamu wake, najua anao na wanasikiliza, hii fursa ni ya Watanzania Watanzania wote wanyonge na maskini, lakini kwa hivi ambavyo tunakwenda, Profesa lazima ufahamu kwamba fursa hii itatumiwa na wale wazazi ambao wana uwezo, waliosomesha watoto wao kwenye shule za *english medium* mpaka wakafika kidato cha sita ambapo naamini wewe mwenyewe Profesa unafahamu kwamba shule hizi mwanafunzi haingii kidato cha sita ikiwa ana wastani wa *average* 'A' ya kuanzia *point* sita.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, una *division one* ya *point* saba, lakini huingii kidato cha sita. Sasa hapa ndipo pale ambapo fursa hii inatumiwa na wale walio wengi. Wale wanyonge ambao wanasomeshwa na Serikali zetu hizi mbili bila malipo, wanaweza kukosa fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Baraza la Mitihani, nilipongeze, wanafanya kazi nzuri, nasi sote ni mashahidi, tunashuhudia kila mwaka ufaulu ukiongezeka lakini kuongezeka huku kwa ufaulu pia ni chachu ya mtendaji huyu na wenzake waliopita ambao wanafanya kazi vizuri katika kulisimamia hili Baraza pamoja na mitihani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sisi Zanzibar kwa maana ya Kisiwa cha Unguja, tunashukuru kwamba sasa Baraza la Mitihani wamejenga ofisi nzuri ya kisasa ambapo waratibu wale wa mikoa na wilaya sasa wamepunguziwa gharama zile za kuja kufuata shughuli za mitihani huku Tanzania Bara. Wana ofisi nzuri na ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunapozungumzia Zanzibar, ni Unguja na Pemba. Mara nyingi ukisema Zanzibar watu wanahisi ni Zanzibar tu, lakini Zanzibar ni Unguja na Pemba. Kwa hiyo, nasi kule Pemba tunahitaji uwepo wa ofisi ambayo itaenda sambamba na hii namna ya ufaulu ambao unaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, kingine naomba nimwulize Mheshimiwa Prof. Mkenda, katika kuchangia kwangu aweze kuja kunijibu hapo. Januari, 2020 katika jimbo langu kulifunguliwa skuli moja

kubwa ya sekondari ambapo Mgeni Rasmi alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Skuli ile ikaitwa jina la Samia Suluhu Hassan. Hadi nazungumza hapa na hadi matokeo ya kidato cha nne yaliyotoka 2023, bado jina la skuli lililotolewa na Mheshimiwa Rais halijatumika. Ukiangalia kwenye *records* zao wataikuta inaitwa Skuli ya Sekondari ya Muambe. Hivi Mheshimiwa Prof. Mkenda kubadilisha jina nako kunahitaji upewe bajeti na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu?

Mheshimiwa Spika, kubadilisha jina tu la shule kutoka *Muambe Secondary School* ukaipeleka kuwa *Dr. Samia Suluhu Hassan Secondary School,* kunahitaji bajeti? Hivi hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu akupatie fedha za kubadilisha jina? Mwaka huu ni wa nne, naomba sana kwenye mitihani ya mwka 2024, skuli hii yenye jina la kiongozi wetu wa nchi liweze kusomeka katika majina ya orodha ya skuli ambazo wanazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuwapongeze Wizara ya Elimu. Tulisema sana na tukaomba sana hapa namna ya kujengwa Chuo Kikuu Huria kule Pemba, tayari tunashukuru, ndani ya wiki hii mkandarasi anakwenda Pemba kukabidhiwa *site*. Tunashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Pia kuna Chuo cha Mwalimu Nyerere, chuo cha kisasa kimeshajengwa kule na ombi langu hapa, hiki chuo kimekamilika, kinachohitajika hapa, kipatiwe samani kwa maana ya *furniture*.

Mheshimiwa Spika, pia pale mahali chuo kilipo, lazima hapa Mheshimiwa Prof. Mkenda atenge bajeti ya kupata usafiri kwa ajili ya wanachuo. Hii itawasaidia sana wanafunzi kwa ajili ya dharura ambazo zitatokea, kadhalika na mahitaji madogo madogo yanayohitaji kutumia usafiri. *(Makofi)*

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, nakuheshimu sana na ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na wala sisubiri kengele. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa sana katika sekta ya elimu hasa katika Jimbo la Kilolo ambapo kuna Chuo cha *VETA* kinajengwa, shule ya wasichana ya mkoa na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii naomba kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo: Kwanza, kwa mara nyingine tena naomba kuendelea kushauri kuhusu umuhimu wa uwazi katika utoaji wa mikopo ya elimu ya juu. Uwazi ni pamoja na kutoa mrejesho, kwa nini mwombaji hajapata mkopo? Bado kumekuwa na malalamiko kwa wale wanaokosa na kudhani kwamba kuna upendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba shule za watu wenye mahitaji maalum ziangaliwe. Shule hizi zina upungufu mkubwa wa vifaa kulingana na mahitaji yao. Serikali ichukue hatua za makusudi kwa ajili ya shule hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya kuwaletea maendeleo Watanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara kwa kusimamia ipasavyo sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuanza kujenga shule za ufundi za sekondari. Hii ni hatua kubwa kwa mustakabali mpana kwa maendeleo ya nchi, na ili kufanikisha hili, ni lazima fedha zilizotengwa zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lingine, nashauri kuhusu maslahi kwa walimu wetu kwamba yaboreshwe na bila kusahau kuendelea kujenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa maendeleo yote yanayoendelea katika sekta ya elimu. Nina mchango mdogo tu, kama mtu ambaye nimetokea Wizara ya Mambo ya Nje na kwa kuzingatia nafasi ya Tanzania katika kupigania ukombozi wa Kusini mwa Afrika, nashauri kama sehemu ya kuendelea kujenga ushawishi katika ukanda wa *SADC,* Maziwa Makuu na ndani ya *EAC* kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje, tuje na kitu kinaitwa *education diplomacy*. Kwa mfano, kwa kutumia Bodi ya Mikopo, tunaweza kutenga 10% kwa ajili ya *education diplomacy* ambapo tunatoa *scholarship* kwa baadhi ya nchi ndani ya eneo letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tukiwa na programu ya kuchukua wanafunzi 100 kutoka Comoro kwa miaka kumi mfululizo, maana yake ni kuwa ndani ya miaka mitano utakuwa na wanafunzi 500, lakini tayari utakuwa na wanafunzi kama 200 ndani ya Comoro ambao wamehitimu Tanzania, kwa miaka kumi unaweza kuwa na idadi fulani ndani ya Serikali ya Comoro katika sekta binafsi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi kwa nchi kama DRC, Zambia, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Burundi, Sudani Kusini na kadhalika tutajenga ushawishi katika nchi hizo na hivyo kunufaika na watu ambao watakuwa na unasaba na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninaamini *economic diplomacy* inaweza kufanikiwa zaidi kwa kuunganisha nguvu mbalimbali iwe elimu, michezo, sanaa na kadhalika; ndiyo maana tutakuwa wenyeji wa *AFCON*, ni sehemu ya *sports diplomacy* kama sehemu ya *economic diplomacy*. Kwa hiyo, pamoja na *exchange program,* naamini Wizara ya Elimu inayo nafasi ya kushiriki *economic diplomacy* zaidi ya kuwaandaa wanafunzi wetu kupitia elimu, bali pia kupitia *education diplomacy*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kuboresha elimu katika Wizara ya Elimu. Pia nampongeza Waziri wa Elimu Profesa Adolf Mkenda na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 ulijielekeza katika kutekeleza maeneo ya kimkakati ikiwa ni kuongeza fursa na kuimarisha elimu ya ufundi nchini, kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu nchini, kuongeza wigo wa shule za ufundi, na kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga *campus* za vyuo zenye kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati ulienda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo: Serikali imeendelea kuimarisha mazingira, miundombinu ya kujifundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari katika kufikia azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo: imejenga shule ya mfano ya sekondari Dodoma eneo la Iyumbu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na imejenga upya vituo vinne kwa ajili ya utoaji elimu ya sekonadari nje ya mfumo rasmi katika Mkoa wa Rukwa - Sumbawanga, Iringa Mjini, Pwani - Kibaha, na Manyara - Babati.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imekarabati vituo vinne katika Mkoa wa Dar es Salaam, Makao Makuu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Morogoro Manispaa, na Ruvuma Songea. Miundombinu hiyo itaimarisha mazingira ya utoaji wa elimu ya ualimu na kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya walimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara ya Elimu na maendeleo kwa wanafunzi wetu. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri, Prof. Adolf Mkenda na Naibu Waziri na uongozi wake wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikitekeleza mkakati wa elimu jumuishi unaowaweka pamoja wanafunzi wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu. Lengo hasa la mkakati huo ni kuleta usawa na kuondoa unyanyapaa na ubaguzi kwa watoto wenye ulemavu ambao waliachwa nyuma kwa sababu ya imani potofu.

Mheshimiwa Spika, kuna uhaba wa fedha ya kukidhi mahitaji ya elimu jumuishi, unyanyapaa, miundombinu isiyo rafiki na kukosekana kwa malezi ya ziada kwa wanafunzi hao. 67% ya walimu wake walikiri shule zao kutokuwa na walimu waliobobea kufundisha wanafunzi wasioona, hivyo ni lazima Serikali iandae mazingira rafiki zaidi kwa watu hawa kupata elimu sawa na wanafunzi wengine ili kupunguza unyanyasaji.

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza changamoto za elimu jumuishi, utafiti huo unapendekeza wadau wote ikiwemo Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, walimu, wazazi au walezi kushiriki katika kuleta mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, mazingira magumu ya shule na vyuo vikuu hasa ukosefu wa mabweni husababisha wanafunzi wadogo kuanza maisha ya kujitegemea yasiyo na ulinzi wala huduma wezeshi katika kujikimu. Hii husababisha ngono za mapema, ukatili wa kijinsia na mimba zisizotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko la kupata mimba kwa wanafunzi wanaoishi *ghetto* na chanzo kikubwa cha mimba hizi ni kutolindwa kwa ma-*ghetto* yaliyozunguka chuo, na na kukosa mahitaji ya muhimu kutoka kwa wazee/walezi wao

ambao hawajui kinachoendelea kuwa wanafanya majukumu yote ya ndoa.

Mheshimiwa Spika, hilo *boom* haliwatoshi. Serikali ihakikishe kama wanalipia ada moja kwa moja vyuoni, basi na mabweni walipiwe moja kwa moja ili isiwape nafasi ya kutoka kwenda kupanga mazingira mengine yanayosababisha uharibifu wa tabia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kwamba vyuo vikuu vikabidhiwe majiji au halmashauri ili kukiwa na shida au changamoto yoyote, basi chuo hicho kinaweza kufanya tafiti kulingana na *issue* iliyopo na hiyo itafanya *impact* za vyuo zionekane *direct* kwa wananchi, na chuo kikuu kinakuwa ndiyo mlezi wa halmashauri au jiji. Hii itakuwa kama wafanyavyo Japan au Indonesia na inasaidia kuona chuo kiko karibu na jamii.

Mheshimiwa Spika, aidha, wanachuo waruhusiwe kufanya *exchange program* hata ndani ya vyuo vyetu, kwa mfano, kutoka *MUST* kwenda *UDOM* au *UDSM* kwenda Nelson Mandela na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wanajifunza na kubadilishana ujuzi mbalimbali, hivyo ku-*gain* jambo ambalo halipo kwenye *home university*.

Mheshimiwa Spika, pia vyuo vikuu vishiriki ambavyo vilitajwa katika kila mkoa vioneshe angalau maendeleo yao yamefika wapi. Mfano, *campus* ya Uhasibu Arusha na Songea hakuna kinachoendelea. Aidha, kuna maeneo kama Ruvuma, vyuo vikuu binafsi vyote vimekufa. Hivyo, naiomba Serikali itafute njia ya kukibeba chuo kama Peramiho, *RUHUWIKO* na *AJUCO* Songea wasaidiwe katika eneo ambalo wamekwama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *retirement age,* maprofesa na madaktari waendelee kufanya kazi kuanzia miaka 65 hadi 85 kwa kuwa kazi yao itakuwa zaidi ku-*mentor* na kuandika maandiko ya tafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi ya wahadhiri ni ndogo sana, vyuo vipewe *autonomy* ya kuajiri kutoka nchi mbalimbali ili kuweka maana ya *university*.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii ya Elimu. Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyopeleka fedha nyingi kwenye miradi ya elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwa kuweza kuanza mtaala mpya ndani ya shule zetu. Kwanza nianze na changamoto, kwani ndiyo zitajitokeza ili mweze kuzifanyia kazi. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kujikita mchango wangu kwenye maeneo yafuatayo: nikianza na ujenzi wa vyuo vya *VETA* vya Wilaya katika ukurasa wa 30, ni jambo zuri sana kujenga *VETA* kila Wilaya, na kwa hili naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna ilivyolisimamia hili kwa nguvu zote kwa kuhakikisha kuwa kila Wilaya inakuwa na *VETA*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia hii nzuri, bado nina swali kwa Wizara kuhusu namna gani wamejipanga kuwa na walimu, vifaa na vitendea kazi katika kuwezesha vyuo hivi kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi kama inavyotarajiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwiano mkubwa wa wanafunzi kwa darasa (msongamano wa wanafunzi darasani), pamoja na kazi kubwa iliyofanyika kwenye elimu nchini, bado kuna changamoto kubwa ya wanafunzi kusongamana madarasani. Hali hii inachangiwa na uhaba wa madarasa kwa baadhi ya maeneo, pia uchache wa walimu. Tatizo hili linaathiri sana ubora wa elimu kwa shule za umma. Ipo haja sasa ya Wizara kuangalia namna ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Elimu iangalie eneo hili. Shule na madarasa yameendelea kujengwa kwa fedha za miradi kama vile *SEQUIP, BOOST, GPE* – na *HEET* lakini tatizo bado linaendelea. Nataka kujua nini mkakati wa Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu kumaliza tatizo hili la msongamano wa wanafunzi darasani?

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya sekta ya elimu nchini inahudumiwa na kujengwa kwa kutumia fedha za wahisani kupitia Benki ya Dunia na washirika wa maendeleo. Je, ni upi mkakati wa Serikali ili tusiendelee kutegemea hizi *projects* kwa kiwango hiki kikubwa? Je, siku ikitokea hatuna miradi ya wafadhili, madarasa yatakuwa hajengwi? Wizara ije na mkakati mahsusi wa namna ya kumaliza changamoto ya vyumba vya madarasa kulingana na *projections* ya *population growth* na *enrolment rates* katika taasisi zetu za elimu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali imekuwa na utaratibu wa kutoa maelekezo ya kila mwaka kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Halmashauri kuhusu ujenzi wa madarasa bila kuangalia uwezo na vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutekeleza maagizo hayo. Utaratibu huu siyo endelevu na wakati mwingine wanatumia mwanya huo kuchepusha fedha wakisingizia kutekeleza maelekezo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya hasa katika Wizara hii ya Elimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri pamoja na wasaidizi/watendaji wake wote wa Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kazi kubwa wanayoifanya ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kuhusu mfumo wetu wa elimu nchini ambao haumwandai mwanafunzi kuweza kujitegemea mara baada ya kumaliza masomo yake. Hivyo basi, kuna haja ya kuboresha mfumo wetu wa elimu nchini ili mfumo wa elimu uweze kumwandaa mwanafunzi kuweza kujitegemea mara baada ya kumaliza masomo yake bila ya kusubiri kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara kupeleka vifaa vya kisasa vya kufundishia kwa walimu na wanafunzi kwa wakati shule zote nchini, pia Wizara iboreshe mazingira wezeshi kwa walimu kutokana na mazingira yaliyopo maeneo yao hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna changamoto ya ukosefu wa ajira nchini, naishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iboreshe na iongeze kujenga Vyuo vya Elimu Amali/Vyuo vya Kati kote nchini, pamoja na kupeleka vifaa vya kisasa vya kufundishia ili kuzalisha wataalam wengi wa fani mbalimbali bobezi. Hii itasaidia jamii kuthamini vyuo hivyo vya kati na vijana wengi kujiunga na kunufaika kwa wingi zaidi na itasaidia sana kupunguza wimbi kubwa la vijana wasio na ajira, vijana wazururaji pamoja na vijana wanaosubiri ajira Serikalini, na pia itapunguza mzigo mkubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, licha ya maboresho mengi ya mitaala na Sera ya Elimu kufanyika, ni vyema Wizara ikawawekea wanafunzi somo maalum la stadi za maisha, stadi za kazi, pamoja na somo la uzalendo ili kuwajenga watoto kuitambua nchi yao kiundani pamoja na kujitambua wao wenyewe ili wawe raia wema na kuwa wazalendo wa nchi yao, kwa sababu vijana wengi waliosoma, wakirudi mitaani wanafanya matukio ya ajabu ajabu yakiwemo wizi na mauaji. Hii yote inasababishwa na kukosa uzalendo na kutokujitambua.

Mheshimiwa Spika, pia kuna haja ya kuwapunguzia mzigo mkubwa wa idadi ya masomo watoto ili kuwapa wepesi katika ufahamu wa masomo yao na wanachokisoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii muhimu kwa ajili ya maslahi mapana ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa aliyoyafanya katika sekta ya elimu kwa ujenzi wa madarasa ya kisasa, ujenzi wa vyuo vya *VETA* 29 ambavyo vimekamilika na vingine vinaendelea kujengwa, na utoaji wa vishikwambi kwa walimu ambacho ni kielelezo tosha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kufanya maboresho makubwa katika elimu. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Prof. Adolf Mkenda, yeye na timu yake kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya na timu yake. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maboresho ya mtaala mpya uliofanyiwa marekebisho mwaka 2023. Mtaala huu ni mzuri kwa kuwa unalenga kuwafanya watoto wetu watoke na ujuzi na endapo utatekelezwa ipasavyo, utasaidia vijana wengi kujiajiri badala ya kutegemea kuajiriwa, lakini changamoto ninayoiona hapa ni namna ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka ukombozi wa Taifa hili na tunataka maendeleo endelevu, ni lazima tuwekeze kwenye elimu. Mataifa kama China na Marekani yamefanikiwa katika uchumi kwa sababu ya elimu. Serikali iangalie na ijue nini kifanyike ili maboresho ya mtaala huu yaweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, kwanza Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga karakana na maabara za kisasa zinazoendana na wakati huu wa sayansi na teknolojia. Pia walimu wapya na wa zamani wajengewe uwezo kwa kuwapa mafunzo ya mara kwa mara yanayoendana na nyakati za sasa. Aidha, Serikali itenge fedha za kutosha za kununua vitendea kazi kwa ajili ya mafunzo ya ufundi stadi na kuwepo na *TV screen*

angalau moja katika vyuo vyetu vya ufundi ili wakati mwingine wanafunzi waweze kujifunza kwa njia ya *video*.

Mheshimiwa Spika, mwanafalsafa mmoja wa Marekani, John Dewey's amewahi kusema, elimu ni maisha na elimu ni kila kitu kwa mwanadamu. Kwa maboresho ya mtaala huu mpya ni kuwapa maisha vijana wetu endapo tu Serikali itajikita kwa nguvu zake zote kuutekeleza mtaala huu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza sana Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda na Naibu wake Mheshimiwa Omari Kipanga na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nitachangia kuhusu mkanganyiko uliopo kwenye matumizi ya *GPA* ya 3.8 katika vyuo vikuu vya Serikali vilivyo chini ya *TCU*.

Mheshimiwa Spika, kwenye kuajiri walimu wa vyuo vikuu, vigezo vinavyotumika ni vya kutumia *GPA* za waombaji. Mwongozo uliotolewa na *TCU* umeelekeza kwamba mtu anayeomba kazi ya kufundisha ni lazima awe na *minimum GPA* ya 3.5 kwenye *degree* ya kwanza, na *minimum GPA* ya 4.0 kwenye *degree* ya pili.

Mheshimiwa Spika, ninavishukuru vyuo binafsi kwani vinafuata mwongozo huo wa *TCU*, lakini inasikitisha kuona kwamba kwenye vyuo vya Serikali, kuna utaratibu unaokiuka maelekezo ya *TCU* na kuwanyima Watanzania haki ya kuajiriwa katika vyuo hivi.

Mheshimiwa Spika, katika vyuo vya Serikali, mtu anayeomba kazi ya kufundisha ni lazima awe na *minimum GPA* ya 3.8 kwenye *degree* ya kwanza na *minimum GPA* ya 4.0 kwenye *degree* ya

pili. Mwongozo wa *TCU* umepanga, *first class 4.4 – 5.0, upper second 3.5 – 4.3, lower second 2.7 – 3.4,* na *pass 2.0 – 2.6.*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kwamba hii *GPA* ya 3.8 inayotumiwa na vyuo vya Serikali imetoka wapi? Kwa *grading system* ya *TCU* iliyoko hapo juu, *GPA* inayoanza na *GPA* 3.5 ni *cut off point* ya *upper second,* ndiyo maana *TCU* wakaelekeza hiyo itumike.

Mheshimiwa Spika, kwenye hiyo *GPA* 3.8, hii wameiweka kwa vigezo gani? Kwa nini isiwe *GPA* 3.6, 3.7 au 3.9. Kwangu mimi naona huu ni ukiritimba na tunawanyima nafasi za ajira vijana wetu wanaotaka kuajiriwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, mtu aliyesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *SUA*, Mzumbe vyenye walimu wabobevu na miundombinu bora ya ufundishaji na akapata *GPA* ya 3.5 anaweza akawa na uwezo mkubwa kuliko aliyetoka chuo "x" na "y" aliyepata *GPA* ya 3.8 chenye uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ifanye marekebisho na kutumia *GPA* ya 3.5 kwa vyuo vyote ili kutoa haki sawa za kuajiriwa katika vyuo vikuu vya Serikali na binafsi. Hii itafanya wanaotaka kuhama kutoka vyuo binafsi wakiwa na *GPA* ya 3.5 hadi 3.7 kwenye *degree* ya kwanza wapate nafasi za kufundisha. Kwa kufanya hivi, tutaondoa ubaguzi unaojitokeza kwenye vyuo vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, nitachangia hoja hii kwa kuanza na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu na hivyo kuongeza wanufaika wa mikopo hii ambao kimsingi wengi ni

vijana na pia napongeza hatua ya Serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati, lakini bado gharama ya kugharamia mikopo wa elimu ya juu ambayo ni asilimia kubwa ya bajeti kila mwaka, mfano mwaka huu ni zaidi ya 60% ya bajeti nzima, tena fedha hizi zinahesabiwa kama *recurrent expenditure* (miradi ya maendeleo).

Mheshimiwa Spika, ili fedha hizi zistahili kuwa sehemu upande wa miradi wa maendeleo ni lazima ziweze kuzalisha na kufikia hatua fulani. Bodi isitegemee tena fedha za Serikali kujiendesha, ziwe *revolving* zenyewe.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri anahitimisha, atueleze kwa nini Serikali mpaka leo haioni haja ya kuleta fungu mahususi la fedha za kugharamia elimu ya juu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Kipanga. Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu na adimu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuniwezesha kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini ili kuweza kumsaidia katika Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, mimi pamoja na Waziri wangu, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Spika wetu, lakini vilevile Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri wenu kuweza kusimamia na kutuongoza katika mjadala wa hoja hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee namshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Husna Sekiboko pamoja

na Wajumbe wote wa Kamati hii ya Elimu, Utamaduni na Michezo, kwanza kwa kuweza kuchambua shauri letu hili.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wote walishiriki kuchambua na kushauri Wizara kikamilifu. Kipekee nichukue fursa hii kuwashukuru kwa kupitia taarifa yetu na vilevile kuchangia katika makadirio haya ya mapato na matumizi ya mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango yao hapa, wametoa pongezi, ushauri na maoni yaliyolenga kuboresha Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na ubunifu. Ndugu zangu, kipekee tunaomba tuwashukuru, na tumepokea pongezi zenu, maoni yenu pamoja na ushauri mlioutoa kwa lengo la kwenda kuboresha utendaji kazi katika Wizara yetu. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa uongozi wake na ushauri. Mheshimiwa Waziri huyu siyo tu ni kiongozi, lakini ni mwalimu. Kwangu mimi ni rafiki wa karibu sana. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana kwa uongozi pamoja na ushauri wako katika uendeshaji wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, namshukuru sana Prof. Nombo, Katibu Mkuu wetu; Naibu Makatibu Wakuu, Prof. Mdoe pamoja na Dkt. Franklin, Menejimenti ya Wizara na watumishi wenzangu wote, kwa ushirikiano mnaotupa katika kuendesha Wizara hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wangu au wananchi wenzangu wa Mafia kwa kuendelea kuniamini na vilevile kunipa ushirikiano na kunivumilia katika kipindi chote ambacho natekeleza majukumu ya Serikali ndani na nje ya mipaka ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 03, 04 na 05, kumetokea dhoruba kubwa kule Mafia, Kimbunga Hidaya, kimeweza kuvamia eneo lile lote la ukanda wa Pwani. Athari zimekuwa ni

kubwa na matatizo makubwa yametokea na uharibifu mkubwa wa mali umetokea. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wenzangu katika madhara na madhila haya yaliyotukumba.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwamba tuendelee kuwa wavumilivu na tuendelee kufanya subira katika kipindi hiki wakati Serikali inalishughulikia jambo hili. Sambamba na Mafia, nafahamu vilevile janga hili liliweza kufika maeneo ya Kilwa, Lindi pamoja na Mtwara na maeneo yote ya Ukanda wa Pwani. Basi nichukue fursa hii kuwapa pole wananchi wote waliokumbwa na madhila haya ya Kimbunga Hidaya.

Mheshimiwa Spika, kipekee naishukuru familia yangu kwa ujumla, watoto pamoja na wake zangu kwa kuendelea kunivumilia, kuniombea dua pamoja na kunipa ushirikiano katika kipindi hiki chote cha kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nami nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi na kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza, ambalo ningependa kuchangia ni mafunzo ya walimu kwa ajili ya utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa. Nafahamu Wabunge wengi wamechangia kwenye eneo hili na kuonesha wasiwasi wao na kutaka kujua namna gani Serikali itafanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwanza kwenye eneo la mafunzo ya walimu, Serikali yenu kupitia Wizara ya Elimu, tumeweza kutekeleza au kutoa mafunzo kwa walimu wote ambao tunatarajia watakwenda kufundisha katika mtaala huu ulioboreshwa. Kwa ujumla Serikali imetoa mafunzo kwa walimu wanaopaswa kufundisha zaidi ya 181,777 wa elimu ya awali mpaka wale wa darasa la saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeweka mpango endelevu kwa sababu mafunzo haya siyo kwamba yatatolewa tu katika kipindi hiki ambacho tumeanza kutekeleza mtaala, lakini

yatakuwa ni mafunzo endelevu katika maeneo yote ya nchi yetu ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza umahiri kwa walimu wetu pindi watakapokuwa wanakwenda kuwafundisha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna yale maeneo ya *the Teachers' Resource Centres,* zitaendelea kutumika na hivi sasa tumeendelea kuziboresha kwa maana ya kuzifanyia ukarabati na vilevile kuongeza vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia kwenye zile *cluster* zetu mbalimbali. Katika ngazi ya *cluster* vilevile mafunzo haya yatakuwa yanaendelea kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi mkubwa kwenye eneo la elimu ya amali, ambapo tumeanza kutekeleza kwa upande wa sekondari, elimu ya amali kwa kidato cha kwanza. Kitu gani ambacho tumefanya mpaka hivi sasa? Serikali kwa kushirikiana na taasisi zilizopo chini ya Wizara, imefanya maandalizi ya walimu kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala mipya.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hapa kilichofanyika ni kuanza kutoa mafunzo kwa walimu watakaokwenda kufundisha katika elimu hii ya amali. Walimu 552 wa shule za sekondari zinazofundisha masomo ya amali wameweza kupata mafunzo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile mafunzo yametolewa kwa walimu 346 wa sekondari wanaofundisha masomo ya jumla. Tunajua kwamba katika utaratibu au mfumo huu, sasa hivi kutakuwa na michepuo miwili. Kutakuwa na yale masomo ya kawaida na vilevile kutakuwa na yale masomo ya amali. Kwa hiyo, tumetoa mafunzo kwa walimu wale ambao watafundisha masomo ya amali.

Mheshimiwa Spika, vilevile kutakuwa na masomo ya kawaida ambayo nayo tumeweza kuwapa mafunzo walimu 346 kwenye masomo haya ya jumla katika mkondo wa amali wa kidato cha kwanza ambapo walimu wa shule za Serikali walikuwa ni 147, na kwa shule zile za binafsi walikuwa ni walimu 199.

Tunafahamu kwamba tuna shule 98 ambazo zimeanza kutoa elimu hii ya amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada za upatikanaji wa walimu wa kutosha kwa upande wa elimu ya amali zinaendelea kupitia mafunzo ya wenzetu wa *VETA*, ambapo walimu wa mafunzo ya amali zaidi ya 68 wameweza kupata mafunzo. Vilevile kupitia taasisi yetu ya Mamlaka ya Baraza la Elimu ya Ufundi, imeweza kuwafundisha walimu 843, wamepata mafunzo haya ya elimu hii ya amali kwenye shule zetu hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, juhudi hizi zinaendelea na niwaondoe hofu na sisi tutazisimamia kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kwamba ule umahiri unakwenda kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili au hoja ya pili ilikuwa ni ya uhaba wa walimu kwa ujumla. Nini Serikali imefanya kwenye eneo hili? Katika kukabiliana na uhaba wa walimu, pamoja na jitihada zilizofanywa za kuongeza ajira za walimu, tunafahamu Serikali yetu kwamba imekuwa ikiajiri walimu kila mwaka. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea na mikakati mingine endelevu kuhakikisha tunapunguza uhaba wa walimu kwa kuwawezesha walimu. Kwa hiyo, sasa tutakuwa na mfumo wa kuwawezesha walimu kuwa na mfumo wa kupata *internship*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, walimu wote sasa watakaokuwa wanamaliza *course* zao za ualimu kabla ya kwenda kazini tutakuwa na mfumo wa kupata *internship* ya mwaka mmoja ili baadaye waje kupata leseni. Katika mfumo huu tutakwenda kupunguza tatizo la upungufu wa walimu zaidi ya 12,988 kila mwaka. Kwa hiyo, ni lazima mwaka mzima hawa waweze kukaa shuleni kwa ajili ya kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupeleka walimu wetu *internship,* tutakuwa na faida zifuatazo: -

(i) Tutawa-*expose* walimu wetu kwenye uzoefu halisi kuhusu fani ya ualimu katika mazingira halisi ya shule;

(ii) Watapata uzoefu wa namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa ufundishaji na ujifunzaji; na

(iii) Tutawapa nafasi walimu wetu (wahitimu) katika ualimu kwa kushirikiana na walimu wazoefu katika eneo la kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, mkakati mwingine wa Serikali ni kuendelea kutumia fursa za walimu wa kujitolea na tumeshatoa miongozo mbalimbali ya namna gani ya kupata hao walimu wa kujitolea kabla hawajapata ajira zao. Kwa hiyo, mkakati huu nao vilevile utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kwenye upungufu katika eneo la elimu ya amali, nimezungumza kule nyuma, lakini sasa tuna mkakati kwa upande wa elimu ya amali ambapo tumedhamiria kuchukua hatua kadhaa. Eneo la kwanza ni kuhakikisha tunakabiliana na upungufu wa walimu wa mafunzo ya amali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwatambua walimu wa mkondo wa amali waliopo kwenye shule zisizokuwa na mikondo ya amali. Kwa hiyo, tumetambua zaidi ya walimu 18 na tumeweza kuwahamisha kutoka kwenye shule zile ambazo zilikuwa hazifundishi masomo hayo na kuwapeleka sasa kwenye shule ambazo zinafundisha mikondo ya amali na walimu hawa wamepelekwa takribani katika shule tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, Serikali itaendelea na uzalishaji wa walimu wa mafunzo ya amali katika ngazi za vyuo vikuu ambapo sasa kuna vyuo vikuu ambavyo tunakwenda kuvibadilisha ili viweze kutoa elimu ya amali.

Mheshimiwa Spika, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba Chuo chetu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya tunakwenda kuki-*convert* na kutengeneza *campus* katika Mkoa wa Mtwara, kwa vile vyuo viwili, Mtwara Kawaida na Mtwara

Ufundi ambapo sasa zile zitakuwa ni *campus* maalum kabisa kwa ajili ya kuzalisha walimu wa amali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Chikota, wakati anazungumza hapa kwamba, lini Mtwara itapata chuo kikuu? Sasa tunakwenda na mpango huu ambapo vyuo vile viwili tunakwenda kuvifanya viwe *campus* ya Chuo Kikuu cha Mbeya na *specifically* vitakuwa ni kwa ajili ya kuzalisha walimu hawa wa amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa tatu, kwenye mitaala yetu ya vyuo vikuu, tunajua kwamba katika mkondo huu wa elimu ya amali utakuwa unaanzia kidato cha kwanza huko, lakini dhamira ni kufika mpaka chuo kikuu. Kwa hiyo, vyuo vikuu sasa kupitia mradi wetu wa *HEET*, vinafanya mapitio ya mitaala ile ili kuhakikisha kwamba tunazalisha walimu ambao vilevile watakuja kufundisha mkondo wa amali kuanzia ngazi ya sekondari mpaka vyuo vikuu kwa wale wanafunzi watakaofika mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, mkakati wetu wa nne pamoja na jitihada hizo za Serikali katika kupata walimu wa mafunzo ya amali, Wizara ya Elimu, Utumishi pamoja na TAMISEMI tutaendelea kuajiri walimu katika kada hii ya elimu ya amali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyofikishwa mbele hapa ni usambazaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia hasa kwenye shule hizi ambazo zimeanza mkondo wa amali. Naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari alishatoa fedha kwenye shule zile 28 za Serikali, jumla ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunanunua vifaa vya kujifunzia na kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Taasisi yetu ya Elimu tayari ilishachapisha nakala 4,500 za masomo manne ya Historia ya Tanzania ambayo wataanza Kidato cha Kwanza; *Mathematics for Ordinary Education, Form One*; *Business Education for Lower Secondary Education, Form One,* pamoja na *English Low Level Secondary Education* ya *Form One*. Vitabu hivi nakala 4,500 tayari vilishachapishwa na kupelekwa kwenye shule hizi zote za amali,

zile za Serikali, na zile shule 68 za binafsi katika uwiano wa mwanafunzi mmoja kwa kitabu kimoja.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna yale masomo ya jumla, tayari taasisi yetu ya *TET* imechapisha jumla ya nakala 104,956 ya vitabu tu vya kiada ambavyo tutakwenda ku-*compliment* kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la Shule za Msingi, hapa vilevile Waheshimiwa Wabunge walionesha wasiwasi kwenye eneo hilo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hilo kuhusu usambazaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwenye shule zetu za msingi, madarasa yaliyoanza kutekeleza mtaala huu ulioboreshwa ni darasa lile la awali, darasa la kwanza na darasa la tatu. Niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari nakala ngumu 9,825,601 zilichapishwa na zimesambazwa. Kuna upungufu kwenye baadhi ya mikoa ambayo hatujaweza kuifikia yote kwa ukamilifu, lakini kwa mikoa ambayo tayari vitabu hivi vimeshapelekwa kwa uwiano wa 1:2 mpaka 1:4 kwa mwanafunzi kwenye mikoa mingi sana, imeshapelekwa isipokuwa kwenye mikoa 10 vitabu hivi havijapelekwa kwa ujumla wake, tumepeleka kiasi fulani, lakini bado havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, mikoa hiyo 10 ni pamoja na Mkoa wa Iringa, Katavi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Songwe na Tabora. Kwa hiyo, kazi ya usambazaji wa vitabu hivi unaendelea, tumefikia 91% na baada ya muda siyo mrefu tutakuwa tumekamilisha. Hii ni kutokana tu na hali ya hewa ambayo imejitokeza.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni mengi, lakini kutokana na muda, naomba kuunga mkono hoja. Nadhani hoja zilizobaki Mheshimiwa Waziri atakuja kuzimalizia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya kuhitimisha hoja. Naanza kwa kuushukuru sana kwa uongozi wako kwa kipindi hiki cha bajeti yetu wewe na viongozi wengine wa Bunge letu na kuendelea kukupongeza kwa nafasi yako ya kuwa Rais wa Mabunge ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa michango mizuri sana, maswali na hoja ambazo kwa kweli tunawajibika kuzitafakari vya kutosha na kuzifanyia kazi. Nyingi tunazibeba kama ushauri kwa ajili ya utekelezaji wa kazi iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukurani za pekee kwa Kamati yetu chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Husna Sekiboko na Makamu wake, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima kwa kazi nzuri sana ya kutusimamia na kutuongoza mpaka hapa tulipofika. Kwa kweli maoni yao kama yalivyowasilishwa katika Bunge lako hili Tukufu, tunayabeba kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Kipanga. Kwanza nampa pole kwa dhoruba iliyotokea kwenye Jimbo lake la Mafia, pia uongozi wake na usaidizi mkubwa sana anaotupatia katika Wizara yetu; Katibu wetu Mkuu Profesa Carolyne Nombo, Profesa James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Franklin Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Mutahabwa, Kamishna wa Elimu; Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na Watumishi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutuwezesha kufika hapa tulipofika.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru vilevile kwa nchi nzima walimu wote, wakufunzi na wahadhiri katika taasisi zote za umma na binafsi kwa kazi kubwa wanayoifanya kuendeleza elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali, labda nimwelezee tu Mheshimiwa Rashid kuhusu suala la shule iliyopo Pemba, kwamba shule za Sekondari haziko kwenye Mfumo wa Muungano. Kwa hili jina zuri lililotukuka la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan linapaswa kuwekwa kule na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na tutawasiliana na Wizara ile tuhakikishe kwamba kweli jina linabadilishwa kama maelekezo yalivyokuwa yametolewa.

Mheshimiwa Spika, tulisikiliza vizuri sana maelezo ya Mheshimiwa Ally Kassinge kuhusu athari za mafuriko katika eneo lake. Tunampa pole na naungana na Naibu Waziri na Watanzania wote kutoa pole kwa wote walioathirika sana na dhoruba hii ya mafuriko na hali mbaya ya hewa.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeona sekta ya elimu vilevile imeathirika. Nilipata fursa ya kutembelea Kibiti na Rufiji kujionea mwenyewe. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inafanya kazi na TAMISEMI imepeleka timu katika maeneo yote kufanya tathmini na kuhakikisha kwamba tunachukua hatua ili masomo yasiweze kuathirika.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Ally Kassinge kwamba hata kule Kilwa vilevile tunashirikiana na TAMISEMI kwamba hatuzuii masomo. Wizara imefanya jitihada ya kupeleka mahema, kuhamisha wanafunzi na kuhakikisha kwamba shule nyingine zinapokea wanafunzi ambao wameathirika, waingie pale waanze kusoma. Naomba tusubiri tuone tutafika wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla tumepata maoni 62 kwa wachangiaji. Maoni 11 kwa maandishi na 51 yamechangiwa humu ndani. Nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu tutayabeba yote, kwani sitaweza kujibu kila hoja.

Nawahakikishia kwamba tunayatilia maanani sana. Kila Mbunge aliyezungumza, kila mmoja amemshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa ya elimu ambayo ameyaahidi hapa Bungeni, na ameyasimamia. Kazi imeanza na inaendelea.

Mheshimiwa Spika, vilevile naungana na Wabunge wenzangu wote kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake haya makubwa na ujasiri wake wa kuhakikisha kwamba tunaanza na kazi hii. Ukiangalia Tume ya Rais ya Elimu ya Mwaka 1982, maarufu kama Tume ya Makweta, baadhi ya mambo mengi ambayo tunazungumza sasa hivi yalikuwepo mle mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kutumia neno amali, mafunzo ya amali tunayoyazungumza sasa hivi yamo kwenye juzuu la kwanza la taarifa ile, lakini hayakutekelezwa. Nadhani kigugumizi labda kilitokana na hali ya uchumi ya wakati ule, japokuwa Mheshimiwa Makweta naye alikuja kuwa Waziri wa Elimu, lakini hali ya uchumi haikuruhusu.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 ambayo ilizinduliwa 2015, karibia mambo yote ya sera mpya hii yamo mle; miaka 10 ya elimu ya lazima, mafunzo ya amali na kadhalika; lakini baada ya kuzindua, hakuna chochote kilichofanyika katika maeneo hayo makubwa kwa sababu nadhani inahitaji sana rasilimali kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameonyesha wasiwasi, kwamba ni suala kubwa sana linahitaji rasilimali watu, rasilimali fedha, kujipanga vizuri na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Rais wetu kuamua kwamba tusonge mbele baada ya kufanya mapitio ya sera ile na kupata toleo la 2023 na anajua kwamba itagharimu fedha na kusema endeleeni na kazi hii, ni ujasiri mkubwa sana kwa Rais wetu. Kwa kweli maua yetu tunayatoa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi yetu wasaidizi wake ni kuhakikisha kwamba hatumwangushi na kuhakikisha kwamba tunawaondoa hofu Watanzania wote kwamba kazi hii itafanyika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mawili makubwa katika mageuzi ya elimu ambayo lazima tuyakumbuke na kuyatilia maanani ni kwamba ikifika mwaka 2027 itakuwa ni lazima kwa kila mwanafunzi kukaa shuleni walau miaka 10 ukichanganya na elimu ya awali ni miaka 11. Hilo ni jambo kubwa na la kwanza na limezungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, inatia hofu wakati mwingine kwamba tutawezaje? Wenzetu Zanzibar hawakuwahi kuondoka kwenye mfumo huo na elimu yao, walishaenda miaka 11, sasa hivi wanarudi tena miaka 10 na wanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kubadilisha mfumo wa elimu kuwa na mikondo miwili katika sekondari ya chini na sekondari ya juu, elimu jumla na elimu ya amali. Sitaweza kufafanua sana hili, tumeshazungumza sana, lakini niko tayari kutoa ufafanuzi kwa fursa nyingine. Hili nalo linahitaji rasilimali watu, rasilimali fedha nyingi na kuhakikisha kwamba tunatekeleza. Sababu yake ni kwamba tumeamua kuanza hatua ndogo ndogo kwenda mbele, kwa sababu tunataka kutafuna kile tunachoweza kukimudu.

Mheshimiwa Spika, kuna kauli ilitolewa hapa kwamba tunafanya *piloting*, siyo *piloting* kabisa. Tumeanza safari, hakuna gia kurudi nyuma. Hii kazi tuliamua kwamba kwa mfano, tungesema sasa hivi twende miaka 10, tunajua changamoto ingekuwa kubwa sana. Tumesubiri mpaka 2027 na nitaeleza rasilimali fedha tutazipata wapi kuhakikisha kwamba tunatekeleza hiki ambacho kimeahidiwa.

Mheshimiwa Spika, hata mafunzo ya amali, hata shule za Serikali nyingine ambazo zilitaka kuingia kwenye mkondo wa mafunzo ya amali, na shule binafsi zimefanyiwa tathmini na Kamishna wa Elimu, nyingi tumewaambia subiri, bado vigezo

havijatimia. Shule za Serikali vigezo vimetimia kwa shule 28 peke yake, shule binafsi ni 68 peke yake. Tumesema tuko tayari kuanza kwa hatua ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Kaboyoka mtani wangu alizungumza hapa vizuri sana. Aliyazungumza hayo utadhani alikuwepo wakati sisi tunapanga namna ya kuweza kutekeleza. Kwa hiyo, haya ni mageuzi makubwa sana, lakini tumehakikisha kwamba tunaenda nayo kwa hatua ambazo tunazimudu. Kila hatua tunayoipiga tunaimudu kwa 100%. Kwa hiyo, haya mageuzi tunaenda nayo, muda ungekuwa unaruhusu ningejaribu kutoa ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie mitaala mipya tunaanza nayo vipi? *Choice* ingekuwa ni kusema kwamba tunafumua mitaala yote na kuanza upya kwa *level* zote na ziko nchi zimefanya hivyo, tumesema hapana, mitaala mipya itaanza elimu ya awali, ambapo imeanza mwaka huu. Darasa la kwanza imeanza mwaka huu, darasa la tatu imeanza mwaka huu na darasa la pili; darasa la nne, darasa la tano, darasa la sita na darasa la saba ni mitaala ya zamani.

Mheshimiwa Spika, watu wengine walishangaa lakini tulisema *we bite what we can chew*. Tunajaribu kuanza na kile ambacho tunaweza kukimudu. Rasilimali zitatosha, vitabu vitatosha. Kama alivyosema Mheshimiwa Kipanga, isingekuwa hali ya hewa, hapa vitabu vipo, vimepelekwa sehemu nyingi na hata vile ambavyo vimepelekwa kwa njia ya mtandao, Airtel tuna makubaliano nao, mwalimu hana haja ya kununua *bundle*. Akiwa na kadi ya Airtel ana-*download*, anavisoma lakini *hardcopy* ndiyo mwendo wenyewe; *softcopy* ni *option.* Tumefanya hivi maksudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa sekondari kwa mwaka huu tumeanza *Form One* kwa wale wa mafunzo ya amali tu kwa mitaala mipya. Kwa hiyo, tumeanza kwa shule 28 za Serilkali na 68 za Serikali kwa *form one*. Tunaenda hivi kwa sababu tunataka kila hatua tunayokwenda tuhakikishe tumewekeza vya kutosha siyo *piloting*. Tunaangalia *resource envelope* ambazo kama

nitakavyoeleza, kwa kweli zitafunguka na nadhani yajayo yanafurahisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaenda *form five*. Baada ya hapa sasa hivi kuchukua wanafunzi wa *form five* wataanza na mitaala mipya. Kwa hiyo, tunaenda hivi kwa sababu hatutaki hofu ambayo kila mmoja ameionesha ambayo ni ya haki kabisa kwamba, tusije tukakimbia sana wakati *resources* tumeziacha nyuma, halafu matokeo yake yatakuwa kama nchi moja ambayo siwezi kuitaja hapa, ambayo Waziri wake wa Elimu alinieleza kwamba, aliamua kufumua kila kitu wakaanza, wakaboronga, wakarudi tena nyuma, wanaanza tena upya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, tumeenda kujifunza kwao, sasa hivi tumekuta wanajaribu tena kufanya kosa lile ambalo walifanya wakati ule, lakini sisi tunajifunza kwa waliofanikiwa na ambao kwa kweli hali haikwenda vizuri sana. Kwa hiyo, tunasema sasa hivi tunaanza na shule chache kwa mafunzo ya amali, lakini nina uhakika kwamba tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nimekisikia, nikiseme kutoa hofu walau Mheshimiwa Mbunge mmoja au wawili kuhusu wale wanaoenda mafunzo ya amali halafu wakishawapeleka kule hawaendi Chuo Kikuu, itakuwaje? Huu ni mfumo nyumbufu. Mafunzo ya amali yanayo mafunzo ya taaluma machache zaidi. *More practical subjects,* lakini wanaweza wakachukua yale machache kwenda *high school* kwenye masomo ya elimu jumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna *high school* za mafunzo ya amali ambazo itakuwa miaka mitatu. Unatoka na *diploma* na cheti cha *form six,* kama ilivyokuwa *Mkwawa High School* kwa wakati ule. Kwa hiyo, hilo tunakwenda nalo na hakuna sababu ya kuogopa kumpeleka mtoto kwenye mafunzo ya amali kwamba yeye hatakwenda mpaka chuo kikuu.

Mheshimiwa Spika, vyuo vikuu tunaanza *streams of vocationalized university degrees* kama nchi nyingine wanavyofanya. Kwa hiyo, unaweza ukaenda na *degree* yako mpaka *Ph.D* na tunaendelea ku-*maintain* unyumbufu kiasi

kwamba unaweza ukarudi huku na kwenda kule bila kupoteza nafasi yako yoyote.

Mheshimiwa Spika, ukizungumza bajeti ya elimu ni muhimu kuzungumza bajeti ya sekta ya elimu, siyo bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia peke yake. Kwa mfano, mwaka huu unaoisha, sekta ya elimu imepewa jumla ya shilingi trilioni 5.95 zote hizi ziko kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu, hizi shule tunazozungumzia zinajengwa kupitia TAMISEMI. Nimesikia Mbunge mmoja amesema tunaona hapo mmepata fedha za kigeni, kwa nini haujaweka fedha za ndani? Nadhani ni Mheshimiwa Mnzava kama sikosei aliyeongelea hili kwamba, mbona hujaweka fedha za ndani?

Mheshimiwa Spika, hizo fedha za ndani utazikuta TAMISEMI, kwa sababu tukichukua *BOOST* hapa, tunapeleka TAMISEMI, wanachukua fedha za ndani, wanaendelea na kazi. Tukichukua *SEQUIP* zinatoka Hazina zinapitia katika Wizara yetu, zinakwenda TAMISEMI. TAMISEMI utakuta *counter part funds* za Wizara ya Ndani, hatuja-*neglect* nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ujumla wake, kwa miaka miwili ijayo; 2024/2025 na 2025/2026 tuna takribani *1.5 trillion* ambayo tutapeleka kwenye miundombinu tu. Tunayo *BOOST*, *EP4R* Awamu ya Pili, tuna *SEQUIP*, *E-Stream*, *GPE* na *TSP,* hizi ni fedha ambazo zipo *assured* kupitia Hazina. Tumeshaingia *commitment* ni kuzitumia. Tumeshakubaliana na wenzetu wa Hazina kwamba tuta-*accelerate expenditure of the money* ili tuhakikishe kwamba tunaandaa miundombinu mapema iwezekanavyo ili tutakapoanza kuchukua wanafunzi kwenda miaka 10 tutakuwa tayari. Ndiyo maana sasa hivi hatuna wasiwasi na suala hili la miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kazi ambayo tunaifanya, nimeona kuna wasiwasi, kati ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI mnaingiliana na nini. Kitabu hiki labda nitaomba wenzetu tuhakikishe kwamba kila Mbunge anakipata kwa *softcopy*. Kimeandaliwa na Wizara ya

Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI, kina shule zote hapa Tanzania. Shule za Msingi katika maeneo ambayo yana watu wengi ambazo kuna eneo kubwa tutatumia *BOOST* kuongeza *form one, form two, form three* na *form four* utaikuta humu.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari kwenye maeneo yenye watu wengi ambayo ina eneo kubwa tutatumia hela za *SEQUIP* kuongeza darasa la kwanza, la pili, la tatu, la nne, la tano na la sita. Kwa hiyo, kuna shule nyingi hapa sasa hivi zitaweza kuchukua mwanafunzi kuanzia elimu ya awali mpaka *Form Four* ili kuweza kutimiza azma yetu ikifika 2027.

Mheshimiwa Spika, shule zote; naweza nikakusomea shule moja hapa, mtu yeyote anayetaka atakipata lakini tutajitahidi kuweka kwenye *softcopy* ili Wabunge waone kwa sababu mimi na mwenzangu Mheshimiwa Mchengerwa tumekubaliana kwamba tutahakiki taarifa hizi na vizuri Waheshimiwa Wabunge wahakiki na kujua katika eneo lako kweli shule iliyowekwa huku iko sahihi ama vinginevyo? Tuko vizuri katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, mnaona shule zinazojengwa sitataja idadi kupitia TAMISEMI kwa kila Kata na bajeti imewekwa, amezuingumza Mheshimiwa Mchengerwa hapa, kuna shule 100, hizi shule 100 siyo shule za amali tu, hili napenda nilielezee kwa sababu amali ni ufundi na ufundi stadi. Shule 100 ni *technical secondary school* ambayo ukimaliza *Form Four your full technician*, unapata cheti, unaweza ukaajiriwa ukaanza kazi. Tulikuwa nazo nadhani kama tisa tu sasa hivi ambazo nazo tunazi-*revamp*.

Mheshimiwa Spika, najua ukiangalia karakana unaona kidogo ziko *outdated*. Nilienda *Tanga school,* nimeiangalia tumewekeza fedha kuzi-*revamp*, tunajenga mpya 100. Tunajenga sehemu mbalimbali, mfano nimchukue Mbunge mmoja, Mheshimiwa Taletale nadhani yumo humu ndani, kwake hakupata *VETA* atapata shule ya ufundi. Wabunge ambao wako kwenye Wilaya yenye *VETA,* lakini yeye Jimbo lake kwenye Wilaya hiyo haikupata *VETA,* atapata *technical secondary school* kuhakikisha kwamba tuna-*balance* na *list* ipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama unajua hukupata *VETA* unaweza ukaja ukahakiki. Fedha zipo, ujenzi unaanza sasa hivi na katika shule hizo 26 zitaanza kuchukua wanafunzi mwezi Januari.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo kila mmoja anasema ni walimu. Tunajipanga kuhakikisha kwamba tutakapoanza tutakuwa na Walimu. Nawakumbusha tena Waheshimiwa Wabunge mtaona *clip* moja inazunguka nadhani *CEO* wa *Apple or* sikumbuki nani, alisema hawaendi kuwekeza China kwa sababu eti gharama ya nguvu kazi ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, gharama ya nguvukazi China ni kubwa, hajui mnapozungumzia China ya gharama ndogo, mnazangumzia China gani? Wanazungumzia kule kwa sababu wana *technicians* wengi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna moja ya kuvutia uwekezaji hapa nchini ni kuhakikisha vijana wetu tunawa-*train in high precision* kwenye *technical education*. Hizi shule tutakazozijenga, hata tunavyozijua zilivyokuwa sijui *Tanga school*, *Moshi school* tunaenda kujifunza kwa wenzetu, tutaendelea kuzi-*modernize* kuhakikisha kwamba kweli zinatoa *technicians* ambao wanakidhi matakwa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naweza nikasema ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge yajayo kwa kweli yanafurahisha. Nadhani ujasiri wa Rais wetu wakati amekubali kupitisha mageuzi haya, tunaona yanazaa matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongeze tu, kwa mfano shule za wasichana 26 za mikoa nazo tunazigeuza, zitakuwa za sayansi vilevile na mafunzo ya amali. Vyuo vya kilimo, namshukuru sana Mheshimiwa Hussein Bashe, baada ya mazungumzo amesema atavitoa vile vyuo vitatumika kwenye mafunzo ya amali. Mazungumzo yanaendelea na Wizara nyingine sizitaji sasa hivi lakini kuna fursa ya kuongeza wigo mpana sana wa kuchukua wanafunzi katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mtu anasoma *diploma* ya kilimo, atakuwa anasoma *high school* na *diploma* ya kilimo lakini *it will be more practical.* Anasoma kupata *certificate,* atapata cheti cha *Form Four na certificate* yake ya kilimo kwa sababu ni mafunzo ya amali kama tunavyotaka.

Mheshimiwa Spika, *VETA* za wilaya zote ambazo tunazijenga, tuna mpango wa kuhakikisha kwamba tunazi-*modernize* kwa kutumia mradi tuliuonao kuhakikisha kwamba kuna *possibility* ya kuchukua wanafunzi wa *O' Level* na *VETA* za mkoa zichukue wanafunzi wa *A' Level*. *FDC* vilevile kama ilivyopendekezwa hapa tutaangalia uwezekano wa kuzitumia vizuri. Tuna Chuo cha Ufundi Dodoma pengine Waheshimiwa Wabunge watapenda kukitembelea maana kinaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, *campus* zote zinazojengwa nje ya *main campus* ambazo zinajengwa, sasa hivi tumeziagiza, zitakuwa za mfumo wa mafunzo ya amali. Kwa mfano, huko Mtwara; narudia tena, Mtwara. Mtwara kawaida na Mtwara ufundi tunaunganisha chini ya chuo kimoja cha ufundi halafu watahakikisha kwamba wanafundisha mambo ya amali, mtu anaenda kusoma kule.

Mheshimiwa Spika, Lindi wapo chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lakini kilimo atakachofundisha *should not be academic,* itakuwa ni mfumo wa mafunzo ya kilimo, mafunzo ya amali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, muda ungeruhusu ningetoa *details* zaidi lakini kuna mambo mengine ni vizuri nikaeleza hapa. Tahasusi zimezusha taharuki, labda haifahamiki kwamba 2010 tulikuwa na tahasusi 80, lakini kuwa na tahasusi zilizoidhinishwa haimaanishi zinafundishwa. Mimi nilimaliza *EGM high school. High school* za Serikali zenye *EGM* ilikuwa ni Pugu, Tosamaganga na *Shy Bush,* tatu tu. Kwa hiyo, kuwa na ile tahasusi haina maana shule zote ziliweza kufundisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuongeza tahasusi kutoka 80 kwenda 88 haina maana zote zinaweza kufundisha bila kuwekeza vya kutosha. Kubwa zaidi kuwa na tahasusi nyingi zaidi za *social*

*sciences* haina maana kwamba tutakuwa na wanafunzi wengi wa *social sciences*. Kama mwelekeo wa wanafunzi wengi *inclination* yao ni *social sciences,* ni *option* yao lakini sisi tumeweka kivutio maalum kwenda kusoma masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Samia Scholarship*, ukitaka kwenda kusomeshwa na Serikali chuo kikuu, wewe kasome tahasusi ya *science* hizo ambazo unaziona ni chache, zinaweza zikatolewa na shule nyingi zaidi kuliko ambazo unaona tahasusi ni nyingi na zikatolewa na shule chache. Wingi wa tahasusi ni kutoa wigo tu wa *choice*. Unataka kusoma nini? Unataka kusoma Kifaransa, unataka kusoma Kichina, lugha nyingine kama Kiarabu na kadhalika, kuna fursa hiyo unaweza ukajisomea.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine zilizoendelea hazina tahasusi, zinakwambia tu utajichagulia wewe mwenyewe masomo matatu unayotaka kusoma au manne. Sisi kwa sababu hatuna rasilimali za kutosha tumepanga yale masomo kuku-*limit* kwa sababu tunajua ukienda kusoma Pugu ukajichagulia tahasusi ambayo haipo, huwezi kusoma.

Mheshimiwa Spika, wakati sisi tunamaliza *Form Four,* nakumbuka Mazengo hapa ilikuwa na tahasusi peke yake Tanzania nzima. Ilikuwa na tahasusi moja tu. Ipo kwenye *list* ya shule inayotoa ile tahasusi, ni moja tu.

Mheshimiwa Spika, sasa motisha ya *Samia Scholarship* imetusaidia. Tumeona wanafunzi wengi, ukitembea *O' Level* wanakwambia nitajitahidi kusoma masomo ya sayansi, nikienda *high school* nitasomeshwa na Serikali, nitamwokolea mzazi wangu gharama ya kusoma.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzie hili la *scholarship,* vigezo vipo wazi. *Samia Scholarship is meritocratic scholarship.* Tunataka *the best brain* zikasome *science*. Kwa hiyo, tunatoa kivutio, pamoja na kusomeshwa, una haki ya kusema mimi nilishinda *Samia Scholarship.* Hiyo yenyewe inaingia kwenye wasifu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nchi nyingine ukipata *scholarship* nzuri ukitamka unajua umefanikiwa. Hakuna sababu ya kusema hii ni kwa ajili ya *Means Testing*. Tunaweza tukaanzisha *facility* nyingine ya *Means Testing,* lakini tunataka daktari mzuri. Kama baba yako ana uwezo sana, unataka kwenda kusoma *Law,* jitangaze wewe mwenyewe umechukua *Samia Scholarship,* kasome udaktari uje ututibu kwa sababu uwezo wako ni mkubwa. Kwa hiyo, tunabakiza vigezo hivi tulivyovisema vipo wazi, hakuna mtu anaonewa.

Mheshimiwa Spika, ukipata *point* tatu kama ni masomo ya sayansi unaenda kusoma sayansi chuo kikuu, huachwi. Ukiachwa, njoo lalamika. Sasa *point* tatu umesoma masomo ya *social sciences,* hupati *Samia Scholarship,* haijalishi ndivyo vigezo vilivyo. Vipo wazi, lazima tuvikubali. Kama tunataka mfumo mwingine kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina *scholarship* ambazo ni *Means Testing.*

Mheshimiwa Spika, tunapambana kuongeza *scholarship* nyingine za *Means Testing* lakini hii ya *meritocracy* tuilinde, tuitetee kwa sababu ni kivutio kikubwa sana cha wanafunzi wenye uwezo mkubwa kwenda kusoma *science*, kwenda kusoma *engineering* na kwenda kusoma elimu tiba vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu vyuo vikuu, yaliyosemwa hapa, kwanza nasema ni kweli lazima tukiri kwenye upungufu. Mheshimiwa Prof. Manya tulikuwa wote chuo kikuu, ni kati ya maprofesa, tumemzungumza Mheshimiwa Prof. Muhongo, hatujamzungumza Mheshimiwa Prof. Ndakidemi. *Professors* wazuri sana humu ndani ni *internationally recognized.* Pia Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya ni Profesa mzuri sana, *very young guy, very well recognized internationally.* Alichosema, yote hapa tunabeba bila kupunguza hata kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yamerudiwa kwa namna moja ama nyingine na Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, ndugu yangu Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, Mheshimiwa Prof. Muhongo na baadhi ya watu wengine hapa tunabeba. Tayari tumeshaanza

kufanya baadhi ya kazi, *congestion* vyuo vikuu ni *problem,* hatuwezi kukaa hapa tukadanganya.

Mheshimiwa Spika, *accommodation is a problem, we are not going to cheat anybody.* Tunataka tuboreshe mazingira na maisha ya wanafunzi chuo kikuu. Tunataka walimu wawe na ofisi za kutosha, wakae kwa kujinafasi vizuri, waendelee kufundisha.

Mheshimiwa Spika, hapa katikati tulikuwa na presha kubwa ya kuongeza, lakini Serikali hii na hii ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan jamani ndiyo imevuta mradi wa *Higher Education for Economic Transformation.* Fedha takribani shilingi trilioni moja kuwekeza katika vyuo vikuu kwenye miundombinu na kufungua *campus* nyingine kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tuna-*decongest* hizi *main campus* tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Prof. Shukrani ungependa pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tujenge kila kitu pale, lakini wenzetu wengine wa Kigoma safari hii watakuwa na *campus* ya chuo kikuu na Lindi watakuwa na *campus,* lakini hizi tutazitumia sasa hivi ku-*address* baadhi ya hizo *issue* ulizosema kuwe na wahadhiri kule, kuwe na nafasi ya kutosha waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la *welfare* kwenye mabweni na kadhalika tunalibeba na tuko *serious,* tunafikiria namna ya kulifanyia kazi. Kwa hiyo, hizi zote ni *point well taken*. Labda niseme kwa upande wa Tunduru kwa sababu Mtwara tumeshazungumza. Mheshimiwa, nisiposema hili maana yake Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru hili amekomaa nalo na ni Mjumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tunduru kikwazo kikubwa kwanza ilikuwa ni ukubwa wa eneo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Kingu, sasa tumepewa eneo kubwa zaidi. *Sokoine University* wanajaribu kumalizia *compensation* halafu baada ya hapo tutaanza kazi. Kwa hiyo, kile ambacho mmekivumilia muda mrefu natumaini baada ya muda kulingana na bajeti

tutakavyopata kwa kadiri tutakavyopata bajeti, Mheshimiwa Kingu tutaona sasa kazi inaenda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, umelisemea hili sana kila mara nikitoka hapa ni hilo hilo umenibana. Nadhani wananchi wa Tunduru wakuelewe, wakusikie, wakupige mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna ya kuhakikisha kwamba tunaongeza elimu ya juu ni kuunga mkono vyuo binafsi. Ndiyo maana hata kwenye mikopo ya wanafunzi tunahakikisha kwamba tunawapa fedha wanafunzi wajichagulie wanaenda kusoma wapi, ilimradi wakidhi vigezo na tunavisimamia vyuo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo tumekuwa tukichukua hatua, tunapoona hawajafikia vigezo. Sasa hivi wameniambia wamekuja Chuo Peramiho pale na Mbunge wa Peramiho namfahamu. Wamenifuata wenye Chuo chao pale kwamba sisi tumeanza kuwekeza, tutapata vigezo vinavyotakiwa, tutafungua tena Chuo Peramiho. Kwa hiyo, nadhani Ruvuma itakuwa siyo na chuo kikuu kimoja tu, pengine siyo viwili tu, lakini hiyo ni juhudi ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, sehemu zote sekta binafsi ikitetereka kidogo, hatupendi kufunga vyuo, hatupendi kabisa kufunga vyuo. Tunapenda kuvishika mkono viendelee, lakini na vyenyewe lazima vituelewe kwamba tunahitaji tusishuke kwenye *standard.* Lazima tujiulize maswali, sasa hivi mwanafunzi ni mtaji kwa chuo. Kwa hiyo, chuo ambacho *source* yake ya *income* ni mwanafunzi, mwanafunzi akifanya vibaya, akiwa *discontinued* ina maana unajinyima mapato kwa chuo binafsi.

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie mkakati, tutafanyaje ili hii *incentive* ya ku-*retain* mwanafunzi ambaye yeye mwenyewe sasa hataki tena kusoma ili kuwa na kipato aendelee kusoma kule? Hili ni muhimu tulifanye au kutoa *marks* kubwa ili wanafunzi waone tukienda huku tunapata *GPA* nzuri sana. Kwa hiyo, vyuo binafsi tutavisimamia, tutavishika, tutaendelea navyo.

Mheshimiwa Spika, naamini huenda Peramiho kikawa Chuo cha kwanza ambacho tutakifungua na hivi vingine ambavyo vimekwama, vimeyumba na vimepata matatizo, tutafanya navyo kazi kwa karibu, na *TCU* itafanya kwa karibu, na Mheshimiwa Mbunge wa Peramiho najua sasa tumemaliza hili suala ambalo nawe umekuwa ukilifuatilia sana.

Mheshimiwa Spika, hebu twende kidogo, na-*pick randomly* sasa hivi, kwenye *VETA*. Nadhani alikuwa Mheshimiwa Dennis Londo alisema sasa *VETA* iende TAMISEMI, ibaki Wizarani au iende wapi? *VETA* ni mamlaka na kama ambavyo vyuo vikuu na hatua zinachukuliwa. Sasa hivi kurudisha ule uhuru wa vyuo vikuu hatua mbalimbali zinachukuliwa, tumezianza lakini kuwa na mamlaka vile vile ina maana siyo idara ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ile inaweza ikafanya kazi vizuri. Tunachohitaji na ku-*demand* kutoka kwenye uongozi wa *VETA* ni kuwa umewa-*robust* kwa sababu *VETA* zitakuwa nyingi sana hapa nchini. Kuwe na usimamizi mzuri na kuhakikisha kwamba zinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shangazi alizungumza kitu ambacho ni muhimu sana. Alijaribu kuonyesha *contradiction* kati ya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 kama ambavyo imefanyiwa marekebisho kadhaa na Sera hii sasa hivi ya Elimu na Mafunzo Toleo la 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna *contradiction* nyingi lakini kwa kweli sheria inatakiwa kuwa zao la sera. Sisi tulivyojua tunabadilisha sera tulisema tusikimbie kwenye sheria mpaka tujue makubaliano kwenye sera tunasema nini? Utaenda kwenye sheria kusema nini? Kwamba elimu ya lazima miaka 10!

Mheshimiwa Spika, hilo linaingia kwenye sheria endapo sera ndivyo ilivyoelekeza. Hapo mengine ya changamoto, tumesema *re-entry program* ambayo nitaizungumzia sasa hivi ambayo ukienda kwenye sheria utakuta ina ukakasi. Mwanafunzi hayuko shuleni siku 90, unamfukuza. Mwelekeo wetu sasa hivi ni kurudisha watoto wote wasome.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi baada ya sera kupita, tumeanza mchakato wa sheria. Mtasikia tu tunakusanya maoni kwa wadau ili twende kwa *AG* kumwuliza anaonaje yale ambayo tunadhani yafanyike, ni sheria mpya au ni marekebisho? Kwa hiyo, hilo tunalifahamu Mheshimiwa Shangazi na baadhi ambao wamezungumza hapa kwa sababu kwa sasa hivi kwa kweli sheria na sera zikikutana, zitagombana kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu tuzungumzie kuhusu *re-entry* kidogo ambayo tumezungumza hapa. Leo hapa wametambulishwa wageni wa Wizara ambao ni ma-*researcher* wanafanya kazi ya *research* aina mbili, moja nilieleza hapa. Moja ni kuhakikisha kwamba takwimu zote za kila Mtanzania zinaingia katika mfumo wa elimu wa *BEST*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi mfumo wa *TCU* utaunganishwa na *NACTVET*, tutaunganisha na Baraza la Mitihani. Wanafunzi hata wakienda kusoma shule ambazo zinatumia *Cambridge Curriculum* itabidi tuwajue, tuwa-*track* wanavyoendelea wakifika chuo kikuu tunataka tujue wanasoma *program* gani ili sasa hivi ukiulizwa wangapi wanasoma *TEHAMA* vyuo vikuu, *degree*? Uweze ku-*click* na kupata taarifa.

Mheshimiwa Spika, kazi inaendelea vizuri sana, inafanywa na wahadhiri wetu wa vyuo vikuu. Tumewakusanya tu, tunawalipa, wanafanya na *support* kidogo ya baadhi ya *donor,* lakini kazi inafanywa chini yetu ili tuweze ku-*trace out.* Maana yake baada ya kazi hii kukamilika ya kuunganisha na takwimu na kuwa tuna *bench mark* na *census,* tutajua kwa ukweli *dropout* ni kubwa kiasi gani kwa haraka haraka tunajua ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaangalia tu wanafunzi walivyoingia darasa la kwanza halafu tunasubiri miaka saba, tukija tukiangalia ni wangapi wamemaliza shule. Hapa katikati kuna mgogoro mkubwa sana, lakini tunajaribu kufanya hiyo tuweze kuwa-*trace*. Lile swali ameuliza Mheshimiwa mmoja kwamba na wale wanaosoma wengine wameacha vyuo vikuu, wameacha kusoma pengine kwa sababu ya mikopo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huo ambao nadhani mwezi wa Sita mwishoni utakuwa umeshaunganishwa, utatusaidia sisi kujua haraka sana nani amejisajili? Ameenda Mzumbe na alisoma miaka mingapi? Ameondoka lini na pengine tutam-*trace out* kujua sababu ya kuondoka kwenda kusoma, lakini tutaenda kuangalia *dropout* kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna timu ndogo inafanya kazi, imepitia Tanga, imeenda Lindi, imeenda Mbeya, imeenda Njombe, iko Dodoma, itaenda Kigoma, itaenda sijui mkoa gani mwingine, imeenda Geita imeenda Mwanza kuwafuatilia wale mabinti ambao waliacha shule kwa sababu ya ujauzito, kuangalia waliorudi changamoto ni zipi na fursa zimekaaje, kuangalia maslahi ya vile vichanga, kuangalia wale ambao hawakurudi, ni kwa nini hawakurudi? Taarifa yenyewe tutaipata. Nadhani itatusaidia zaidi kuimarisha namna ya kuwarudisha hawa mabinti shuleni kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoamini ni kwamba baada ya hapo itakuwa ni kazi kubwa itakayofanywa na timu hii ambayo wanaangalia *re-entry program* kwa *teens pregnancy* na *dropout* ya *boys* kwa ujumla wake kwa nchi nzima kwa sababu kwa kweli ni tatizo kubwa ambalo wanasema ni *elephant in the room, nobody talks about it,* lakini ni *time* ya kuli-*adress* hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……...................Sh. 10,257,937,145

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kuna Waheshimiwa Wabunge hapa wameomba kupata ufafanuzi wa mambo kadhaa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na wakati huo huo Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 123 inazungumzia matumizi ya muda wetu hapa Kifungu cha kwanza na cha pili.

Kifungu cha kwanza kinatukumbusha muda wa kumaliza na kwamba zikibaki dakika 10 tuongeze nusu saa, ikiisha nusu saa tunaingia kwenye *guillotine*. Kanuni yetu mpya inasomwa hivyo. Kwa hiyo, kifungu hiki kina Waheshimiwa Wabunge hapa, ninayo majina yao. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa muda wa kutafuta ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Wakati anatoa maelekezo, ameongelea mambo mengi. Mimi napenda tu kupata ufafanuzi wa dhati na wa kina. Kuna tatizo la wafanyakazi wa vyuo vikuu, idadi inashuka kwa kasi, wahadhiri na wanataaluma, lakini *enrolment* inapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu tulizonazo, *Professors* wanaohitajika kwenye vyuo vyetu vikuu ni 516 lakini tuna 93, *Professors* washiriki 689 lakini tuna 207 na wanataaluma wengineo. Napenda kujua, hii imeathiri hata uwiano wa mwanataaluma na wanafunzi, badala ya mmoja kwa 12 tuna mmoja kwa 43. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi wa Serikali. Serikali ina mkakati gani wa dhati wa kuboresha mazingira ya kufundisha ili ku-*retain Professors* wetu na wanataaluma wabaki vyuoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo ina mkakati gani wa kuzalisha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hoja huwa ni moja.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa kina.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ya kutoa ufafanuzi. Kama alivyoeleza na ilivyoelezwa na Waheshimiwa wengi hapa, tuna kipindi tunapitia sasa hivi kwa vyuo vikuu kwa sababu ya kasi ya kuongeza idadi ya wanafunzi na kwa bahati mbaya sana idadi ya ajira haikuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kidogo kuna wakati ajira zilisimamishwa kwa muda mrefu tu. Kwa hiyo, unakuta wakati mwingine kuna *Professors* wanakaribia kustaafu, lakini ambao wameshapanda kufikia *level* ile bado wapo mbali sana. Serikali sasa hivi inaendelea na utaratibu wa kuwaajiri na sasa hivi tunamalizia kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza mazungumzo ya kuhakikisha kwamba *councils* zinaruhusiwa kuajiri. Hiyo namba moja. Pili, tunapeleka wahadhiri kwenda kusoma hasa kupitia

Mradi wa *HEET* ambapo tunapeleka kwenda kusoma mahali popote hapa nchini. Sasa hivi wahadhiri 516 tayari wameshapata fursa ya kwenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo mojawapo ukiwa umeajiriwa chuo kikuu kama hujapata *Ph.D* huwezi kupanda, hata kama ungekuwa *competent* kiasi gani darasani. Kwa hiyo, kuwapeleka kwa ajili ya kusoma inasaidia kuwa-*unlock* hawa ambao wanakwenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunatoa *incentives* kwa ajili ya wao kuchapisha na kuandika kwa sababu ndicho kigezo cha kupanda. Pia tumeanza kwa upande wa sayansi, elimu tiba na uhandisi, na ninashukuru kwamba hii ilipita katika Bunge lako Tukufu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mbunge hakuonesha kama anaweza akawa hajaridhika au ameridhika. Yeye ameomba tu ufafanuzi na ufafanuzi umeshatolewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtaniwia radhi kidogo, Mheshimiwa Waziri kuhusu hii hoja ya hawa maprofesa ambayo umezungumzia, hivi, kwa Kiswahili *incentive* ni nini?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni motisha.

**MWENYEKITI:** Motisha. Mpaka mtu kuja kufikia kuwa profesa kamili, safari ile ni ndefu sana, halafu muda wake wa kuondoka chuoni ni ule ambao sisi tumeona ni utumishi wa umma, na fedha ambazo mnakuwa mmewekeza, kama mlivyosema hapa, hao mia tano na ngapi mnawapeleka kusoma, waje waanze kupanda wakutane na changamoto alizozisema Mheshimiwa Bashiru, yaani achapishe halafu asubiri miaka mitatu. Yaani hii hoja ikoje? Kwa sababu kitendo cha wao kupungua ni pamoja na hiyo, kwamba watu hawana moyo tena, wanaona bora wakafanye shughuli nyingine, hilo limekaa namna gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hao maprofesa ambao tulikuwanao huko mwanzo walikuwa wana-*publish. Any way, in any case,* hata bila motisha ambayo tumeianzisha sasa hivi, kwa hiyo, hii ni *added advantage* tu. Hii *publication* ni kwenda ku-*publish* kwenye *journals* kubwa, kwa sababu *incentive* nyingine ambayo naweza nikaiita *disincentive* ni kujaribu ku-*publish* kwenye majarida ambayo *scrutiny* yake siyo *rigorous* sana ili kuwahi kupata *promotion*. Kwa hiyo, vile vile tuna-*encourage* kama wanaweza wakakaa wakafanya kazi na wakapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshangaa mpaka Chuo cha Mipango watu wame-*publish* katika *Journals* ambazo ni *top* na wamepata hii motisha. Hii ni *step* moja tu, hii haileti utatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo natakiwa niliseme, mazungumzo yanaendelea kuhusu kuwa-*retain* maprofesa vyuo vikuu, kwa wale ambao kweli wataonesha wako *active* kwenye *academia beyond* ule muda ambao sasa hivi wanaweza wakastaafu, kwa sababu kwa kweli maprofesa wengine wanafikisha hadi miaka 80 bado wako *active,* wana *publish* na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya kuweza kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Niseme tu kwamba sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri isipokuwa tu naomba ufafanuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ya muda mrefu. Naishukuru Serikali kwa sababu mara zote imekuwa ikinipa tumaini kwamba ni hoja ambayo inafanyiwa kazi ambayo inahusiana na utolewaji wa mikopo ya elimu ya juu kama ruzuku kwa watu wenye ulemavu. Sasa nilikuwa naomba kufahamu kwamba, ule mchakato ambao nimekuwa nikiambiwa kwamba hiyo hoja iko kwenye mchakato, ni lini mchakato huo utakamilika? Ama kwa sasa hivi iko kwenye hatua gani, na ni lini mchakato huu utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiiomba Serikali, kwa sababu kama tunavyofahamu ulemavu ni gharama, sasa mtu anapoanza kazi anaanza kukatwa na ule mkopo aliochukua. Natolea mfano wa aina nne za ulemavu; mtu asiyeona atahitaji msaidizi amlipe, hapo hapo alipe na ule mkopo, atahitaji maisha mengine yaendelee, lakini mtu mwenye ualbino anunue mafuta, mtu mwenye ulemavu wa viungo anahitaji vifaa visaidizi, atahitaji *wheelchair* na pengine anahitaji bajaji au gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu mchakato huu umefikia hatua gani, na ni lini utakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Stella Ikupa amekuwa akilifuatilia jambo hili muhimu sana kwa muda mrefu. Kwa sasa hivi ulemavu ni kigezo muhimu sana cha kuhakikisha kwamba wanapewa mkopo 100% kama *qualification* nyingine za kuingia chuo kikuu, unazipata. Sasa hivi tunapitia vigezo vyote, na ni kama ilivyoelezwa humu ndani kwenye Bunge lako Tukufu. Bado kuna malalamiko kwamba tunatumiaje vigezo hivi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anayestahili zaidi anapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati wa kupitia tutamwomba Mheshimiwa Stella Ikupa ashirikiane nasi ili tupitie, tuangalie uwezekano wa kuingiza hiyo kama kigezo, kwa sababu anachokisema ni kwamba wale tuwape *scholarship* moja kwa moja. Ninadhani ni hoja yenye uzito mkubwa lakini nafikiri twende nayo wakati tunamalizia mageuzi yote ya vigezo vya kupata mkopo au ufadhili wa 100%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi pia sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ninaufahamu uchapakazi wake na nia yake ya kusimamia utekelezaji wa mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipate ufafanuzi wa Serikali, na Waheshimiwa wengi wakati wanachangia wameonesha wasiwasi wao kwamba sera na mtaala ni kitu ambacho kinakwenda kutukomboa kwa sababu, unatoa maarifa mapya na ujuzi ambao wahitimu watakwenda kuajiriwa na kujiajiri; lakini changamoto kubwa ni ugharamiaji wa hii sera na huu mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza maelezo ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri bado hupati maelezo ya kina kwamba fedha ziko wapi za kugharamia kitu hiki kikubwa ambacho kina maslahi mapana kwa nchi yetu. Kwa hiyo, nilitaka nipate ufafanuzi wa Serikali, je, ina mkakati gani wa kupata fedha za kutosha kugharamia sera hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu maandishi yaliyopo Wizarani kwa miaka kumi ya mwanzo inahitajika shilingi trilioni 5.5 kwa kila mwaka ili waweze kujenga shule mpya, tuwe na maabara ambazo zina vifaa vya kutosha na tuwa-*train* walimu wote na siyo vipande vipande au idadi ya walimu wachache kutoka shuleni. Ili mtaala huu utekelezeke vizuri, tuepuka makosa tuliyoyafanya kule mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule mwanzoni wakati tunafanya maboresho ya mtaala tulihama kutoka kwenye *content based* kwenda kwenye *competence based*, Mhamo wa ruwaza, tuka-*train* walimu wachache kila shule, kitu ambacho ufanisi wake ulikuwa mdogo na mtaala haujatekelezeka ipasavyo. Tunataka walimu wote wanaotekeleza mtaala wapate hayo maarifa mapya ya namna ya kuutekeleza. Sasa je, Serikali imejiandaaje ili kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mtaala huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi. Naona Waziri wa Fedha anataka kueleza namna alivyojipanga kugharamia. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza maelezo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri

Profesa Mkenda pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba jambo hili Serikali imelibeba kwa ukubwa wake na limeshapita katika ngazi zote za kiserikali. Kwa maana hiyo, Serikali inaweka jambo hili kwenye vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokifanya, sasa hivi tumeweka kwenye bajeti hii, na pia tunaendelea kufanya *alignment* za ndani ya Serikali, na tunaendelea kufanya mazungumzo na wadau wetu wa masuala ya kifedha na mazungumzo yanaendelea. Tunaamini hata tutakapokuja kwenye hotuba kuu ya Serikali kuna tamko ambalo tutaendelea ku-*cement* haya ambayo yalisemwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna mazungumzo mengine ambayo bado tunaendelea nayo, yatakayowezesha kwenda sambamba na ukubwa huo ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema. Serikali inatambua kwamba hiki ni kipaumbele, na kwamba ni kweli gharama yake ni kubwa, lakini faida yake ni kubwa zaidi kuliko gharama itakayoongezeka kwenye hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitegemei kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri ila nataka ufafanuzi katika suala la usajili wa shule nchini. Wananchi wanajenga shule za awali, shule za msingi na shule za sekondari, lakini Wizara imekuwa na ukakasi wa kutokuzikuzisajili hizi shule nchi nzima. Je, hili suala ufafanuzi wake umefikia wapi katika kuzisajili shule hizi? Maana imekuwa taabu kwa wananchi. Tunawatesa wananchi ilhali haki ya kujenga shule ni suala la Serikali. Wananchi wamejitolea kujenga shule na ninyi mna-*lock* kutokuzisajili. Tunaomba ufafanuzi wa Serikali katika jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kueleza hili. Tulishazungumza na Mheshimiwa Tabasam hata kwenye bajeti iliyopita. Ni kwamba wale wanaosajili shule wanaangalia vigezo. Hatutaki kuvilegeza vile vigezo, lakini wananchi wanapojenga shule ambayo ingejengwa na Serikali halafu wakawa wamebakiza kitu kimoja, labda choo au labda kuna vitu vidogo vidogo vimebaki, msimamo wetu ni kwamba wale wanaotakiwa kusajili watoe taarifa kwetu, sisi Serikali tumalize ile nguvu ya wananchi. Hii itahimiza wengine kufanya vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilifanya ziara maalum Sengerema na kwa ndugu yangu Mheshimiwa Erick Shigongo, kule Buchosa, kwa sababu kule wananchi wanajitolea sana kujenga shule. Tumeipeleka Mamlaka ya Elimu Tanzania, wamekwenda kule kuzikagua kwa ajili ya kutoa fedha za kumalizia nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi kujitolea katika masuala ya elimu, na unapojitolea tutajitahidi kuja kukushika mkono. Japo Serikali ina wajibu wa kufanya kazi hii, lakini wananchi wakijitolea wanatusaidia sana. Kwa hiyo, wale wote ambao wanafanya kazi kama hiyo ya kujenga shule ambazo ni za umma, usajili wake tutauharakisha kwa sisi kwenda kumalizia ile kazi ambayo inakwamisha ule usajili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kipengele hiki tunazungumzia sera, ninaona hata Mheshimiwa Waziri katika hivi vipengele vyake ameweka vipaumbele ambavyo vitamsaidia kutekeleza sera. Nitazungumzia eneo moja tu la ugharamiaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tumekuwa tukizungumza kwamba bajeti ya Wizara ya Elimu sehemu kubwa sana, 60% inakwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu, nao wanai-

*term* kama miradi ya maendeleo, na 40% peke yake ndiyo inakwenda kwenye ile miradi ya maendeleo; kuna zile *OC* na kuna miradi yenyewe ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini Serikali wamekubali kujibana kwenye kutekeleza sera yake kwenye vipaumbele vyake kwa kuunganisha fungu kubwa zaidi ya 60% kwenye miradi ya maendeleo na kutolitengea fungu la mikopo ya elimu ya juu *vote* yake peke yake; yaani fungu peke yake ili sasa aidha tulifanye liwe *revolving* ili watu walipe lijiendeshe ili tuseme miaka hii kumi tutatoa pesa kiasi hiki kwa ajili ya mfuko, baada ya hapo watu wa mfuko kusanyeni madeni, jiendesheni, au tuliwekee fungu lake ili tuone tunalitafutiaje fedha kwa ajili ya kuliendesha? Nilitamani kujua ni kwa ni Serikali haioni hoja hii kama ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kushika shilingi, ila nilitamani kujua tu msimamo wa Serikali kwenye hili kwa sababu ni la msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mbunge ina mantiki. Hata sisi kwenye mjadala kuhusu kupangilia kipi kiwe kwenye *development expenditure* na kipi kiwe kwenye *other charges,* bado tuna-*debate*. Hata wiki hii tulikuwa na *mission* na wenzetu wa *IMF* na hiyo ilikuwa ni sehemu ya mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie, tulichukue hili jambo kwa sababu lina *technicalities* zake, lakini kimsingi kama Serikali tunatamani tuongeze bajeti kwenye masuala ya maendeleo ya kisera kwenye maeneo mengine, ndiyo maana mmeona bajeti ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia aliongeza kwenye ujenzi wa vyuo na maeneo mengine. Pia ni kweli ukirudi kwenye *literatures,* uwekezaji kwenye elimu ni sehemu ya bajeti ya maendeleo. Kwa hiyo, tuna *debate* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Nusrat aridhie tulipokee, tutaendelea kukaa na mwalimu wangu wa

Uchumi, Mheshimiwa Prof. Mkenda tukubaliane na wenzetu tunaofanyanao kazi za kupangilia namna ya kuweka hizi bajeti *items* ili bajeti ya maendeleo kwenye maeneo mengine isiathiriwe na kuongezeka kwa bajeti ya mikopo ya elimu ya juu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..…….Sh. 1,645,424,501
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…...............Sh. 2,244,377,500
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……........................Sh. 1,325,412,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…......Sh. 868,585,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*.....Sh. 663,291,000
Kifungu 1007 – *Legal Unit*…………………………........…Sh. 656,749,000
Kifungu 1008 – *Information, Communication, Technology and E-learning*…………..………………Sh. 898,918,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…......Sh.1,205,756,499
Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*..............................................Sh. 85,701,925,504
Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*…....……Sh. 56,471,589,659
Kifungu 7001 – *Higher Education*……….…………Sh. 345,357,282,798
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*................................Sh. 68,560,536,189
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*….............................……Sh. 59,329,921,005

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 18 – TUME YA TAIFA YA UNESCO**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 2,882,154,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 – WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………………Sh. 1,150,000,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………Sh.1,694,945,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…………..…Sh. 72,167,012,321
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…....……………………Sh. 722,718,475
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*….Sh. 776,621,295
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..….Sh.16,653,826,518
Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*……………….......…………Sh. 152,096,303,599
Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*…………..Sh. 7,593,962,695
Kifungu 5001 – *Teachers Education*……………..........……………Sh. 0
Kifungu 7001 – *Higher Education*…………......……Sh.941,709,991,534
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*……………………Sh. 120,433,829,349
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*……..............................…Sh. 13,043,463,214

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge likikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri na sasa nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. baada ya kuwahoji na ninyi kusema ndiyo, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Wizara yake inayohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na viongozi wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya. Tunawatakia kila la heri katika kutekeleza yale ambayo mmewaahidi Waheshimiwa Wabunge hapa, nao wamewapitishia makadirio yenu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo namshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, anafanya kazi nzuri sana; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati. Jambo la Elimu ni jambo zito nani la muhimu sana kwa Taifa letu, nao wanatusaidia. Kwa hiyo, Mwenyekiti tunakushukuru sana na Kamati yako yote na Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmepata nafasi ya kutoa mawazo yenu. Kwa kweli mmetoa mawazo mengi na Mheshimiwa Waziri kama alivyosema hapa, hajaweza kuwajibu wote lakini amezichukua hoja zenu na

ataendelea kuzifanyia kazi ili kuhakikisha sekta hii ya elimu inakaa sawa, na sote tunakuwa na uelewa wa pamoja kwa ajili ya kusogeza Taifa letu mbele.

Mheshimiwa Waziri, kama nilivyosema awali kwamba hii ni Wizara ambayo ningetaka nikae kule ili nichangie, lakini kwa sababu sikukaa kule na kwa hivyo sikujipa nafasi ya kuchangia, ni dhahiri kwamba Waheshimiwa Wabunge sote tunafahamu mwelekeo wa nchi yetu na kwa kweli tunayo Mawazo, tunatamani wapi paendelee kuwa bora. Mengine tunaendelea kufuatilia haya mambo mapya ambayo Wizara inaendelea kuyaleta ili elimu yetu ikae vizuri. Kwa hiyo, tuendelee kutoa mawazo ili Wizara nayo iendelee kuyafanyia kazi kadri tunavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, mawazo ambayo ningechangia kama ningekaa kule, nitayachangia kwa sura hiyo na siyo kwa kusimama hapa mbele, kwa sababu la sivyo. Mheshimiwa Waziri ataona amepewa maelekezo. Kwa hiyo, nitampa mchango wangu wakati utakapofika. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yote mliyoitoa na kwa kweli mmefanya kazi kubwa sana, sana, sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja tu ambalo naweza kulizungumza hapa mbele ni kuhusu *IDM* ambayo nadhani kwa Kiswahili Fasaha ni Chuo cha Uongozi na Maendeleo au Chuo cha Uongozi wa Maendeleo, kimojawapo katika hayo; lakini kwa sababu mmeanza na huu utaratibu wa hivi vyuo na shule kwa ajili ya mafunzo haya ya amali, ni muda sasa wa kuanza kutafakari kama kile chuo kirejee. Kwa nini? Kwa sababu kilikuwa kinafundisha kuhusu uongozi wa maendeleo.

Nafikiri na nchi yetu tumeshafika mahali ambapo kile chuo ama ile taasisi irejee mahali pake. Kwa sababu sasa hivi tunaona kuna mahali yaani kumetoboka katika uongozi ndani ya nchi yetu na ninafikiri mojawapo ni kwa sababu hatuna chuo cha namna ile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, pengine tunafikiri ile *Uongozi Institute* ingeweza kushughulika na haya, lakini nadhani inafanya kitu tofauti kabisa na iliyokuwa *IDM*. Kwa hiyo, hilo tu ndilo naomba nilizungumze hapa mbele ili muone namna ambayo mnaweza kuanza kufanya utafiti kwa sababu mmesema mlitambulisha watafiti hapa na hilo kama siyo muda muafaka wa kurejesha, lakini mliangalie ili watu waende kule wakajifunze uongozi huo unaohusu maendeleo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.04 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Mei, 2024 Saa Tatu asubuhi)*